HADITHI YA ALLAN QUARTERMAIN



H. Rider Haggard

HADITHI YA ALLAN QUARTERMAIN



H. Rider Haggard

HADITHI YA UMSLOPAGAAS

Muandishi: H. Rider. Haggard, 1887

Mtafsiri: F. Johnson na E. W Brenn.

MAAJABU YALIYOWAPATA ALLAN QUATERMAIN NA WENZAKE

YALIYOMO

Sura ya 1

Sura ya 2

Sura ya 3

Sura ya 4

Sura ya 5

Sura ya 6

Sura ya 7

Sura ya 8

Sura ya 9

Sura ya 10

Sura ya 11

Sura ya 12

Sura ya 13

Sura ya 14

Sura ya 15

Sura ya 16

Sura ya 17

Sura ya 18

Sura ya 19

Sura ya 20

Maelezo ya bwana George Curtis

SURA YA KWANZA

SIKU saba zilikuwa, zimepita tangu mwana wangu mpenzi alipozikwa na jioni ilipofika, nilikuwa Nikitembea huko na huko chumbani mwangu nikifikiri, mara mlango unabishwa, Nikaenda nikaufungua mlango mwenyewe, Kumbe rafiki zangu wa zamani Sir Henry Curtis na Bwana John Good wapo nje.

Niliwakaribisha ndani wakaingia chumbani. Wakakaa mbele ya moto uliokuwa ukiwaka humo.

‘’Mmefanya vyema kuja kunitazama.’’

Hawakujibu neno, ila Sir Henry alishindilia tumbako katika kiko chake akakiwasha kwa kaa alilolitoa motoni, Alipokuwa akiinama mbele kufanya hivyo moto, uliwaka zaidi ukaangaza chumbani, nikafikiri jinsi alivyo mtu mzuri mno.

Uso wake mtulivu wenye nguvu, sura yake thabiti, macho yake makubwa ya kijivu ndevu na nywele zake rangi ya manjano.

Sura yake yote ilikuwa ya mtu aliye bora, tena umbo lake halikuwa kinyume cha uso wake, Sijapata kuona mabega mapana, zaidi wala kifua kinene kama chake.

Umbo la Sir Henry ni pana, ingawa ni mrefu wa futi sita na inchi mbili lakini haonekani kuwa mrefu nilipokuwa nikimtazama hivi, sikuweza kujizuia nisifiri namna mimi nilivyo mwembamba mfupi na namna nilivyohitilafiana na uso wake mzuri, na umbo lake bora.

Embu wazeni basi juu ya mtu mfupi aliyesinyaa, mwenye uso wa rangi ya manjano na umri wa miaka sitini na mitatu mwenye mikono myembamba, macho makubwa ya kahawia, kichwa kimefunikwa na nywele zinazoingia mvi na kusimama wima kama brashi iliyotumika, kiasi uzani wake pamoja na mavazi aliyovaa ratili mia moja thelathini na mbili tu.

Basi hapo ndipo mtakapofahamu namna alivyo Allan Quatermain, ambaye kwa desturi huitwa Mwindaji Quatermain, na Waafrika humwita ‘’Makumazahn,’’ maana yake akeshaye usiku, yaani mtu mwerevu asiyedanganyika.

Tena, yupo Bwana Good ambaye hafanani na Sir Henry wala na mimi maana ni mfupi, mweusi kidogo, mnene mnene sana ana macho meusi yang’aayo na katika jicho moja siku zote huvaa rodi, yaani miwani ya jicho moja.

Nilisema yeye ni mnene, lakini neno hilo halitoshi kueleza namna alivyo mnene. Sir Henry humwambia ya kuwa amenenepa hivi kwa sababu yu mvivu, tena anakula sana, ingawa Bwana Good hapendezwi kwa maneno yake, lakini hawezi kuyakana.

Tulikaa kwa muda mfupi, kisha niilichuka kiberiti ili niiwashe taa, kwa sababu niiona giza linachosha, maana ndivyo inavyoelekea hasa ikiwa muda wa siku saba tu umepita tangu mtu alipozika tumaini la maisha yake.

Huku nyuma Sir Henry na Bwana Good walikuwa wamekaa kimya, wakiona nadhani, ya kuwa hawana la kusema linaloweza kunifariji, wakaridhika kunifariji kwa kuwapo kwao na rambirambi zao za kimya.

Ni kweli ya kuwa twapata tumaini na faraja katika saa za majonzi kwa kuwapo wengine, wala si kwa maongezi yao ambayo huelekea kutuudhi tu. Wakakaa wakivuta tumbako, na mimi nilisimama mbele ya moto nikivuta tumbako pia na kuwaangalia.

Halafu kidogo nilisema, ‘’Je rafiki zangu wa zamani, tangu tuliporudi toka nchi ya Ukukuana hata leo, miaka mingapi imepita? ‘’Bwana Good akasema, ‘’Miaka mitatu. Kwa nini unauliza?’’.

Nikajibu, ‘’Nauliza kwa sababu nafikiri ya kuwa muda niiokaa pamoja na watu mijini umenitosha kabisa, Nitarudi mwituni tena.’’

Hapa Sir Henry alikipeleka nyuma kichwa chake, akacheka mcheko wake wa kindani, akasema, ‘’Ama ni ajabu sana, sivyo Good?’’

Bwana Good akaniangalia, na huku anacheka katika rodi yake, kama kwamba anaficha siri, akasema, ‘’Ndiyo, ajabu sana ajabu kweli kweli.’’

Mimi ni mtu asiyependa mafumbo na mambo ya sirisiri, basi niliwatazama mmoja mmoja, kisha nikasema, ‘’Siwezi kufahamu vizuri,’’

Sir Henry akasema, ‘’Hufahamu? Basi, nitaeleza. Good na Mimi tulipokuwa tukija hapa tuliongea.’’

Nikayakatiza maneno yake kwa ukali kidogo, nikasema, ‘’Nadhali kama Good alikuwapo, hamkosi mliongea maana Good ni mtu apendaye sana maongezi. Je, mliongea habari gani?’’

Sir Henry, akauliza, ‘’Ee wafikiri tuliongea habari gani?’’

Nikatikisa kichwa changu.

Haiwezekani nikajua Good aliongea nini, maana mara nyingi huongea habari za mambo mengi.

Sir Henry akasema, ‘’Tuliongea juu ya shauri dogo nililoliwaza yaani kama wewe utakubali tutafunga mizigo yetu na kuiendea nchi ya Afrika kufanya safari nyingine,’’

Nilipoyasikia maneno yake, nilishtuka sana, nikasema, ‘’Ni kweli usemayo?’’ akajibu, ‘’Ni kweli, na Good naye amekubali pia, sivyo Good?’’

Na yeye akaitikia, ‘’Ndiyo.’’

Basi, Sir Henry akaendelea, na sauti yake ilionyesha namna anavyoona hamu, akasema, ‘’Nami pia nimechoka kukaa bure kiubwana katika nchi iliyokinai mabwana.

Kwa muda wa mwaka mzima na zaidi nimekuwa nikitukutika kama tembo mzee anusaye hatari.

Kila mara ninaota ndoto za nchi ya Ukukuana, na bibi kichawi Gagula, na Mashimo ya Mfalme Sulemani. Nakuambia ya kuwa nimenaswa na hamu

nisiyoweza kuieleza.

Nimechoka kupiga kanga na kwale, na sasa nataka kuwinda wanyama wakubwa. Mwaka ule mmoja tuliokaa pamoja katika nchi ya Ukukuana huonekana kama kwamba thamani yake inapita thamani ya jumla ya miaka yote ya maisha yangu.

Labda ni mpumbavu kwa hamu ninayoiona, lakini sina nguvu kuishinda, natamani kwenda, tena sina budi kwenda.'' Basi alisita kidogo, kisha akaendelea..

''Tena, kwa nini nisiende? Sina mke wala baba, wala mama, wala mtoto wakunizuia nisiende. Nikipatikana na ajali, cheo changu na Mali itarithiwa na ndugu yangu George na mwanawe, nao watairithi kwa vyovyote.

Mimi si kitu kwa mtu yeyote.'' Akasema,

''Ah! Nilifikiri utasema hayo. Na wewe Good, mbona wewe unataka kusafiri, unayo sababu?''

Bwana Good, akasema na huku anajizuia asicheke, ''Ndiyo, ninayo sababu. Mimi sifanyi neno bila kuwa na sababu. Lakini ukitaka kujua sababu ya kweli, nitakwambia, ingawa sipendi kukuambia. Ninaanza kuwa mnene zaidi!''

Basi, nilitia moto kikoni, maana ulikuwa umezimika, ndipo niliposema tena, nikauliza, ''Ninyi mmepata kusikia habari za mlima Kenya?''

Bwana Good akajibu, ''Sipajui mahali hapo.''

Nikauliza tena, ''Mmepata kusikia habari za kisiwa kiitwacho Lamu?''

Bwana Good akajibu, ''La. Ngoja si mahali palipo kaskazini ya Unguja kadiri ya maili mia tatu?''

Nikasema, ''Ndipo. Sikilizeni. Shauri langu ni hili.

Twendeni Lamu, na kutoka huko tutasafiri ndani ya nchi kadiri ya maili mia mbili na hamsini mpaka mlima Kenya. Kutoka mlima Kenya tuendelee

mbele tena kusikia habari zake. Kumbuka Mashimo ya Mfalme Sulemani.’’

Kadiri ya majuma kumi na manne yamepita tangu tulipoongea hivyo, na sasa habari hizi zinatokea katika mahali pa namna nyingine kabisa.

Baada ya kufikiri na kuhojiana sana habari, tuliona ya kuwa itafaa kuianza safari yetu kuuendea mlima Kenya mahali karibu na mlango wa mto Tana, wala si Mombasa.

Basi, ikatokea ya kuwa tulipofika Lamu, tuliteremka pwani pamoja na vitu vyetu vyote, na kwa kuwa hatukujua mahali pa kwenda, tulikwenda moja kwa moja mpaka nyumbani kwa Bwana Balozi wa Serikali ya Kiingereza, tukapokewa kwa ukarimu.

Lamu ni mahali pageni kabisa, lakini mambo yanayodumu katika fikira zangu hata leo ni uchafu wake na uvundo wake. Hasa uvundo wake ni mno. Mbele ya jumba la Bwana Balozi ni pwani, au tuseme fungu la matope liitwalo pwani.

Maji ya bahari yapwaapo huacha nafasi wazi , ndipo mahali panapotupwa taka zote za mji. Pia, hapo wanawake huja wakafukia nazi katika matope na kuziacha humo mpaka makumbi yaoze, ndipo huja kuyafukua na kuzitumia nyuzinyuzi zake, yaani usumba, kutengenezea busati na vitu vinginevyo.

Kwa kuwa mambo hayo yameendelea kwa vizazi na vizazi, ni heri hali ya pwani hiyo ilivyo iwaziwe tu kuliko kuelezwa. Katika siku za maisha yangu nimepata kunusa harufu mbaya nyingi, lakini harufu kali iliyotoka pwani ya Lamu tulipokuwa tumekaa juu ya gorofa ya Bwana Balozi inazifanya zote ziwe kama si kitu kabisa.

Si ajabu ya kuwa watu hushikwa na homa Lamu. Lakini hata hivyo mahali hapo pana uzuri wa namna yake ingawa labda utamchosha mtu upesi.

Basi, tulipokwisha kula, tulikaa tukavuta tumbako, na rafiki yetu Balozi mkarimu aliuliza, ‘’Je, ninyi mabwana mnakwenda wapi?’’

Sir Henry akajibu, ‘’Tumekusudia kuuendea mlima Kenya, kisha, kuendelea mbele mpaka mlima Lekakisera. Quatermain amesikia hadithi ya

kuwa liko taifa la watu weupe wanaokaa katika nchi za mbali zisizojulikana bado, kupita huko.’’

Bwana Balozi aliyatega masikio yake, akajibu ya kuwa hata na yeye amepata kusikia habari kama hizo.

Nikamuuliza, ‘’je, umesikia nini?’’ Akajibu, ‘’Si nyingi, ila najua ya kuwa zamani, kadiri ya mwaka mmoja, nilipata barua kutoka kwa Bwana Mackenzie, mtu wa misioni anayekaa mahali mwisho wa mto Tana panapofikiwa na mitumbwi, naye alitaja habari hizo.’’

Nikamuuliza, ‘’Je, unayo barua hiyo?’’

Akasema, ‘’La, niliitatua; lakini nakumbuka alisema ya kuwa mtu mmoja alifika kwake akasema kwamba alikwenda mbali kadiri ya safari ya miezi miwili kupita mlima Lekakisera, ambao hapana mtu mweupe aliyeufikia yaani kwa kadiri nijuavyo mimi akavumbua huko ziwa liitwalo Laga.

Kisha akaendelea upande wa mashariki ya kaskazi, safari ya mwezi mzima kuvuka jangwa na mbuga na milima mirefu, mpaka alipofika nchi wanapokaa watu weupe wakaao katika nyumba za mawe.

Huko alipokewa kwa ukarimu akakaa kwa muda, mpaka makuhani wa nchi ile walipo chochea habari ya kuwa yeye ni shetani, basi watu wakamfukuza, akasafiri muda wa miezi minane hata akafika mahali alipomkuta Bwana Meckenzie, alikuwa hoi taabani.

Basi, hivyo ndivyo nilivyosikia, na hizo ndizo habari ninazozijua. Mimi nasadiki ya kuwa ni uwongo mtupu lakini ukitaka kujua habari zaidi, afadhali uufuate mto Tana mpaka mahali hapo anapokaa Bwana Mackenzie, ukamuulize yeye habari hizo.’’

Sir Henry na mimi tulitazamana, maana sasa tumekwisha pata habari za kuzithibitisha zile tulizokwishazisikia. Nikasema, ‘’Nadhani tutakwenda kwa Bwana Mackenzie.’’

Bwana Balozi akasema, ‘’Vyema, ni shauri linalowafaa zaidi, lakini nawaonya ya kuwa labda safari yenu itakuwa ya matata, maana nimesikia

kuwa Wajivuni wanatembeatembea huko, nao kama mjuavyo si watu wapole.

Shauri litakalofaa zaidi ni kuchagua watu wachache wenye sifa nzuri wawe watumishi na wawindaji wenu na kuajiri wapagazi kuichukua mizigo yenu toka mji mpaka mji.

Jambo hili litawasumbua, lakini nadhani litakuwa shauri jema na rahisi kuliko kuajiri wapagazi kufuatana nanyi safari nzima, tena udhia wa wapagazi kutoroka utapungua.’’

Kwa bahati yetu, walikuwapo Lamu askari wa Kikazi wachache. Wakazi wamefanana na Wajivuni ni watu hodari wenye nguvu, wenye tabia nyingi njema kama zile za Wazulu, tena ni wawindaji hodari.

Watu hawa walikuwa wamekwenda safari ndefu pamoja na Mwingereza aliyetoka Mombasa akasafiri kuuzunguka mlima Kilimanjaro.

Mwingereza huyo maskini alikufa kwa ugonjwa wa homa wakati alipokuwa akirudi. Alikuwa amekwisha fika karibu na Mombasa; ilibaki Safari ya siku moja tu.

Basi, wawindaji wake walimzika, kisha wakaja mpaka Lamu katika jahazi.

Rafiki yetu Bwana Balozi alitushauri afadhali tujaribu kuwaajiri watu hao, na kwa hivi asubuhi yake tulifuatana na mkalimani wetu tukaenda ili tujaribu kupatana nao.

Tuliwakuta katika nyumba mwisho wa mji. Watatu walikuwa wamekaa nje ya nyumba, nao walikuwa watu wazuri wanaonekana kama kwamba wanaweza kutumainiwa.

Tuliwaambia sababu tuliyowaendea, na kwanza hawakukubali hata kidogo. Walisema ya kuwa hawawezi kabisa kwenda pamoja nasi, ya kuwa wamechoka kabisa kwa safari ndefu, tena mioyo yao ni mizito kwa kufiwa na bwana wao. Walikusudia kurudi makwao wakapumzike kwa muda.

Nikawauliza wenzao wako wapi, maana niliambiwa ya kuwa wako sita, na hapo ni watatu tu. Mmoja wao akasema, ‘’Wamo ndani ya nyumba wamepumzika baada ya taabu waliyopata. Usingizi unawaelemea machoni ni bora walale usingizi, maana usingizi huleta usahaulifu.’’ Lakini walikubali kuwaamsha.

Baadaye kidogo wale watatu wengine walitoka nyumbani, wanapiga miayo watu wawili wa kwanza walikuwa wa kabila lile lile na namna ile ile ya wale tuliowakuta wamekaa nje ya nyumba, lakini Yule watatu alinifanya nishtuke mno.

Alikuwa mtu mrefu sana, nakisia urefu wake ulikuwa kadiri ya futi sita na inchi tatu, lakini mwembamba, na viungo vyake vilikuwa na nguvu kama nyuzi za chuma.

Mara nilipomtazama nilitambua ya kuwa huyu si Mkazi ni Mzulu halisi. Alitoka, na huku ameuweka mkono wake mwembamba mbele ya uso wake kukiziba kinywa chake alipokuwa akipiga miayo, nikaona ya kuwa ni mtu mzima, naye ana shimo lenye pembe tatu katika paji la uso wake.

Kisha, aliuondoa mkono wake, nikaona uso wa nguvu wa Kizulu, na kinywa cha ucheshi, na ndevu fupi zenye mvi kidogo, macho ya kahawia makali kama ya mwewe.

Nikamtambua mara ile, ingawa nilikuwa sijamwona kwa muda wa miaka kumi na miwili. Nikasema kwa sauti ndogo kwa lugha ya Kizulu, ‘Hujambo Umslopogaas?’’

Mtu huyo mrefu, ambaye hadithi zake nyingi zilisimuliwa katika nchi ya Wazulu, na ambaye katika watu wake huitwa ‘’Gogota,’’ na ‘’Mchinjaji’’ alishtuka, na shoka lake la vita lenye kipini kirefu lilikuwa karibu kumponyoka kwa mshangao.

Mara ile alinitambua akawa ananiamkia.

‘’Mkuu, mkuu wa zamani. Mkuu, mkuu! Baba! Makumazahn, mzee mwindaji, muuaji wa tembo, mla simba, mwerevu akeshaye! Hodari,

mwepesi! Ambaye risasi zake kabisa hazikosi shabaha, apigaye shabaha ya kweli, rafiki mwaminifu.

Mkuu! Baba! Ile methali ya kikwetu isemayo ‘’Milima haikutani lakini wanadamu hukutana,’ ni ya kweli kabisa na yenye busara.

Tazama! Tarishi alikuja toka Natal, akalia, ‘Makumazahn amekufa! Nchi haitamwona Makumazahn tena.’ Haya yalitokea zamani sana.

Na sasa, tazama hapa katika nchi ngeni ya harufu mbaya namwona tena Makumazahn, rafiki yangu.

Ndiye bila shaka. Manyoya ya mzee mbweha yameingia mvi; lakini macho yake na meno yake ni makali kama zamani.

Ha! Ha! Makumazahn, unakumbuka namna ulivyoipeleka risasi katika jicho la nyati aliyekuwa akishambulia, unakumbuka?’’

Basi, nilikuwa nimemwacha aendelee hivyo, kwa sababu niliona ya kuwa wale Wakazi watano walionekana kwamba wanaweza kufahamu maneno mengine katika yale aliyosema, tena yanawatia fikira, lakini sasa niliona inafaa kumnyamazisha, maana hakuna kitu kinachonichukiza kuliko desturi ile ya Wazulu iitwayo kubonga, yaani kusifu kupita kiasi.

Nikasema, ‘’Nyamaza! Ala, maneno yako yenye kelele yamezibwa tokea tulipoachana, na hii ndiyo sababu yanabubujika na kutughalikisha hivi? Unafanya nini hapa pamoja na watu hawa, wewe ambaye tulipoachana ulikuwa mfalme katika nchi ya Wazulu?

Umekujaje hapa katika nchi iliyo mbali na kwenu, na kukaa pamoja na wageni?’’

Umslopogaas aliliegemea shoka lake refu la vita, ambalo kipini chake ni kipande kizuri cha pembe ya kifaru, na uso wake ulikuwa umejaa huzuni, kisha akawatazama wale Wakazi, akasema, ‘’Baba yangu, ninazo habari nitakazokuambia, lakini siwezi kusema mbele ya watu wanyonge hawa maneno yangu ni baina ya mimi na wewe tu..

Baba yangu, nitasema haya tu: Mwanamke alinihaini mauti, akalifunika jina langu kwa aibu, ndiyo, mke wangu mwenyewe, mwanamwali mwenye uso kama mwezi, alinihaini, lakini niliokoka na mauti, ndipo nilipoponyoka katika mikono ya wale waliokuja kuniua.

Nilipiga mapigo matatu tu kwa shoka langu hili Inkosikazi hakika baba yangu atalikumbuka, moja upande wa kuume, moja upande wa kushoto, na moja mbele yangu, niliwaacha watu watatu wamekufa.

Kisha, nilikimbia, na kama baba yangu ajuavyo, ingawa mimi ni mzee, lakini miguu yangu ni myepesi kwenda mbio kama ile ya paa, wala hapana mtu anayeweza kunigusa tena nikisha mtoka mbavuni pake.

Mbele nilikimbia, na matarishi wa mauti waniandama nyuma, na sauti zao zilikuwa kama sauti za mbwa wanaowinda. Kutoka nyumbani kwangu nilikimbia, nikampita yule aliyenihaini, alikuwa akiteka maji kisimani.

Nilimpita upesi kama kivuli cha mauti, na nilipokuwa nikipita nilimpiga dharuba moja kwa shoka langu, tahamaki! Kichwa chake kilimtoka, kikaanguka kisimani. Kisha, nilikimbilia kaskazini.

Siku baada ya siku nilisafiri; kwa miezi mitatu nilisafiri, nisipumzike, nisisimame, ila nilizidi kukimbilia kwenye usahaulifu, mpaka nilipoonana na safari ya yule mwindaji mweupe aliyekwisha kufa, nami nimekuja hapa pamoja na watumishi wake.

Wala sikuleta kitu pamoja nami. Mimi aliye mtoto wa watu, ndiyo, wa damu ya mfalme mkuu Chaka, mimi niliye mkuu mwenyewe, jemedari katika kikosi cha Nkomabakosi, sasa mimi ni mgaagaa, mtu asiye na nyumba.

Wala sikuleta kitu pamoja nami ila shoka hili langu, kwa nguvu zake ambazo kwazo niliwatawala watu wangu.

Wamegawana ng’ombe wangu, watwaa wake wangu na watoto wangu hawautambui uso wangu tena. Hata hivyo, kwa shoka hili hili nitakata njia nyingine nifike mpaka kwenye usitawi. Nimesema! ‘’Basi, akalizungusha shoka lake kichwani likalialia lilipokuwa likiikata hewa.

Nilitikisa kichwa changu, nikasema, ‘’Umslopogaas, nimekujua tangu zamani.

Wewe siku zote ulitamani kupata nguvu na uwezo zaidi, tabia hii imo katika damu yako, lakini naona ya kuwa umeshindwa safari hii.

Zamani ulipotaka kufanya shauri juu ya Kitswayo bin Mpande, nilikuonya, ukanisikiliza. Lakini nilipokuwa sipo karibu nawe kukuzuia mkono, ulichimba shimo kwa miguu yako mwenyewe na kuliangukia sivyo?

Lakini yaliyotendeka yamekwisha tendeka. Na ni nani awezaye kufufua mti uliokwisha nyauka? au kuiangalia nuru iliyokuwako mwaka jana? Nani awezaye kurudisha neno lililokwisha semwa, au kurudisha roho za wale walioangamia? Yale yaliyomezwa na wakati hayarudi tena. Kisa chako na kisahauliwe basi!

‘’Na sasa, tazama, Umslopogaas, nakujua ya kuwa u mtu jasiri wa damu ya kifalme, mwaminifu mpaka kufa.

Hata katika nchi ya Wazulu ambako watu wote ni hodari, walikuita, ‘Mchinjaji,’ na wakati wa usiku walipokuwa wamekaa kuzunguka moto walisimulia hadithi za matendo yako na za nguvu zako.

Nisikilize basi, wamwona mtu mrefu huyu, rafiki yangu’’ nikamwelekezea kidole Sir Henry; ‘’yeye ni mtu jasiri pia kama ulivyo wewe, naye ana nguvu kama ulivyo nazo wewe, aweza kukutupa begani mwake. Jina lake ni Inkubu.

Tena, wamwona huyu; mwenye tumbo, na jicho linalong’aa, na sura ya kuchangamka? Jina lake ni Bougwan, kwa sababu ya rodi anayoivaa jichoni, naye ni mtu mwema mwaminifu.

‘’Basi, sisi watatu unaotuona tunataka kusafiri kupita Dongo Egere, ule mlima mrefu mweupe, na kuingia karibu nchi isiyojulikana.

Hatuna habari za mambo tutakayoona huko; tunakwenda kutafuta matendo ya ujasiri, na kuona mahali papya, kwa kuwa tumechoka kukaa bure na kuzungukwa na mambo yale yale siku zote.

Je, utafuatana nasi? Wewe utakuwa na amri juu ya watumishi wetu wote, lakini yatakayokupata siyajui kamwe.

Zamani sisi watatu tulisafiri pamoja, tukamchukua mtu kama wewe, jina lake Umbopa, tazama, tulipoagana naye alikuwa amekwisha kuwa mfalme wa nchi kubwa, ana majeshi ishirini ya askari, na kila jeshi lilikuwa na askari elfu tatu, waliokuwa wanamngojea kuzitimiza amri zake.

Mambo yatakayo kupata wewe siyajui; labda mauti inakungojea wewe na sisi pia. Je, utashirikiana nasi na kuandamana nasi na kubahatisha ajali, au unaogopa Umslopogaas?''

Yule mkuu wa zamani alichekelea, akasema, ‘’Maneno yako yote ni ya kweli Makumazahn.

Kweli nimefanya mashauri mengi katika maisha yangu, lakini sikuangamia kwa kutafuta uwezo kupita kiasi; ila ni aibu juu yangu kusimulia kwamba ni uso mzuri wa mwanamke, ndiyo ulioniangusha.

Haya heri na tuyasahau. Basi, tutaona habari kama zile tulizoziona zamani Makumazahn, tulipofika na kuwinda katika nchi ya Wazulu, Ndiyo, nitaenda, kama ni kwa maisha, ama kama ni kwa mauti, ni sawa tu kwangu, mapigo yaanguke upesi na damu imwagike tu.

Ninazidi kuwa mzee na vita nilivyopigana havijanitosha! Nami ni mtu wa vita kuliko watu wa vita, tazama makovu yangu’’ akaonyesha makovu na alama za majeraha zisizo na hesabu, michomi, mikato, iliyokuwapo katika ngozi ya kifua na miguu na mikono yake.

Tazama shimo hili katika paji la uso wangu, ubongo, wangu ulitokeza humu, na hata hivyo nilimuua Yule aliyenipiga, nami ni hai, je, wajua watu wangapi niliowaua katika vita vilivyopiganwa mkono kwa mkono Makumazahn?

Tazama, hii ni hesabu yake’’. Alionyesha mstari mrefu wa michoro katika kipini cha shoka lake, ‘’Zihesabu Makumazahn mia moja na tatu nami sikuwahesabu ila wale niliowatumbua kama ilivyo desturi yetu, wala sikuwahesabu wale. Waliopigwa na mtu mwingine.’’

Basi, nilitambua kuwa anaanza kuona hamu, kumwaga damu, nikasema, ‘’Nyamaza, nyamaza. Unaitwa ‘Mchinjaji’ kwa haki.

Hatutaki kusikia habari zako za kumwaga damu. Kumbuka ya kuwa ukija pamoja nasi, sisi hatupigani isipokuwa kujitetea tu. Sisi tunahitaji watumishi, Wakazi. Hawa wamesema kuwa hawataki kuja pamoja nasi.’’

Umslopogaas akasema kwa sauti kuu, hawa! Yu wapi mbwa anayekataa kuja baba yangu? Wewe’’ akaruka mbele akawarukia wale Wakazi niliosema nao kwanza, akamshika mmoja mkononi akamkokota mbele yetu, akamtikisa hata yule mtu alitishika sana, akasema.

‘’Wewe mbwa ulisema ya kuwa hutaki kufuatana na baba yangu? Sema maneno yale tena nami nitakukaba koo, wewe na wale walio pamoja nawe.’’

Vidole vyake virefu vilimkaba koo. Kisha akasema .. ‘’Je, umesahau jinsi nilivyomfanyia ndugu yako?’’

Yule mtu akatweta, akasema kwa kigugumizi, ‘’Basi! Basi! Tutafuatana na mtu mweupe huyu.’’

Umslopogaas akafanya kama amefura kwa hasira, akasema, ‘’mtu mweupe! Unamtaja nani mbwa mwenye ufidhuli?

Yule mkazi akajibu upesi, ‘’Basi! Basi! Tutafuatana na bwana mkubwa .’’

Basi, Umslopogaas akatuliza sauti yake, akamwacha Yule mtu akaanguka chini, akasema, ‘’Ndiyo, nafikiri ya kuwa mtafuatana nasi.’’

SURA YA PILI

Baada ya muda, mambo yalipokuwa tayari, tulitoka Lamu, na baada ya kusafiri siku kumi na kukutana na mambo mengi, ambayo hapana haja kuyataja hapa tulifika mahali paitwapo Chara, kando ya mto Tana.

Katika mambo tuliyoyaona ni magofu ya miji ya zamani, nayo ni mengi katika pwani hizi. Kwa kadiri ya magofu ya misikiti na nyumba za mawe yaliyopo, miji hii ilikuwa na watu wengi sana zamani. Miji hiyo ni ya zamani sana.

Nimeambiwa ya kuwa ilikuwa maarufu hata katika wakati wa Agano la Kale, na watu waliokaa. Humo walikuwa wakifanya biashara na watu wa Uhindi na wa nchi nyinginezo.

Lakini utukufu wake umetoweka, biashara ya watumwa imeumaliza na mahali pale waliposimama zamani matajiri wa kutoka nchi zilizostarabika wakati ule, wakishindania bei katika masoko yaliyojaa watu, sasa simba huja na kufanya baraza zao usiku, na badala ya mazungumzo ya watumwa na sauti za bidii za watu waliokuwa wakiwanadi, mlio wa simba hulialia katika magofu.

Huko Chara tuligombana sana na mnyapara wa wapagazi tuliowaajiri kufuatana nasi mpaka hapo, maana alitaka kututoza fedha nyingi kuliko ile tulivyopatana. Mwishowe alijaribu kututisha, ya kuwa atawapeleka Wajivuni kutushambulia.

Usiku ule yeye pamoja na wapagazi wote walitoroka pamoja na mizigo waliyoichukua. Kwa bahati hawakuziiba banduki wala risasi wala nguo zetu; si kwa sababu hawakuzitaka, ila kwa sababu zililindwa na wale askari watano wa Kikazi.

Basi, hapa tuliona dhahiri ya kuwa hatuwezi kuvumilia matata mengine ya wapagazi, na kwa kweli hatukubaki na vitu vingi vya kuchukuliwa. Lakini kama hatuna Wapagazi, tutaweza kuendelea namna gani?

Bwana Good ndiye aliyetoa shauri la kufaa. Alituonyesha mto, akasema, ‘’Hapa pana maji, na jana niliona wenyeji wengine katika mitumbwi wanawinda viboko.

Nadhani mahali anapokaa Bwana Mackenzie ni kando ya mto Tana. Je, kwa nini tusipate mitumbwi na kuiendesha mpaka kufika kwake?’’

Shauri hili zuri lilipokewa kwa furaha, na mara ile nilianza kufanya shauri la kununua mitumbwi inayofaa, kwa wenyeji wa karibu.

Baada ya kujaribu siku tatu niliweza kununua miwili mikubwa, kila mmoja uliweza kuchukua watu sita pamoja na mizigo mingine. Bei ya mitumbwi hiyo ilikuwa mavazi yetu yote yaliyobakia, tena tukatoa na vitu vingine pia.

Basi, siku iliyofuata ile tuliyonunua mitumbwi, tulianza safari yetu tena. Katika mtumbwi wa kwanza mlikuwamo Bwana Good, Sir Henry na Wakazi watatu, katika ule wa pili, mimi, Umslopogaas na Wakazi wawili.

Kwa kuwa tulikuwa tukipanda mtoni, ilitupasa kuvuta kasia nne katika kila mtumbwi; ikawa kazi ngumu sana. Baada ya siku ya kwanza Bwana Good aliweza kusimamisha mlingoti katika kila mtumbwi, akatengeneza matanga, na kazi ilikuwa rahisi zaidi.

Lakini mkondo wa maji ulikuwa na nguvu, nasi hatukuweza kwenda zaidi ya maili ishirini kutwa.

Desturi yetu ilikuwa kuondoka asubuhi na mapema na kupiga kasia mpaka saa nne na nusu, ndipo jua linapokuwa kali zaidi. Basi, tulifunga mitumbwi kando ya mto tukala chakula kidogo kisha tulilala au kujizungumzisha mpaka saa tisa.

Saa tisa tulianza tena kupiga kasia mpaka saa kumi na moja hivi, ndipo tulishuka kando ya mto kufanya kambi, na Bwana Good alianza kujenga boma la miiba na kukoka moto kwa msaada wa askari wetu.

Mimi pamoja na Sir Henry na Umslopogaas tulikwenda kuwinda tupate nyama kwa kitoweo chetu.

Kwa desturi hatukuona shida kupata mnyama, maana wanyama wa kila namna wapo kando ya mto Tana. Siku moja jioni Sir Henry alipiga twiga mchanga wa kike, na ubongo na mifupa yake ulikuwa mtamu sana.

Siku nyingine nilipiga kuro wawili, mmoja upande wa kushoto, na mmoja upande wa kuume, na siku moja Umslopogaas, ambaye kama Wazulu wote walivyo, hana shabaha, aliwahi kupiga pofu mnono kwa bunduki niliyomwazima.

Pengine tulibadili namna ya chakula chetu kwa kupiga kanga au ndege wengine waliokuwa wengi, kwa risasi, au kwa kuvua namna ya samaki wazuri waliokuwamo tele katika mto Tana.

Siku tatu baada ya kuondoka, jambo baya lilitokea.

Tulikuwa tunakaribia kando ya mto ili kufunga mitumbwi yetu na kupanga kambi tayari kwa usiku, tukaona mtu amesimama juu ya kilima kidogo mwendo wa yadi arobaini toka hapo tulipokuwapo, naye alikuwa anatuangalia sana. Kumtazama tu, mara nilitambua ya kuwa ni askari wa Kijivuni.

Na hata kama ningalikuwa na shaka kulitambua kabila lake ningalijuwa mara ile, maana Wakazi walinong'ona kwa hofu, ''Mjivuni!''

Jinsi alivyotisha alipokuwa amesimama hivyo, amevaa mavazi yake ya vita! Nimezoea sana watu wa makabila mengi maisha yangu yote, lakini nadhani sijaona mmoja aliyekuwa wa kutisha zaidi ya huyo.

Kwanza alikuwa mrefu sana, nakisia alikuwa mrefu kama Umslopogaas, tena umbo lake zuri mno ila labda jembamba kidogo.

Lakini uso wake ulikuwa mwovu sana. Alikuwa ameshika mkuki mrefu kadiri ya futi tano na nusu katika mkono wake wa kuume, na bamba lake lilikuwa na urefu wa futi mbili na nusu, na upana wake inchi tatu, na mwisho wa kipini chake ulikuwa na ncha ya chuma urefu wa futi moja au zaidi.

Kwa mkono wake wa kushoto alikuwa ameshika ngao ya ngozi ya nyati iliyotiwa alama alama.

Alikuwa amevaa vazi la manyoya ya mwewe begani, na kuzunguka shingo yake alivaa kipande kirefu cha kitambaa kadiri ya futi kumi na saba, na upana wake ulikuwa futi moja na nusu; kina mstari wa rangi katikati yake kwa marefu.

Ngozi ya mbuzi iliyokuwa mavazi yake ya siku za amani ilifungwa kiunoni kwa mkanda, na katika mkanda amechomeka sime upande wa kuume na rungu upande wa kushoto lakini labda vazi lililonivuta macho zaidi lilikuwa manyoya ya mbuni yaliyofungwa kuuzunguka uso wake.

Duara hii ya manyoya ilifungwa chini ya kidevu chake, ikapita kichwani ikawa kama duara inayouzunguka uso wake mwovu.

Katika visigino vya miguu alikuwa amevaa manyoya meusi, na kwa juu ya machavu ya miguu amevaa vishungi vya manyoya ya mbega.

Basi, hayo ndiyo mavazi ya yule Mjivuni, aliyesimama akituangalia tulipokuwa tukikaribia katika mitumbwi yetu, lakini kueleza tu hakufai, lazima mtu amwone ndio atambue namna alivyokuwa.

Kweli sikuweza kuona sehemu zote za mavazi yake kwa mara ile, ila nilipata nafasi nyingi baadaye kuziona.

Tulipokuwa tukisita na kufikiri shauri la kufanya, Yule Mjivuni alijinyosha wima kwa madaha, akautisa mkuki wake kutuelekea, kisha, aligeuka akateremka upande wa pili wa kilima.

Sir Henry aliita kutoka mtumbwini mwake, akasema, ‘’Ati! Yule mnyapara amelishikilia neno lake na kutuletea Wajivuni.

Je, waonaje, itakuwa salama kuteremka kando ya mto?’’

Mimi sikufikiri ya kuwa itakuwa salama, lakini hata hivyo hatukuweza kupika katika mitumbwi yetu, wala hatukuwa na chakula kilichoweza kuliwa bila kupikwa, kwa hivi ilikuwa vigumu kujua shauri la kufanya.

Mwishowe, Umslopogaas alitoa shauri, yaani yeye aende kupeleleza, akatambaa katika kichaka kama nyoka, nasi tulikaa katikati ya mto tukingoja, Baada ya kupita nusu saa alirudi, akatuambia kuwa hakuona hata Mjivuni mmoja karibu.

Lakini aliona mahali walipokuwa wamefanya kambi karibuni, naye alifikiri ya kuwa waliondoka kadiri ya saa moja tu na Yule mtu tuliyemwona hakosi alipelekwa kupeleleza habari zetu.

Basi, hapo tulishuka, tukaweka mtu wa kushika zamu, tukaendelea kupika chakula na kukila. Kisha, tulifanya shauri juu ya hali yetu.

Kwetu yakini, iliwezekana kuwa yule Mjivuni hana shughuli na sisi, ila labda ni mmoja wa kikosi cha Wajivuni waliokuwa wakienda kuwashambulia watu wa kabila jingine.

Rafiki yetu Yule Bwana Balozi wa Lamu alituambia kuwa vikosi vya namna hiyo vinatembea tembea.

Lakini tulipojikumbusha maneno ya yule mnyapara, na kufikiri namna Yule Mjivuni alivyotutikisia mkuki wake, tuliona ya kuwa jambo hilo halikuendelea bali lilielekea ya kuwa wanatufuata wakingojea wakati unaofaa kutushambulia.

Basi, kama ni hivi, yapo mashauri mawili yanayowezekana, la kwanza tuendelee mbele, na la pili turudi nyuma.

Lile la pili lilikataliwa mara ile, maana ilikuwa dhahiri kwamba tukirudi tutapambana na hatari zilezile tutakazo pambana nazo kama tukiendelea, tena tulikuwa tumekaza nia kwenda mbele kwa vyovyote.

Lakini tuliona kuwa si salama kupiga kambi na kulala usingizi nchi kavu, kwa hivi tuliingia katika mitumbwi yetu, tukaipeleka katikati ya mto, ambao haukuwa mpana sana, tukatia nanga, yaani mawe makubwa yaliyofungiwa kamba ya mnazi.

Hapa tulikuwa karibu kabisa kuliwa na mbu, na jambo hili pamoja na fikra za hali yetu lilinizuia nisilale usingizi kama wenzangu, ingawa

wanashambuliwa na mbu.

Basi nilikaa nikivuta tumbako na kuwaza juu ya mambo mengi na hatari ipo ya kupatwa na homa kwa kulala mahali kama hapa, tena mguu wangu wa kuume umekufa ganzi kwa kukaa hali umekunjwa katika mtumbwi, lakini nilianza kuufurahia uzuri wa usiku.

Miali ya mbalamwezi ilichezacheza juu ya uso wa maji yanayopita kasi kuendea baharini, kama maisha ya wanadamu yapitavyo kuendea kaburini, mpaka yakang'aa kama utando mpana wa fedha, yaani mahali pa wazi pasipo fikiwa na vivuli vya miti.

Lakini karibu na kando ya mto palikuwa giza sana na upepo ulivuma katika matete, ukafanya sauti ya kuhuzunisha.

Upande wa kushoto, ng'ambo ya mto, palikuwapo namna ya ghuba ndogo yenye mchanga pasipo na miti, na hapo niliweza kuona vivuli vya wanyama wengi waliokuja kunywa maji, mpaka kwa ghafla nilisikia ngurumo ya kutisha sana, na mara ile wote wakatimka.

Baadaye kidogo, niliona umbo kubwa la simba akija kunywa maji baada ya kula kwake.

Halafu aliondoka, ndipo niliposikia kishindo katika matete kadiri ya yadi hamsini kutoka hapo tulipokuwapo, na baada ya dakika chache kitu kikubwa cheusi kiliibuka katika maji.

Kumbe, ni kichwa cha kiboko. Kikazama tena bila kufanya sauti, kikaibuka tena karibu, yaani kadiri ya yadi tano tu kutoka mahali tulipo.

Hapo niliona ya kuwa yupo karibu sana, na kwa hivi sikuona raha, na hasa kwa kuwa alionekana kama atakaye kujua mitumbwi yetu ni kitu gani.

Alikifunua kinywa chake kipana, labda apige miayo tu, nikayaona meno yake, nikafikiri jinsi anavyoweza kuusagilia mbali mtumbwi wetu mdogo kwa dhoruba moja.

Nilianza kufikiri labda itafaa nimpige risasi, lakini nilipofikiri zaidi, niliazimu kumwacha kama asipojaribu kuushambulia mtumbwi. Halafu alizama tena bila kufanya sauti hata kidogo, wala sikumwona tena.

Papo hapo nilitupa macho ng'ambo ya kuume, nikawa kama ninaweza kuona kitu cheusi kinapita katika mashina ya miti.

Macho yangu ni makali sana, nami nadhani niliona kitu kwa hakika, lakini kama ni ndege, au mnyama, au mtu sikuwa na hakika.

Lakini papo hapo wingu jeusi lilipita mbele ya mwezi, kwa hiyo sikukiona kile kitu tena. Tena, papo hapo nilisikia mlio kama wa bundi akilia mfululizo, baadaye kukawa kimya kabisa isipokuwa sauti za kuchakacha katika miti na matete, wakati upepo ulipoyatikisa.

Lakini kwa jinsi isiyoelekezeka, sasa nilianza kushuku hatari za kuona hofu,hapakuwapo wala sababu ya dhahiri ya kunitia hofu hivyo zaidi ya zile zinazomzunguka msafiri yeyote katika nchi ya Afrika, lakini hata hivyo, bila shaka niliona hofu.

Lakini nilikaza nia nisishindwe na hofu, ingawa jasho baridi lilinitoka pajini mwa uso. Wala sikukubali kuwaamsha wenzangu.

Hali yangu ilizidi kuwa mbaya, na moyo wangu ulinipigapiga kama moyo wa mtu anayekaribia kufa. Na mishipa yangu ilinichezacheza kana kwamba kitisho kiovu kiko karibu. Watu waliopata kuota jinamizi, watafahamu namna hali yangu ilivyokuwa.

Lakini hata hivyo nilijikaza nikakaa kimya, nikageuza uso wangu tu kumtazama Umslopogaas na Wakazi wale wawili waliokuwa wamelala kando yake.

Nilisikia kishindo kidogo cha kiboko mbali, na yule bundi alilia tena, na upepo ulianza kuvuma katika miti na kufanya sauti ya kuhuzunisha iliyopoozesha moyo. Baadaye nilipata kujua kuwa Wajivuni huitana kwa kuiga sauti ya bundi.

Juu niliona wingu jeusi, na chini maji meusi yalikuwa yakipita kasi, nikaona kama kwamba mimi na mauti tupo katika yake. Niliona ukiwa kabisa.

Mara damu yangu ilikuwa kama imevia katika mishipa yangu, na moyo wangu kusimama kimya. Je, ni ndoto tu ama ndio mwendo?

Niliyageuza macho yangu kuutazama mtumbwi wa pili uliokuwa ukielea kando yetu, nisiuone, ila badala yake niliona mkono mweusi mwembamba umeinuliwa juu ya ubavu mwa mtumbwi.

Hakika ni jinamizi! Lakini mara ile uso mwovu ulitokea juu kama kwamba umetoka majini, ndipo mtumbwi ulipoinama, kisu kikang'aa ghafla, na Mkazi mmoja aliyekuwa amelala kando yangu akapiga ukelele na kitu cha moto kilichuzurika usoni pangu.

Mara ile kuduwaa kwangu kukakoma, nikatambua kwamba si jinamizi, ila tumeshambuliwa na Wajivuni wanaogelea majini.

Nikashika silaha ya kwanza niliyoweza kuipata ikatokea kuwa ni shoka la vita la Umslopogaas, nikapiga kwa nguvu zangu zote pale nilipokuwa nimekiona kisu kinang'aa .

Pigo liliangukia juu ya mkono wa mtu likaugandamiza juu ya ubavu mnene wa mtumbwi, na kuukata kisiginoni.

Yule mtu asifanye sauti hata kidogo akatoweka kama kivuli, alikuja kama kivuli na akaondoka kama kivuli. Ameacha nyuma yake ule mkono wake wenye damu ungali umeshika sime ile iliyokuwa imechomwa katika moyo wa mtumishi wetu.

Mara kulikuwa ghasia na fujo, nikadhani, sijui ni kweli au je, nikaona vichwa vyeusi vingine vikielea majini kuendea ng'ambo ya kuume, ambako mtumbwi wetu uliendea kasi kwa sababu kamba ile iliyokuwa na nanga ya jiwe imekatwa kwa kisu.

Mara nilipotambua hivyo, nilifahamu pia ya kuwa shauri lao ni kuikata kamba ili mtumbwi uchukuliwe na maji ili kuiendea ile ng'ambo ya kuume;

na huko bila shaka Wajivuni wanangojea kutuchoma kwa mikuki yao.

Basi, nilishika kasia moja mwenyewe, nikamwambia Umslopogaas aishike nyingine, maana wale Wakazi walikuwa wameduwaa kwa hofu hata kushindwa kuhema, tukapiga kasia kwa nguvu kurejea tena katikati ya mto.

Wala hatukufanya hivyo kwa haraka zaidi kuliko ilivyopasa, maana katika dakika nyingine tungali kwamba na bila shaka ingalikuwa ndiyo mwisho wetu.

Mara tulipofika katikati ya mto tena, tulianza kupiga kasia kupaendea pale ulipokuwapo ule mtumbwi mwingine umetiwa nanga nayo ilikuwa kazi ngumu na hatari pia, kwa sababu hakuna la kutuongoza ila sauti ya Good, maana alipiga kelele mara kwa mara.

Mwishowe tuliufikia mtumbwi, tukashukuru tulipoona ya kuwa hawakushambuliwa.

Haikosi ule mkono ulioikata kamba ya mtumbwi wetu ungaliikata yao, na yule mtu asingalivutwa na tamaa ya kuua na jambo hilo, ingawa lilitupotezea maisha ya mtu mmoja na Yule Mjivuni mkono wake, lakini pia lilituokoa sote wengine tusiangamizwe.

Kukosa kukiona kile kitisho kiovu kikitokea juu ya ubavu wa mtumbwi, kitisho ambacho sitakisahau mpaka siku ya kufa kwangu. Mtumbwi wetu ungalichukuliwa kando ya mto kabla sijatambua umepatwa na nini, na habari hizi hazingaliandikwa nami.

SURA YA TATU

Tulifunga mtumbwi wetu pamoja na mtumbwi ule mwingine kwa kipande cha kamba kilichobaki, tukakaa tukingojea mapambazuko, na kufurahi kwa vile tulivyookoka.

Baada ya kukesha sana, kukapambazuka, nami sijapata kupendezwa kuuona mwangaza kama nilivyopendezwa kuuona siku ile, ingawa uliangaza juu ya kitu cha kutisha ndani ya mtumbwi wangu.

Maana, pale chini katika mtumbwi yule askari alikuwa amelala na sime imesimama kifuani mwake, na ule mkono uliokatwa ungali umeishika sime.

Sikuweza kuvumilia kumtazama zaidi, basi, nililivuta ndani lile jiwe lililokuwa nanga yetu, nikamfungia Yule askari aliyeuawa, nikamtumbukiza majini, akazama mpaka chini.

Kisha, tulitoa mtu mmoja katika mtumbwi mwingine tukamweka katika mtumbwi wangu, tukaendelea tena katika safari yetu, wote tumeshikwa na majonzi, wala hatukuweza kuona raha kwa kufikiri juu ya mambo ya mbele yetu, ila tulitumaini kufika misioni kabla ya kuingia usiku.

Hapo mambo yalizidi kuwa mabaya, maana jioni ilipokaribia, ilianza kunyesha mvua tukalowa kabisa, tena ikawa lazima pengine kukumba maji katika mitumbwi, na kwa kuwa upepo ulitulizwa na mvua, matanga hayakufaa kitu, ikawa lazima tupige kasia kadiri tulivyoweza.

Saa tano tulishuka mahali pa wazi kando ya mto kwa upande wa kushoto, na kwa kuwa mvua ilipungua kidogo, tulivua samaki tukazibanika motoni. Hatukuthubutu kwenda kutafuta wanyama.

Saa nane tuliondoka tena, tukachukua akiba ya samaki wa kuchoma na baada ya kitambo ilianza kunyesha tena mvua nyingi kuliko kwanza.

Tena, tulianza kuona shida zaidi kwenda mbele mtoni kwa sababu ya miamba mingi, na mafungu ya mchanga, na nguvu ya mkondo wa maji

ilizidi, basi, ilikuwa dhahiri ya kuwa hatutawahi kuifikia nyumba ya Bwana Mackenzie kabla usiku haujaingia na habari hizi zilizidi kutusumbua.

Ingawa tulivuta kafi kadiri tulivyoweza, lakini hata hivyo hatukuweza kwenda mbele zaidi ya maili moja kwa saa moja, na ilipofika saa kumi na moja jioni, tulikuwa tumechoka taabani, na kwa kadiri tulivyoweza kukisia, nyumba ya misioni ipo mbali mwendo wa maili kumi.

Basi, tulianza kutengeneza mambo kadiri tulivyoweza tayari kwa usiku.

Baada ya mambo yaliotokea jana, hatukuthubutu kufanya kambi nchi kavu, na hasa kwakuwa kingo za mto Tana zimefunikwa na vichaka vinene vya kutosha Wajivuni elfu tano kujificha humo wasionekane, na kwanza tulifikiri tutakuwa hatuna budi kukaa tena katika mitumbwi.

Lakini kwa bahati, tuliona kisiwa kidogo, kadiri ya upana na urefu wa yadi kumi na tano, katikati ya mto. Basi, tulipiga kafi mpaka kufikia, tukaiegesha mitumbwi yetu, tukashuka na kutengeneza mambo kadiri tulivyoweza.

Mvua ilizidi kunyesha, tukaona baridi hata ndani ya mifupa yetu, wala hatukuweza kukoka moto.

Lakini mvua ilitufariji kwa neno moja, yaani Wakazi walituambia kuwa Wajivuni hawata tushambulia wakati wa mvua kwa sababu inawasumbua sana. Tulikula kipande cha samaki kilicholowa maji, isipokuwa Umslopogaas, maana yeye kama Wazulu wote, hali samaki.

Ndipo ulipoanza usiku wa taabu kupita zote ninazozikumbuka, isipokuwa taabu ya usiku ule ambao sisi watu weupe watatu tulivumilia pamoja tulipokuwa karibu kuangamia kwa baridi na theluji juu ya Ziwa la Sheba katika safari yetu ya kuiendea nchi ya Wakukuana.

Usiku ulikuwa kama hauna mwisho, na mara mbili tatu nilifikiri labda askari wetu wawili watakufa kwa maji na baridi na taabu. Bila shaka wangalikufa kama tusingaliwapa divai mara kwa mara.

Niliweza kuona ya kuwa hata yule mzee shupavu Umslopogaas naye pia anaona maumivu, ingawa alikaa kimya tu, wala si kama wale Wakazi waliolalamikia hali zao bila kunyamaza. Mambo yalizidi kuwa mabaya kwenye saa saba ya usiku tuliposikia tena mlio wa bundi.

Basi, tukajifanya tayari kujitetea kama tukishambuliwa, lakini nadhani tungalishambuliwa wakati huo, tungalishindwa upesi.

Lakini labda mlio ulikuwa wa bundi hasa, au labda Wajivuni nao waliona taabu hata hawana moyo kutushambulia. Kwa vyo vyote hatukuwaona kabisa.

Hatimaye kulipambazuka na ukungu ukatambaa juu ya uso wa maji, na kulipokuwa kweupe, kukatakata, na mvua iliacha kunyesha, ndipo jua tukufu lilipochomoza, tukajivuta miguu, tukaenda tukasimama katika joto la jua, tukashukuru.

Naweza kufahamu kwa nini watu wengine wasiostarabika huliabudu jua, na hasa kama hali ya maisha yao huwalazimisha pengine kuvumilia mvua na baridi kali.

Baada ya kupita nusu saa, tulikuwa tukiendelea tena vizuri kwa msaada wa upepo mzuri. Mioyo yetu ilichangamka kwa kuuona tena mwanga wa jua, tukawa tayari kuzicheka shida na hatari zilizotuelemea jana.

Basi, hivyo tuliendelea kwa furaha mpaka kadiri ya saa tano, na hapo tulipoanza kufikiri kushuka kama ilivyokuwa desturi yetu ili tujaribu kuwinda wanyama tupate kula, mara mto ulipinda, tukaona nyumba imara ya Kizungu iliyozungukwa na baraza imesimama vizuri juu ya mwinuko.

Nyumba ilikuwa imezungukwa na boma la mawe, na handaki nje ya boma.

Karibu na nyumba palikuwa na mti mrefu sana, namna ya msonobari.

Mimi nilikuwa wa kwanza kuiona ile nyumba, nami sikuweza kujizuia nisipige ukelele wa furaha, na wenzangu nao na watumishi wetu pia wakapiga ukelele kadhalika.

Sasa hatukuwa na nia ya kusimama tena. Tukasukuma mbele kwa nguvu, lakini ingawa nyumba ilionekana kama i karibu, ilikuwa mbali kwa kuufuata mwendo wa mto, wala hatukuifikia mpaka saa saba.

Ndipo tulipojiona chini ya mwinuko iliposimama ile nyumba.

Tuliisogeza mitumbwi, yetu mpaka kando ya mto, tukashuka, tukawa katika kuikweza nchi kavu ndipo tulipoona watu watatu waliovaa mavazi ya Kizungu wanatujia kwa haraka wakipita katikati ya miti.

Bwana Good aliwachungulia kwa rodi yake, akasema, ‘’Bwana mmoja, na Bibi mmoja na mtoto mwanamke mmoja, wanakuja kistaarabu karibu na bustani ya kistaarabu kutulaki katika mahali kama hapa kweli hili ni jambo la ajabu kupita yote!’’

Basi, walitukaribia. Yule bwana Mckenzie alikuwa mtu mwembamba, mwenye mvi, na uso wake ulikuwa wa kupendeza, akasema, ‘’Mhali gani mabwana, natumaini hamjambo?

Watu wangu waliniambia tangu saa moja ya kuwa waliona mitumbwi miwili inakuja mtoni, basi, tumekuja kuwalaki.’’ Na yule bibi, akasema, ‘’Tumefurahi sana kuonana tena na watu weupe.’’

Tukavua kofia zetu kuwaamkia, tukawajulisha tu nani. Kisha, Bwana Mackenzie akasema, tumefurahi sana kuwaona. Mwaka mzima umepita tangu alipofika hapa mtu mweupe wa mwisho aliyetujia.’’

Huku nyuma tulikuwa tukiupanda ule mwinuko ambao sehemu ya chini yake ni mashamba ya mahindi na maboga na viazi, na vyakula vinginevyo.

Wenyeji wengine, watu wa misioni walikuwa wamejenga nyumba zao katika mashamba hayo.

Katikati ya mashamba palikuwa na barabara, na kando yake ilikuwapo michungwa mingi iliyojaa machungwa.

Tokea hapo nimependa sana bustani, na nilipoiona ile ya Bwana Mackenzie nilifurahi sana, nikasema, ‘’Lo, bwana, tazama jinsi ilivyo nzuri bustani

yako’’.

Akajibu, ‘’Kweli, ni bustani nzuri sana, wala si ajabu kwa sababu nimefanya kazi nyingi humo, lakini pamoja na hivyo tabia ya nchi hii ni nzuri, na miti huota vizuri sana.’’

Basi, tukaendelea, tukafika kwenye ile handaki ambayo upana wake ulikuwa futi kumi, imejaa maji, na ng’ambo yake palikuwa na boma la mawe urefu wa kwenda juu futi nane, lina vitundu huko na huko vya kupitishia bunduki.

Na juu yake pametapakaa mawe makali na vigae vilivyosakafiwa katika mgongo wa ukuta.

Bwana Mackenzie akalielekezea kidole chake, akasema, ‘’Hii ndiyo kazi yangu iliyo kubwa, au tuseme hii pamoja na kanisa lililojegwa nyuma ya nyumba.

Ilichukua mimi na wenyeji ishirini muda wa miaka miwili kuichimbua ile handaki, na kulijenga boma, lakini kabisa sikuweza kuona ni salama, mpaka kazi zilipokwisha.

Sasa ninaweza kujitetea juu ya watu wakali wote wa katika nchi ya Afrika, maana chemchem inayojaza handaki maji imo ndani ya boma juu ya mwinuko, nayo hububujika siku zote, nami kila mara ninayo akiba ya chakula nyumbani cha kutosha miezi minne.’’

Basi, tulivuka daraja dogo, tukapita katika mlango mwembamba katika ukuta wa boma tukaingia katika bustani nzuri sana.

Katikati ya kiwanja mbele ya nyumba, tuliuona ule mti mrefu, na Bwana Mackenzie alituambia kuwa ni mnara wake wa kuangalia nchi yote, kisha, akasema, ‘’Lakini hamkosi mnaona njaa, basi haya twendeni.’’

Tulipokwisha kula, tuliviwasha viko vyetu vya tumbako, na Sir Henry akasimulia habari za safari yetu, na mkarimu wetu alisikiliza kwa fadhaa.

Akasema, ‘’Ni dhahiri ya kuwa wale Wajivuni waovu wanawafuata, nami nashukuru sana kuwa mmefika nyumbani kwangu salama.

Nadhani hawatadhubutu kuwashambuli hapa. Lakini ni bahati mbaya, maana karibu watu wangu wote wamekwenda pwani kupeleka pembe za ndovu na vitu vingine.

Wako watu mia mbili katika msafara huo, na kwa hivi wamebaki watu ishirini tu wanaoweza kulilinda boma letu ikiwa watatushambulia.

Lakini hata hivyo, nitatoa amri kadha wa kadha ili tusije tukatokewa ghafla.’’ Akamwita mtu mmoja aliyekuwa amesimama nje katika bustani, akamwambia maneno kwa Kiswahili. Yule mtu alisikiliza, kisha, alipiga saluti akaondoka.

Bwana Mackenzie alipokaa tena, nilimwambia, ‘’Natumaini sana ya kuwa hatutawaletea misiba, basi ni afadhali twende mbele na kubahatisha ajali yetu, kuliko kuwaletea wale watu waovu hapa.’’

Akajibu, ‘’Hapana kabisa, hamwendi sasa. Wajivuni wakija, basi watakuja, lakini nadhani nitaweza kuwapokea kwa namna itakayofaa. Mimi siwezi kumwondoa mgeni aende zake hata kama Wajivuni wote wa duniani wakija.’’

Nikasema, ‘’Sasa nakumbuka, Bwana Balozi wa Lamu alituambia kuwa alipata barua kutoka kwako, ambayo kwayo ulimpa habari ya kwamba mtu mmoja alifika toka mbali akasema ameona watu weupe mbali sana ndani ya nchi. Je, unasadiki habari alizokuambia?

Nauliza kwa sababu mara mbili tatu katika, maisha yangu nimesikia tetesi ya habari hizo kwa wenyeji waliotoka kaskazini mbali sana, ya kuwa taifa la watu hao lipo.’’

Bwana Mackenzie asijibu kwanza, ila alitoka chumbani, kisha alirudi tena amechukua upanga wa namna.

Ulikuwa mrefu, na bamba lake ambalo lilikuwa nene na zito lilikuwa limetiwa temsi lote hata kufika karibu na makali yake, na kazi yake

ilipambwa kwa dhahabu. Akasema, ‘’Je, umepata kuuona upanga kama huu?’’

Sote tuliutazama sana, tukavitikisa vichwa vyetu.

Akaendelea akasema, ‘’Nimeuleta kuwaonyesha kwa sababu yule mtu aliyesema ameona watu weupe ndiye aliyeuleta pamoja naye tena, kwa sababu unafanya habari alizozisema kuwa kama kwamba ni kweli.

Kama asingaliuleta nisingalimsadiki. Tazameni; nitawaambieni habari zote kadiri ninavyozijua, lakini si nyingi.

Siku moja jioni nilikuwa nimekaa barazani, na maskini mtu aliyedhoofu sana alikuja akichechemea, akaketi mbele yangu.

Nikamuuliza ana habari gani, akaanza kuniarifu habari kama yeye ni mtu wa kabila linalokaa mbali sana kaskazini.

Na jinsi kabila lake lilivyoangamizwa na watu wa kabila jingine, na yeye pamoja na watu wengine wachache waliosalia, walifukuziwa kaskazini zaidi kupita ziwa liitwalo Laga.

Kutoka huko, alikwenda mpaka ziwa jingine lililoko juu ya mlima, akaliita ‘ziwa lisilo na mwisho kwa kwenda chini.’

Na huko mkewe na ndugu yake wakafa kwa ugonjwa wa kuambukiza labda ndui na kwa hivi watu wa huko walimfukuzia jangwani atoke katika miji yao.

Akatangatanga kupita juu ya milima muda wa siku kumi, kisha, akaingia katika gongo la mwitu wa miti yenye miiba.

Na siku moja akaonekana huko na watu weupe wengine waliokuwa wakiwinda, wakamchukua mahali ambapo watu wote ni weupe, wakaao katika nyumba za mawe.

Alikaa hapo muda wa juma moja amefungiwa katika nyumba, mpaka siku moja mtu mwenye ndevu nyeupe, aliyemtambua kuwa ni mganga, akaja kumtazama, kisha akaongozwa kupita katika mwitu wa miti yenye

miiba mpaka jangwani, akapewa chakula na upanga huu, ndivyo alivyosema, akaachwa huru.’’

Sir Henry alikuwa akisikiliza sana habari hizi, akasema, ‘’Ndiyo, halafu alifanya nini?’’

Bwana Mackenzie akasema, ‘’Kadiri alivyosema, alipatikana na taabu na maumivu yasiyo na idadi, akaishi siku nyingi anakula mizizi na matunda ya porini, na vinyama alivyoweza kuvikamata na kuviua.

Mradi aliweza kuishi, na kwa mwendo wa Pole pole alisafiri akijia kusini mpaka akafika hapa.

Sikupata simulizi ya mambo yote ya safari yake, nilimwambia arudi kesho yake, nikamwamuru mmojawapo wa wanyapara amtunze usiku ule.

Yule mnyapara alimchukua, lakini yule maskini alikuwa na upele mwingi hata mke wake mnyapara asikubali aingie ndani asije naye akapata upele pia. Basi alipewa blanketi akaambiwa alale nje.

Ikatokea ya kuwa wakati huo, simba mmoja alizoea kutembeatembea karibu, na kwa bahati mbaya alisikia harufu ya yule msafiri maskini, akamrukia, akamuuma kichwa hata karibu kutoka kabisa.

Wale waliokuwamo nyumbani hawakuwa na habari, na huu ulikuwa ndio mwisho wake na wa hadithi yake juu ya watu wale weupe na ikiwa habari hizo ni kweli ama si kweli, siwezi kuwaambia.

Je, wewe Bwana Quatermain waonaje?’’

Nilitikisa kichwa changu, nikajibu, ‘’Mimi sijui.

Yapo mambo mengi ya ajabu yaliyofichika katikati ya nchi hii kubwa, nami sipendi kusema kuwa ni kweli, ama si kweli.

Lakini liwalo lolote na liwe, tumekaza nia kujaribu kuvumbua habari. Tumenuia kusafiri mpaka Lekakisera, na kutoka huko tutaenda kule kwenye Ziwa Lagana kama wako watu weupe wanaokaa kupita hapo, basi tutajaribu tuwezavyo kuwagundua.’’

Bwana Mackenzie akasema, ‘’Ninyi watu ni jasiri sana.’’ Akacheka kidogo, tukaziacha habari zile.

SURA YA NNE

Tulipokwisha kula tulitembea kuzitazama nyumba na mashamba na bustani za misioni. Nadhani ni mahali pazuri kupita pote nilipopata kupaona katika Afrika.

Kisha tulirudi tukakaa barazani, nikamwona Umslopogaas anazisafisha bunduki zetu. Alikuwa amekaa chini, na shoka lake la vita likiegemea ukutani nyuma yake, akawa anaisafisha kila bunduki kwa uangalifu sana. Kila bunduki aliipa jina.

Moja kubwa sana aliita ‘’Mngurumaji,’’ nyingine ndogo aliita ‘’Yule mdogo anayelia kama mchapo wa mjeledi,’’ nyingine zilizotoa risasi mfulizo aliziita ‘’Wanawake wanaosema upesi sana, hata huwezi kutambua neno moja linapokwisha na jingine linapoanza,’’ na bunduki sita za vivyo hivyo, aliziita ‘’watu tu,’’ na vivyo hivyo.

Alipokuwa akizisafisha, alisema nazo kama kwamba ni watu, akazisimulia habari za matendo aliyoyafanya katika vita alivyopigana.

Pia alizoea kusema na shoka lake ambalo alilifanya kama ni sahibu yake. Aliliita shoka lake ‘’Inkosikazi’’ kwa Kizulu maana yake, mke wa mfalme. Nililitwaa shoka hilo ili nilitazame vizuri.

Kipini chake kilifanywa kwa pembe kubwa sana ya faru, na urefu wake ulipata futi tatu na inchi tatu, na unene wake kadiri ya inchi moja na robo, na mwisho wa kipini ulikuwa kama rungu, yaani kisiweze kuponyoka mkononi.

Kipini hicho kiliweza kupindika kama henzarani lakini kilikuwa na nguvu sana, hata hivi kilizungushiwa nyuzi za shaba huko na huko.

Karibu na sehemu iliyoingia katika shoka lenyewe, kilichorwa alama nyingi, ndiyo hesabu ya watu waliouawa kwa shoka hilo katika vita.

Basi,ndiyo lilivyokuwa shoka la Umslopogaas alililiita Inkosikazi, naye ni shida sana kuliacha popote wakati wowote isipokuwa anapokula, na hamu wakati huo aliliweka chini ya miguu yake.

Sikuweza kufahamu kwa siku nyingi kwa nini alililiita Inkosikazi, yaani mke wa mfalme, na siku moja nilimwomba anieleze. Akasema ya kuwa kwa hakika shoka ni mwanamke, maana ni desturi yake kupeleleza sana katika mambo, tena kwa hakika ni malkia au mke wa mfalme kwa sababu watu wote huanguka mbele yake wameshangaa kwa uzuri na nguvu zake.

Tena alieleza ya kuwa amezoea kumuuliza shauri akipatikana na shida, kwa sababu halikosi lina akili nyingi kwa sababu limechungulia katika ubongo wa watu wengi!

Basi, nilipokwisha kulitazama sana shoka, nikamrudishia Umslopogaas, akaendelea katika kazi yake ya kuzisafisha bunduki.

Hapo mtoto wa Bwana Mackenzie aitwaye Flossie akaja akanichukua nikayatazame maua yake katika bustani. Mengine yalikuwa mazuri sana nisiyopata kuyaona mpaka siku hiyo.

Nikamuuliza kama anayo maua ya namna Fulani ambayo nilisikia habari zake zamani kuwa ni mazuri mno.

Mtoto Flossie alitambua namna yake, akaniambia kuwa alijaribu kuyapanda katika bustani yake yasiote, akasema ya kuwa anadhani ataweza kunipatia ua moja la namna ile.

Baadaye wale watu waliotumwa na Bwana Mackenzie kupeleleza habari za Wajivuni walirudi, wakatuambia kuwa wametafuta kila mahali katika mwendo wa maili kumi na tano wasione hata Mjivuni mmoja, wakafikiri wamekwisha rudi walikotokea.

Tuliposikia habari hizi tulifurahi. Basi, watu wote walipoondoka tulizungumza, na halafu tukaenda kulala.

SURA YA TANO

Asubuhi tulipokuwa tunakula chakula sikumwona mtoto Flossie; nikamuuliza mama yake, ‘’Yuko wapi?’’

Akaniambia, ‘’Nilipoamka asubuhi niliona barua hii imewekwa nje ya mlango wa chumba changu amesema lakini isome mwenyewe.’’

Akanipa ile barua, nikaisoma.

‘’Mpenzi mama, ndiyo kwanza kunapambazuka sasa nami nakwenda milimani nimpatie Bwana Quatermain ua analolitaka, basi nitarudi halafu. Nimechukua punda weupe na yaya, na watumishi wawili wanafuatana nami tena nimechukua chakula cha kutosha, maana nimekusudia kulipata lile ua, hata kama ni kazi ya kutembea mwendo wa maili ishirini. Flossie.’’

Basi, nilianza kuona shaka, nikasema, ‘’Natumaini hatapatwa na mabaya, sikutaka aende na kushughulika hivi kulipata lile ua.’’

Mama yake akasema, ‘’Flossie anaweza kujitunza vizuri, na mara nyingi huenda hivi kama mtoto wa kweli wa mwituni.’’

Hapa, Bwana Mackenzie aliingia chumbani, akaisoma ile barua, nikaona ya kuwa anaona shaka, lakini hakusema neno.

Tulipokwisha kula chakula cha asubuhi, nilimchukua upande nikamuuliza kama itawezekana kutuma watu kumrudisha Yule mtoto, maana nilifikiri kuwa labda Wajivuni wengine wapo karibu na mtoto atadhurika.

Akajibu, ‘’Naona haiwezekani; labda amekwisha fika mbali mwendo wa maili kumi na tano, tena haiwezekani kujua njia ipi aliyofuata.’’

Nikasema afadhali tupande katika mti ule mrefu ulio mbele ya nyumba tuangalie kila mahali kwa darubini, basi tulifanya hivyo, na Bwana Mackenzie alituma watu wengine wajaribu kuzifuata nyayo za Flossie.

Tulipopanda katika mti ule, tuliangaza sana kila upande tusione hata alama ya Flossie wala punda wake, tukashuka tumefadhaika sana, tukarudi barazani tena.

Hapa nilimkuta Umslopogaas amekaa analinoa shoka lake Inkosikazi, kwa kinoo, nikamuuliza, ‘’Unafanya nini Umslopogaas?’’

Akajibu, ‘’Nasikia harufu ya damu.’’ Wala hakusema neno jingine ila hayo tu.

Tulipokwisha kula chakula cha mchana tuliupanda tena mti ule mrefu, tukatizama kila mahali kwa darubini, tusione kitu.

Tuliposhuka tena Umslopogaas alikuwa angali analinoa shoka lake, ingawa makali yake yalikuwa kama wembe.

Bwana Mackenzie akasema, ‘’Asema anasikia harufu ya damu? natumaini si kweli. Ninaanza kuona hofu kwa ajili ya mtoto wangu mdogo. Hana budi amekwenda mbali sana, kama sivyo, saa hizi, angalikuwa amerudi. Sasa ni saa tisa na nusu.’’

Nilimkumbusha ya kuwa mtoto amechukua chakula pamoja naye, na labda alikuwa hana nia kurudi mpaka jioni; lakini hata hivi moyo wangu ulijaa mashaka, na hofu na mashaka niliyoyaona yalikuwa dhahiri.

Baadaye kidogo watu wale waliotumwa na Bwana Mackenzie kumtafuta Flossie walirudi, wakasema walizifuata nyayo za punda kwa mwendo wa maili mbili, kisha zikapotea katika njia yenye mawe, wala hawakuweza kuziona tena.

Walikuwa wametafuta kila mahali wasimwone. Basi, saa zilikawia sana, na jioni ilipofika bila kuwapo dalili ya Flossie, mashaka tuliyoona yalizidi sana.

Mama yake maskini alikuwa ameshikwa sana na majonzi, lakini baba yake alijipa moyo.

Kila pambo lililowezekana kufanywa lilifanywa; watu walitumwa kila njia, tukapiga bunduki zetu ziwe ishara, tukaendelea kuangalia toka katika mti ule mrefu, lakini yote yalikuwa kazi bure.

Basi, giza likaingia, na hata sasa hakuna dalili ya Yule mtoto mzuri Flossie. Saa mbili tulikula chakula cha usiku. Kilikuwa chakula cha huzuni, na Bibi Mackenzie hakuja mezani.

Sisi watatu tulikaa kimya kabisa, maana pamoja na mashaka tuliyoyaona kwa ajili ya mtoto, ulielemewa na fikra ya kuwa kuja kwetu kumeleta msiba huu juu ya mkarimu wetu.

Chakula kilipokuwa karibu kwisha, niliomba ruhusa niondoke mezani. Nilitaka kwenda nje, nikafikiri juu ya mambo.

Nikaenda barazani, nikakitia moto kiko changu, nikakaa katika kiti karibu na mwisho wa baraza.

Nilikuwa nimeketi muda wa dakika sita saba, nikafikiri nimesikia mlango wa ukuta wa boma unafunguliwa, Nikatazama huko nisione kitu, nikafikiri ni mawazo yangu tu, Ulikuwa usiku wa giza, na mwezi haujapanda juu bado.

Baada ya kupita dakika moja tena, kitu kama tufe kilianguka juu ya sakafu ya baraza, kikaviringika kikapita mahali nilipokuwa nimekaa.

Kwanza sikuondoka, nilikaa nikifikiri ni kitu gani. Kisha nilifikiri labda ni mnyama mdogo. Ndipo wazo jingine likanijia, nikaondoka hima.

Kile kitu kilikuwa kimelala mbali kidogo, nikaunyosha mkono wangu karibu nacho, kisijongee, basi ni dhahiri si mnyama. Nikakigusa. Kilikuwa laini chenye uvungu na kizito. Nikakitwaa kwa haraka, nikakiinua katika mwangaza wa nyota. Kilikuwa ni kichwa cha mwanadamu ndio kwanza kimekatwa!

Mimi ni mtu aliyezoea mambo mengi, wala sichafukwi na moyo upesi, lakini lazima nikiri ya kuwa nilipokitazama kichwa kile, moyo wangu

ulielea, nikataka kutapika. Kilifikaje hapa? Cha nani? Nilikiweka chini nikaukimbilia ule mlango mdogo.

Sikuweza kuona kitu wala kusikia mtu. Nilianza kutoka na kwenda katika giza nene, lakini nilikumbuka ya kuwa nikifanya hivyo nitakuwa ninajiweka katika hatari ya kuchomwa mkuki.

Nikarudi, nikaufunga mlango, nikatia komeo. Kisha, nilirudi barazani, nikamwita Sir Henry kwa sauti ambayo nilijaribu kuifanya kama hakuna jambo lililotokea.

Lakini naona sikuweza, maana si Sir Henry tu aliyetoka, ila Bwana Good na Bwana Mackenzie, wote wakaondoka mezani wakaja nje mbio. Bwana Mackenzie akauliza, ‘’Kuna nini?’’ Basi, ikawa sina budi kuwaambia.

Rangi ya uso wa Bwana Mackenzie ilibadilika, ikawa kama ya mfu. Tulikuwa tumesimama nje ya mlango wa sebule, na humo ndani mlikuwamo taa.

Akakishika kile kichwa kwa nywele zake, akakiinua ili akione vizuri, akasema, ‘’Ni kichwa cha mtu mmoja katika wale waliofuatana na Flossie.

Namshukuru Mungu si chake!’’ Sote tulisimama tukatazamana, tumetunduwaa, lakini tufanyeje! Hapo mlango ukabishwa, na sauti ikalia, ‘’Fungua baba, fungua!’’

Basi, tuliufungua mlango, na mtu alijiingiza amejaa hofu. Alikuwa mmoja wapo wa watu wale tuliowatuma kupeleleza habari.

Akasema, ‘’Baba yangu Wajivuni wanatujia! Jeshi kubwa limepita kuzunguka mwinuko, na sasa linaliendea lile boma la mawe la zamani la ng’ombe lililoko karibu na mto. Baba yangu, ujikaze moyo! Katikati yao nilimwona yule punda mweupe na juu yake amekaa bibi Flossie.

Mjivuni mmoja alikuwa anamwongoza punda, na yaya alikuwa anatembea ubavuni analia. Sikuwaona wale watu waliofuatana nao asubuhi.’’

Bwana Mackenzie aliuliza kwa sauti iliyopwaya ‘’Mtoto yu hai?’’

Yule mtu akajibu, ‘’Ni mweupe kama theluji, lakini hakudhurika, baba yangu. Walipita karibu sana nami, nikauona uso wake.’’

Bwana Mackenzie akaguna, akasema, ‘’Mungu amsaidie yeye na sisi pia.’’

Nikauliza, ‘’Wako Wajivuni wangapi?’’

Akajibu, ‘’Zaidi ya mia mbili na hamsini.’’

Tukatazamana tena, tukaulizana kimoyo moyo, ‘’Tufanyeje?’’

Ndipo tuliposikia sauti inalia kwa uthabiti nje ya mlango. Ikasema, ‘’Fungua mtu mweupe, fungua mlango! Nimetumwa kusema nawe.’’

Umslopogaass alikimbilia ukutani, akainyosha mikono yake mirefu akajiinua aweze kutazama juu ya ukuta, akasema, ‘’Namwona mtu mmoja tu. Anazo silaha, tena amechukua kapu mkononi mwake.’’

Nikasema, ‘Fungua mlango,’’ Umslopogaas, akatwae shoka lako ukasimame hapa karibu na mlango. Mwache mtu mmoja tu apite ndani, mwingine akijaribu kuingia, muue.

Basi, mlango ulifunguliwa. Katika kivuli cha ukuta Umslopogaas alisimama ameliinua shoka lake juu tayari kupiga.

Hapo mwezi ukaangaza. Kukawa kimya muda kidogo, kisha, Mjivuni mmoja akaingia amevaa mavazi ya vita kama yale niliyoeleza, tena, amechukua kapu kubwa.

Mwezi uliung’arisha mkuki wake alipokuwa akijongea. Alikuwa mtu mshupavu, mwenye umri upatao miaka thelathini na mitano.

Alipofika karibu alisimama, akaliweka lile kapu chini, akaukita mkuki wake katika ardhi. Ukasimama wima. Akasema , ‘’Tuongee, Tarishi wa kwanza tuliye mtuma hakuweza kuongea,’’ akaonyesha kile kichwa kilicholala barazani kitu cha kutisha katika mwangaza wa mwezi.

‘’Lakini ninayo maneno ya kusema kama ninyi mnayo masikio ya kuyasikia. Tena, nimeleta zawadi.’’ Akaonyesha lile kapu, akacheka kwa

ufedhuli na kiburi kisichoweza kuelezeka, na hata hivi hatuna budi kumsifu, hali amezungukwa na adui.

Bwana Mackenzie akasema, ‘’Haya, sema.’’

Akasema, ‘’Mimi ni mkubwa wa sehemu ya Wajivuni wa Guasa Amboni. Mimi na watu wangu tumewafuata watu weupe hawa watatu,’’ akawaonyesha Bwana Henry, na Bwana Good na mimi, ‘’lakini walikuwa werevu wakatushinda, wakaokoka wakaja hapa. Tuna kisa nao, nasi tutawaua.’’

Nikasema moyoni mwangu, ‘’rafiki, sema labda tutawaua’’

Akaendelea, ‘’Katika kuwafuata watu hawa asubuhi tuliwakamata watu wawili, mwanamke mmoja, punda mweupe na mtoto mwanamke mweupe. Tulimuua mtu mmoja kichwa chake ni kile pale barazani, Yule wa pili aliwahi kukimbia.

Yule mwanamke na mtoto mweupe na punda mweupe tumewateka nao wa pamoja nasi sasa.

Nimeleta kapu hili alilochukua yule mtoto liwe ushuhuda.

Je, kapu hili si la mtoto wako?’’

Bwana Mackenzie akakubali, na Yule Mjivuni akaendelea, ‘’Vyema! Hatuna kisa na wewe wala na mtoto wako, wala hatutaki kuwadhuru, isipokuwa ng’ombe zako ambao tumekwisha kuwateka mia mbili na arobaini.’’

Hapa Bwana Mackenzie aliguna, maana aliwathamini sana ng’ombe aliowafuga kwa uangalifu mwingi sana.

‘’Basi, mtaachiliwa ila ng’ombe zako, hasa kwa sababu naona mahali hapa patakuwa pagumu sana kupashambulia.

Lakini habari za watu hawa ni shauri jingine. Tumewafuata siku kadha wa kadha mchana na usiku, na kwa hivi hatuna budi kuwaua. Tukirudi kwetu

bila kuwaua, wanawake wetu watatucheka na kutudharau. Basi, shauri liwe na matata namna gani, kufa hawana budi kufa.’’

‘’Sasa nina shauri ninalotaka kukuambia. Hatutaki kumdhuru yule mtoto mweupe; ni mzuri sana, tena moyo wake mkuu.

Utupe mmojawapo katika watu hawa watatu maisha kwa maisha nasi tutamwacha mtoto salama huru, tena tutamwacha na yule mwanamke pia. Hili ni shauri la haki, mtu mweupe.

Tunataka mmoja tu, si watatu; hatuna budi kungojea nafasi nyingine kuwaua wale wawili wengine. Hata kumchagua mtu mwenyewe simchagui, ingawa ningependa zaidi yule mkubwa,’’ akamwonyesha Sir Henry; aonekana kama ana nguvu, naye atakufa polepole zaidi.’’

Bwana Mackenzie akasema, ‘’Je, nikikataa kumtoa mtu mmoja?’’

Yule Mjivuni akajibu, ‘’Usiseme hivyo mtu mweupe, maana kama ni hivyo mtoto wako atauawa kesho kutakapo pambazuka, na yule mwanamke aliye pamoja naye asema kuwa huna mtoto mwingine. Nitamuua kwa mkono wangu mwenyewe, ndiyo, kwa mkuki huu huu. Waweza kuja kushuhudia kama utataka.

Nitakuongoza salama,’’ akasema yule mtu mwovu na akacheka sana kwa neno lake la ukatili.’’

Huku nyuma nilikuwa ninafikiri sana na kwa haraka haraka, kama afikiriavyo mtu katika shauri la ghafla, nikanuia nijitoe mwenyewe ili Flossie aachiwe huru.

Sipendi sana kutaja habari hizi nisije nikafikiriwa visivyo Msifikiri lilikuwa shauri la ushujaa, hasha! Ila ni la akili na la haki.

Maisha yangu ni ya kizee, wala hayana thamani tena, yake ni ya ujana yenye thamani. Tena, Yule mtoto akiuawa, kufa kwake kutaelekea kumuua baba yake na mama yake pia, lakini hakuna mtu atakayepata hasara kwa kufa kwangu mimi.

Tena, kwa kweli yule mtoto mpenzi yumo hatarini kwa matendo niliyo tenda mimi.

Mwisho, inafaa mwanaume akikabili kifo cha namna yoyote hata kama ni kibaya, kuliko yule mtoto mwanamke mzuri kuuawa.

Fikira hizi zote zilinipita katika akili zangu katika muda mdogo sana, kisha, nikasema, ‘’Usihangaike Bwana Mackenzie, mwambie yule mtu ya kuwa mimi nitajitoa ili Flossie aachiwe, ila lazima kwa sharti ya kuwa yeye awe salama nyumbani humu humu kabla hawajaniua.’’

Sir Henry na Bwana Good wakasema pamoja kwa sauti moja, ‘’Hapana kabisa, hivyo haiwezekani,’’

Bwana Mackenzie akasema, ‘’Hapana, hapana. Sikubali mauti ya mmoja yeyote iwe katka mikono yangu.

Kama ni mapenzi ya Mungu mtoto wangu afe kifo hiki kibaya, basi, mapenzi yake yatimizwe. Wewe ni mtu hodari, tena shujaa Bwana Quatermain, lakini kwenda, ng’o, hutakwenda.’’

Nikasema kwa uthabiti, ‘’Kama shaurio lingine halitokei, kwenda sina budi nitakwenda.’’

Bwana Mackenzie akamwambia yule mkubwa wa Wajivuni, ‘’Shauri hili ni kubwa sana, nasi hatuna budi kulifikiri. Nitakupa jibu kesho kabla hakujapambazuka.’’

Yule Mjivuni akasema kama kwamba si kitu cha maana, ‘’Vyema, lakini ufahamu ya kuwa kama jibu lako likichelewa, kile kitumba chako cheupe hakitachanua kuwa ua, maana nitakuwa nimekwisha kikata kwa huu,’’ akaugusa mkuki wake.

‘’Ningeweza kufikiri labda ungefanya hila na kutushambulia usiku, lakini yule mwanamke amekwisha niambia ya kuwa watu wako wote wamekwenda pwani, nawe umebaki hapa na watu ishirini tu.

Je, umefanya busara kubaki na watu wachache hao ishirini kulilinda boma lako? Vyema, kwa heri, na ninyi watu weupe wengine kwa herini, ambao makope yenu nitayafumba daima hivi karibuni, kutakapo pambazuka utaleta jibu lako. Kama sivyo basi, mambo yatakuwa kama nilivyosema.’’

Kisha, akageuka akamtazama Umslopogaas aliyekuwa amesimama nyuma yake kama anamlinda.

‘’Hebu, fungua mlango, upesi sana, haya upesi!’’

Amri, hii ilimchukiza sana, muda wa dakika kumi alikuwa amesimama kama kawaida anatamani kumpiga yulejivuni.

Hapo basi hakuweza kustahimili zaidi, akauweka mkono wake mrefu juu ya bega la yulejivuni, akamvuta kwa nguvu hata kumgeuza kabisa na kumfanya amtazame usoni, kisha aliupeleka uso wake mkali katika uso wenye duara ya manyoya ya yule mjivuni.

Akasema kwa sauti iliyonguruma;

‘’Waniona?’’

Yule mjivuni akajibu,

‘’Ndiyo, nakuona kitwana.’’

Umslopogaas akasema,

‘’Waliona hili?’’

akaweka Inkosikazi mbele ya macho yake.

Yule Mjivuni akasema,

‘’Ndiyo, kitwana, nimekiona kidude chako cha kuchezea, kinahusikaje hapa?’’

Umslopogaas akasema,

‘’We Mjivuni mbwa, mpayapaya, wewe mjivuni, wewe mkamata wanawake kwa ‘kidude’ hiki nitavikongoa viungo vyako. Ni vyema ya kuwa u tarishi, ama sivyo, ninge vitawanya tawanya viungo vyako chini katika majani.’’

Yule Mjivuni akautikisa mkuki wake mrefu, akacheka sana kwa muda mrefu, akajibu, ‘’Laiti tungeweza kushindana mimi na wewe peke yetu, ningekuonyesha kazi.’’ Aligeuka aende zake huku anacheka.

Umslopogaas akajibu, na ‘sauti yake ingali ikinguruma,’

‘’Usiwe na shaka, tutashindana peke yetu mimi na wewe.’’

‘’Utashindana uso kwa uso na Umslopogaas, wa damu ya Chaka, wa kabila la Wazulu, mkuu wa jeshi la Nkomabakosi, kama wengi wengine walivyofanya; nawe utajisalimisha mbele ya Inkosikazi kama walivyofanya wengi wengine. Ndiyo, cheka, cheka ila mwisho wako nakuhakikishia fisi watakuwa wanacheka na huku wanavunja mifupa na kuzitafuna mbavu zako.’’

SURA YA SITA

Alipokwisha kwenda Yule Mjivuni, mmoja wetu alilifungua lile kapu. Ua zuri sana lilionekana ndani yake, tena barua ndogo iliyoandikwa katika karatasi iliyofungiwa chakula alichokichukuwa, maneno ya barua hiyo ni haya:

‘’Wapenzi Baba na Mama, Wajivuni wametukamata tulipokuwa tukirudi pamoja na ua hili. Nilijaribu kukimbia nisiweze, Hawakunidhuru wala yaya, lakini wamesema watanibadilisha kwa mmoja wapo wa rafiki za Bwana Quatermain, Mimi sikubali shauri hili.

Usimwache mtu yeyote atoe maisha yake kuniokoa mimi. Jaribu kuwashambulia usiku; wanafanya karamu ya ng’ombe watatu walioiba na kuchinja. Ninaogopa sana, lakini namtumaini Mungu. Siwezi kuandika zaidi, maana wanaanza kunitazama.

Kwa herini

Flossie.’’

Kwa nje ya karatasi iliandikwa, ‘’Nisalimie Bwana Quatermain. Wanachukua kapu, basi atalipata lile ua.’’

Nilipoyasoma maneno yaliyoandikwa na yule mtoto mwanamke shujaa wakati wa hatari ambayo ilitosha kumtia wazimu mtu mzima mwenye nguvu, nakiri ya kuwa nililia machozi, tena, katika moyo wangu nilinuia kabisa ya kuwa hafi ikiwa maisha yangu yanaweza kumuokoa.

Basi, hapa tulianza kuzungumza kwa bidii juu ya shauri la kufanya.

Nikasema tena ya kuwa nitakwenda, na tena Bwana Mackenzie alikataa, na Sir Henry na Bwana Good kama watu wema na waaminifu walivyo, walisema nikienda, basi na wao watakwenda pamoja nami na kufa pamoja nami.

Mwisho, nilisema, ‘’Ni lazima kabisa tufanye jambo kabla ya kufika mapambazuko.’’

Tulikaa pamoja na bwana Mackenzie na kupanga shauri, mwisho tulikubaliana kuwa tuwavamie kijeshi ifikapo muda wa mapambazuko kwa kujua muda huo ulikuwa ni mzuri kwani watakuwa wapo kwenye usingizi mzito.

Pamoja na kuwa hatukuwa na jeshi la kutosha kwani walinzi wengi wa pale mission walikuwa wamesafiri mbali lakini hatukukata tamaa.

Hao hao wachache waliokuwepo tuliona kuwa wanatosha kabisa kuwaunganisha pamoja na kwenda kupambana na wale Wajivuni.

Cha kwanza tuliunda kundi dogo la wapelelezi waende kule kwenye boma la ng’ombe walipoweka kambi yao kwa ajili ya kuwapeleleza na kutupatia ripoti ya nini kinaendelea kila waonapo inafaa kufanya hivyo.

Basi, tulipokwisha weka mambo yote tayari, ilikuwa karibu saa saba ya usiku, tukasubiri. Wapeleleze wetu walituambia kuwa Wajivuni wamekwisha kunywa damu ya ng’ombe na kula nyama nyingi sana, na sasa wamelala kuizunguka mioto yao, lakini watu wakulinda zamu wamewekwa kila mlango.

Flossie, Yule mtoto mdogo alikuwa amewekwa karibu ya ukuta katikati ya upande wa magharibi ya boma, na yaya wake yu karibu naye, na punda weupe amefungiwa kigingi.

Miguu ya mtoto imefungwa kwa kamba, na Wajivuni wamelala huko na huko kumzunguka.

Basi kwa kuwa hakuna jambo tena la kufanya, tulikula kidogo, tukalala kwa muda wa saa mbili.

Niliona ajabu jinsi mzee Umslopogaas alivyoweza kujitupa chini na kupata usingizi mara ile, ingawa mambo makubwa yanamngojea.

Sijui habari za wale wenzangu, lakini mimi sikuweza kulala usingizi. Kwa hakika niliogopa, na sasa kwa kuwa nilikaa kimya, nilianza kufikiri juu ya mambo tunayojaribu kuyafanya, nami sikuyapenda hata kidogo.

Tulikuwa watu thelathini jumla na hawakosi wengine hawakuzoea kupigana, nasi tunakwenda kuwashambulia watu wakali mia mbili na hamsini, watu hodari na stadi wa vita kuliko wenyeji wote wa Afrika, na zaidi ya hayo, walikuwa wamelindwa kwa boma la mawe.

Kweli ni jambo la hatari, na hasa kwa sababu hatuna budi kupafikia mahali petu bila kufanya kelele zozote, tena bila kuonekana na wale Wajivuni waliowekwa kulinda zamu.

Hakika, tukiwaamsha kwa jambo lolote kama vile bunduki ikifyatuka kwa bahati mbaya basi, tumekwisha potea wote, maana Wajivuni wote wataamka mara ile, na tumaini letu la kushinda ni kuwatokea ghafla.

Baada ya kupita muda, nilimsikia Bwana Mackenzie akinong'ona nje ya chumba changu, maana kila jambo lazima lifanywe kimya sana, akaniambia kuwa ni saa tisa, nasi hatuna budi kuanza kazi yetu saa tisa na nusu.

Basi, nilimwambia aingie chumbani, na wakati huo kila mtu alikuwa akivaa na kujitengeneza tayari.

Huku nyuma Umslopogaas alikuwa akiwakusanya watu kiwanjani chini ya ule mti mrefu, akawakagua kuona kama kila mtu ana silaha zake tayari.

Mwisho tulibadili shauri kidogo, tulitoa watu wawili katika wale waliokuwa na bunduki, tukawapa ngao na mikuki ya Kijivuni, tukawaambia wafuatane na Sir Henry na Umslopogaas na yule Mkazi kuulinda mlango mkubwa wa boma lote tuliona kwa dhahiri ya kuwa watu watatu, hatakama ni hodari na wenye nguvu namna gani, hawatoshi kwa kazi ile.

SURA YA SABA

Basi, sasa tulingoja, tukasimama kimya katika baridi na kimya na giza tukiungojea wakati wa kuondoka.

Labda wakati huo wa kungoja ulikuwa wakati mbaya kuliko nyakati zote, muda wa robo saa tu, lakini ulikuwa kama haupiti, jinsi ulivyokawia.

Umslopogaas tu ndiye aliyeonekana kama kwamba hawazi kitu, amesimama ameliegemea shoka lake Inkosikazi, na mara kwa mara ananusa tumbako.

Mwezi ulishuka kabisa ukaiacha dunia nzima giza tupu isipokuwa ukungu wa kijivu katika mashariki, dalili ya mapambazuko yanayokaribia.

Bwana Mackenzie akasimama ameshika saa yake mkononi, na mke wake amemshika mkono akijaribu kujizuia asilie.

Akasema, ‘’Saa kumi kasoro dakika ishirini: nadhani mwangaza utatosha kushambulia saa kumi na dakika ishirini! Bwana Good, nadhani afadhali wewe uanze kwenda, maana lazima utangulie wewe.’’

Bwana Good akaisugua rodi yake, akaivua kofia yake akamuaga Bibi Mackenzie, akaondoka kwenda mwisho wa boma la ng’ombe kwa njia za kuzunguka zilizotokana na watu wake.

Hapa kijana mmoja akaja akatoa habari ya kuwa Wajivuni wote katika kambi wamelala usingizi isipokuwa wale wanaolinda zamu,. Mmoja anatembea mbele ya mlango mkubwa, na mmoja mbele ya mlango mdogo wa nyuma.

Basi, hapo sote tuliondoka. Kwanza kiongozi alitangulia, kisha Sir Henry na Umslopogaas na yule Mkazi na wale watu wawili wa Bwana Mackenzie waliochukua mikuki mirefu na ngao.

Mimi nilifuata pamoja na wenyeji watano wenye bunduki, na Bwana Mackenzie akafuatana pamoja na watu wake sita kulielekea lile boma la ng'ombe walimofanya kambi Wajivuni.

Lilikuwa chini ya mwinuko ule, ambao juu yake nyumba ya misioni imesimama kadiri ya yadi mia nane.

Tulikwenda yadi mia tano za kwanza kwa mwendo wa haraka kidogo kimya kimya; kisha tukaanza kwenda mbele kwa kimya zaidi kama chui anayewinda, tukinyemelea toka mti mpaka mti na mwamba mpaka mwamba.

Basi, tulinyemelea hivi, tukafika karibu na boma la ng'ombe kadiri ya yadi hamsini. Sasa ikawa lazima tupite mahali pa wazi mpaka kulifikia boma, lakini, hapa tulipo tumefichwa katika kichaka. Kulianza kupapazuka na nyota nyingi tukaweza kuona ukungu unazificha.

Mashariki tuliweza kuliona boma kwa shida kidogo, tukauona mwangaza wa mioto ya kambi ya Wajivuni.

Basi, tulisimama tukaangalia, maana tulijua ya kuwa yule anayelinda zamu amewekwa katika mlango wa boma.

Baadaye kidogo alionekana mtu mshupavu, akipita taratibu huko na huko mbele. Ya mlango uliozibwa kwa miiba. Tulikuwa tumetumaini kumwona ameshikwa na usingizi, lakini sivyo. Alikuwa macho kabisa.

Kama hatuwezi kumuua Yule mtu, tena kumuua bila kufanya kelele, basi tmekwisha potea. Tukajikunja na huku tunamwangalia.

Halafu Umslopogaas aliyekuwa karibu nami, alinigeukia, akafanya ishara, kisha, akalala kitumbotumbo kama nyoka, akamwangalia yule mlinda zamu, na mara alipopata nafasi alianza kujinyonganyonga mbele katika majani bila kufanya hata sauti.

Yule mlinda zamu asishuku hatari, akaanza kuimba kwa sauti ndogo na Umslopogaas akazidi kujinyonganyonga mbele, na mlinda zamu

akaendelea kutembeatembea. Halafu aligeuka akatazama juu ya ukuta katika boma.

Mara ile Yule nyoka mwanadamu aliyekuwa akimnyemelea alijinyonganyonga mbele zaidi kadiri ya yadi kumi, akajificha nyuma ya chungu ya majani.

Yule mlinda zamu alipogeuka tena, aliiangalia chungu ile ya majani kama kwamba ameona kitu, akaikaribia kidogo, kisha aliinama akaokota jiwe akalitupa katika yale majani.

Jiwe likampiga Umslopogaas kichwani bila kufanya kishindo.

Basi, Yule mlinda zamu alionekana kama ameridhika, akauegemea mkuki wake, akayatazama yale majani kivivu vivu. Alisimama hivi kwa muda wa dakika tatu, kama kwamba anafikiri, na sisi tulijikunja tukiogopa kuwa jambo baya litatokea.

Mwisho alitazama mashariki kama kwamba anaona zamu yake i karibu kwisha, akaisugua mikono yake, akaanza kwenda upesi upesi ili kujipasha moto.

Mara alipogeuka tena, Yule nyoka mweusi mrefu alijinyonga mbele tena, akajificha nyuma ya chungu nyingine ya majani ambayo ilikuwa hatua mbili tu kutoka mahali yule mlinda zamu anapofika katika mwendo wake.

Yule Mjivuni akageuka akaenda kupita ile chungu ya majani asishuku kuwa adui amejikunja nyuma yake.

Aliipita, ndipo adui yake aliposimama wima akainyosha mikono yake akamfuatia nyuma.

Dakika moja ikapita, na Yule Mjivuni alipotaka kugeuka tena, yule Mzulu mkubwa alimrukia, na katika mwangaza uliokuwa ukizidi tuliweza kuiona mikono yake mirefu myembamba ikimzunguka Mjivuni shingoni na kumkapa koo.

Sasa miili yao wote wawili ilinyongwa pamoja, mara nikaona kichwa cha Mjivuni kinavutwa kwa nyuma, nikasikia kilio kikali kama kwamba kijiti kimevunjwa, akaanguka chini na viungo vyake vinapapatika.

Umslopogaas alikuwa amezitumia nguvu zake za ajabu na kuivunja shingo ya Yule Mjivuni.

Kwa dakika moja zaidi alimkalia mtu wake angali akimkaba koo tu, mpaka akajua hakika hakuna la kuogopa tena kwake, ndipo alipoondoka akatuashiria tuendelee mbele, tukatambaa mbele kwa miguu na mikono kama kundi la nyani.

Tulipolifikia boma tuliona ya kuwa yule Mjivuni alikuwa amezidi kuuziba mlango ambao upana wake ulikuwa kadiri ya futi kumi kwa kuuvutia matawi mengine.

Basi, hapo tuligawanyika ; Bwana Mackenzie na watu wake walitambaa katika kivuli cha ukuta upande wa kushoto, na Sir Henry na Umslopogaas walishika mahali pao mbele ya mlango, mmoja upande huu na mmoja upande huu wa wale watu wawili wenye mikuki na yule Mkazi wakalala chini mbele ya mlango.

Mimi na watu wangu tulitambaa upande wa kuume wa boma, ambao urefu wake ulikuwa kadiri ya hatua hamsini.

Nilipofika katikati nilisimama, nikawapanga watu wangu, nikaacha nafasi ya hatua nne katikati yao, kisha, nilichungulia juu ya ukuta wa boma.

Sasa kulianza kuwa kweupe kidogo, nikamwona Yule punda mweupe, na karibu naye niliweza kuuona uso mweupe wa mtoto Flossie, aliyekuwa ameketi kama Yule kijana alivyoeleza, kadiri ya hatua kumi toka ukutani.

Wajivuni wengi walikuwa wamelala kumzunguka, wameshikwa na usingizi. Huko na huko niliona mioto, na kuzunguka kila moto Wajivuni wapatao ishirini na watano walikuwa wamelala, wameshiba sana.

Pengine mtu mmojawapo aliinuka kidogo na kupiga miayo na kutazama mashariki; lakini hapana aliyeondoka.

Nikafikiri kungojea dakika tano zaidi kwanza, ili mwangaza uzidi kidogo nione shabaha vizuri zaidi, tena, kumpa Bwana Good na watu wake nafasi wajipange tayari.

Mara nilipokuwa nikijifanya tayari kutoa ishara ya kuanzisha shambulio, meno ya mtu mmoja aliyekuwa karibu nami yalianza kugongagonga kwa baridi au kwa hofu, na mara ile Mjivuni aliyekuwa karibu sana aliamka akatazama huko na huko akitafuta kitu kinachofanya kelele.

Mimi nilimkasirikia sana mtu yule kwa sababu ya kufanya kelele, hata nikaingiwa na shaka, nikampiga tumboni kwa kitako cha bunduki yangu ili kuikomesha kelele yake.

Kweli ilikoma, lakini alipojikunja kwa kupigwa, bunduki yake ilifyatuka na risasi yake ilipiga karibu na kichwa changu.

Basi, sasa hapakuwa na haja ya kufanya ishara. Kutoka pande zote mbili za boma la ng'ombe, mifululizo ya risasi ilipigwa, nikaipiga bunduki yangu pia, nikawahi kumwangusha yule Mjivuni aliyekuwa karibu na Flossie.

Alipokuwa katika kuondoka. Basi, hapo nilisikia sauti kutoka mwisho wa boma iliyopanda juu ya kelele zote, nikatambua ni sauti ya Bwana Good, nikafurahi, na katika dakika iliyofuata, mambo yalitokea ambayo sijaona mfano wake wala sitauona tena.

Wale Wajivuni wote walio ndani ya boma waliruka wakainuka kwa sauti moja ya hofu na hasira, na wengi walianguka palepale wamepigwa risasi za bunduki kabla hawajawahi kujijongeza hata yadi moja.

Wale wengine wasiopigwa walisimama kwa muda wameshangaa, kisha walisikia kelele zinatokea upande wa juu wa boma, wakaduwaa kwa risasi zinazowamiminikia, kisha, wote kwa nia moja walijipeleka kuuendea mlango uliozibwa kwa miiba.

Walipokuwa wakienda, sisi tuliwapiga risasi upesi kadiri tulivyoweza kuzishindilia bunduki zetu.

Nilikuwa ndiyo kwanza nimemaliza kupiga risasi kumi zote zilizokuwa katika bunduki yangu, nikataka kutia nyingine, nikamkumbuka yule mtoto Flossie.

Nikamwona anapanda juu ya ukuta akisaidiwa na yaya wake aliyekuwa amelala juu ya ukuta, akawahi kupanda juu salama na kuteremka upande wa pili; nikajua ya kuwa yu salama kwa kadiri ilivyowezekana.

Mambo hayo yanachukua muda kuyasimulia, lakini nadhani labda yalichukua nukta kumi na tano tu kufanyika.

Basi hapa nilitia risasi nyingine katika bunduki yangu, nikaanza tena kupiga, si katika wale waliojilundika mlangoni mwa boma, ila katika wengine waliojaribu kupanda ukutani na kukimbia.

Basi, sina haja kusimulia habari zaidi juu ya vita vikali ambavyo vilikuwa mauaji makubwa ya kutisha.

Neno moja tu lastahili kusimuliwa. Nilikuwa nikitumaini ya kuwa vita vimekwisha, na mara ile nikaona mtu akiruka kwa nyuma ya maiti alipokuwa amejificha, akaruka juu ya chungu za maiti, akakimbia mbio karibu na mahali nilipokuwa.

Lakini, kumbe, hakuwa peke yake, Mara ile nilimwona Umslopogaas anamfuatia, na waliponikaribia zaidi, nilimtambua yule Mjivuni, ndiye yule tarishi aliyetujia usiku.

Basi, yule Mjivuni alipoona ya kuwa ingawa anakimbia kadiri awezavyo, lakini yule anayemfuata anazidi kumkaribia tu, akasimama na adui yake ili apatane naye.

Umslopogaas naye akasimama vile vile, akasema kwa dhihaka.

‘’Ah,ah, ni wewe niliyesema nawe usiku, Mkubwa wa Wajivuni! Tarishi! Mkamata watoto wa kike aliyekuwa tayari kumuua mtoto wa kike! Ndiwe uliyetumaini kusimama uso kwa uso kuwahiana na Umslopogaas, mkubwa wa ukoo wa Makwilisini, wa kabila la Wazulu? Tazama, mambo yako

yametimizwa! Nami, niliapa kuwa nitavikongoa viungo vyako, mbwa mfidhuli wewe, Tazama, nitaitimiza nadhiri yangu sasa!’’

Yule Mjivuni aliyasaga meno yake kwa hasira, akamrukia Umslopogaas na mkuki wake mkubwa.

Alijidanganya, Umslopogaas aliepa vizuri, akalipunga shoka lake juu kichwani kwa mikono yote miwili, akalishusha tena kwa nguvu, likampiga Yule Mjivuni nyuma ya mabega shingo inapoungana na kiwiliwili.

Na makali yake yalikata mfupa na nyama na mishipa, yakawa karibu kutenga kichwa na mkono mmoja na kiwiliwili. Pale pale yule Mjivuni alidondoka chini akiwa maiti.

Umslopogaas aliitazama maiti ya adui yake, akasema, ‘’Basi, Nimetimiza nadhiri yangu ama lilikuwa pigo zuri.’’

SURA YA NANE

Basi, vita vilikwisha. Mahali mbele ya mlango mkubwa wa boma palikuwa pa kutisha sana. Mauaji yalikwisha na mlango ulikuwa umezibwa kwa maiti.

Sisi tulipigana tukiwa na watu thelathini, na katika hao, kumi na watano tu waliobaki hai. Basi, tulipanda mlimani kwa shida na maumivu, na pale mlangoni Bibi Mackenzie alikuwa anatungojea analia kwa ajili ya hofu ya mambo yaliyokuwa yametokea.

Nikasimulia habari za vita kwa maneno machache lakini yule mtoto Flossie ambaye alikuwa amekwisha fika nyumbani salama amekwisha mwambia mengine.

Tukaingia nyumbani tukavua nguo zetu, tukaganga majeraha. Nafurahi kusema ya kuwa mimi sikujeruhiwa, na Sir Henry na Bwana Good waliumia kidogo tu. Lakini Bwana Mackenzie aliumia vibaya sana.

Tulipokwisha kula chakula cha asubuhi, tulilala, wala hatukuamka tena mpaka wakati wa chakula cha mchana, kisha, tuliwakusanya watu wote wanaume, na wanawake, na vijana, waje kwenye mauaji ya asubuhi ili kuzika maiti. Tukazitupa maiti za Wajivuni katika mto Tana.

Basi, tulipoitupa maiti ya mwisho mtoni, mambo mabaya ya asubuhi ya kuishambulia kambi ya Wajivuni yalikwisha.

SURA YA TISA

Zilipopita siku saba, tulikuwa tumekaa tukila chakula cha jioni mezani mwa misheni. Tulikuwa tukihuzunika sana, maana kesho yake na mapema tutaagana na rafiki zetu wema akina Mackenzie, na kuendelea katika safari yetu.

Hatukusikia wala kuona tena habari za Wajivuni, na kwa kweli isipokuwa kwa mikuki miwili mitatu iliyoachwa katika majani nje ya boma la ng'ombe, na maganda machache ya risasi, hakuna alama iliyobaki kuonyesha kuwa vita vikali vimepiganwa huko.

Bwana Mackenzie alikuwa anaendelea vizuri katika kupona kwa sababu ni mtu wa kiasi; na wale waliojeruhiwa walikuwa nao wanaendelea vizuri isipokuwa mtu mmoja aliyekufa kwa sababu jeraha lake lilioza.

Tena, watu wa Bwana Mackenzie walikuwa wamekwisha toka pwani, kwa hiyo walitosha sasa kuilinda nyumba yake.

Basi kwa kuwa mambo yalikuwa hivi, ingawa tulikaribishwa tukae siku nyingi zaidi, lakini tuliona lazima tuendelee mbele, kwanza mpaka mlima Kenya, kisha, katika nchi isiyojulikana, kutafuta taifa lile la watu weupe tuliokusudia kuligundua.

Tulikuwa tumefanya shauri la kuchukua punda kumi na wawili katika safari yetu badala ya wapagazi kuichukua mizigo yetu na sisi pia ikitokea haja.

Sasa tulikuwa na Wakazi wawili tu waliobaki kuwa watumishi, wala hatukuweza kupata wenyeji wengine kufuatana nasi kuiendea nchi isiyojulikana tuliyokusudia kuigundua na nani aliweza kuwalaumu walipokataa?

Basi, ilipopata saa moja asubuhi tulikuwa tumekwisha pakia mizigo yetu, na wakati wa kuagana ulifika.

Tuliona huzuni nyingi tulipoagana na rafiki zetu, na hasa tulipoagana na yule mtoto mdogo Flossie, naye alilia sana.

Basi, baada ya kupeana mikono mara nyingi na kuagana na wenyeji wa huko, tuliondoka, na hii ilikuwa mara ya mwisho kuiona ile nyumba ya misheni. Lakini mara nyingi nawakumbuka wale akina Mackenzie.

Basi, tuliendelea bila kupingwa sana mpaka tulipofika chini ya mlima Kenya, kisha tulilipita ziwa linalokaa peke yake liitwalo Baringo, na huko Mkazi mmoja katika wale wawili waliosalia alikufa.

Aliumwa na nyoka aitwaye pofu aliyemkanyaga, na ingawa tulijaribu tuwezavyo kumwokoa lakini hatukuweza.

Kisha tuliendelea kadiri ya maili mia moja na hamsini mpaka mlima mzuri mwingine wenye theluji juu ya kilele chake, uitwao Lekakisera, ambao mpaka wakati huo kadiri nijuavyo, haujafikiwa na Mzungu yeyote.

Tulipofika hapo tulipumzika muda wa siku kumi na nne, ndipo tulipoondoka tena, tukapita katika mwitu wa nchi iitwayo Elgumi, usio na njia wala watu, Katika mwitu huo wako tembo wengi zaidi kuliko niliopata kuona wakati wote wa maisha yangu.

Wanyama wakubwa hawa walikuwako kila mahali, nao hawakusumbuliwa na wanadamu. Hatukupiga wengi.

Kwanza kwa sababu hatukutaka kuzitupa bure risasi zetu ambazo zilikuwa zinaanza kupungua, maana punda mmoja aliyetwikwa mzigo wa risasi alichukuliwa na maji ya mto mmoja uliofurika, tena kwa sababu hatukuweza kuchukua pembe zao.

Nasi hatukutaka kuua kwa ajili ya kupenda tu. Basi, tuliwaacha isipokuwa wawili watatu tuliowapiga ili kujiinda. Wanyama wa kila namna pia walikuwako katika mwitu huo wa Elgumi.

Tena, walikuwako mainzi wabaya wengi sana waitwao mbung’o. Ilifikiriwa ya kuwa punda na wanadamu hawadhuriki wakiumwa na mbung’o lakini kwakweli punda wetu walidhurika, labda kwa sababu punda

walikuwa wamedhoofu au labda kwa sababu mbung’o wa hapa wana sumu kupita kiasi, sijui, lakini punda wetu walikufa.

Kwa bahati hawakufa mpaka ilipopita miezi miwili baada ya kuumwa, na nilipowachuna niliona mistari yenye rangi ya manjano juu ya nyama, ndiyo dalili kuwa walikufa kwa kuumwa na mbung’o.

Tulipotoka mwitu wa Elgumi, tulizidi kuendelea upande wa kaskazini, maana ndiyo njia aliyoitaja yule msafiri maskini aliyemfikia Bwana Mackenzie aliyekufa kwa namna ile ya kuhuzunisha niliyokwisha eleza.

Hatimaye tulilifikia lile ziwa liitwalo Laga, ambalo urefu wake wapata kadiri ya maili hamsini, na upana wake maili ishirini.

Ndipo tulipoendelea mbele kadiri ya mwezi mzima tulipita katika nchi yenye vilima vilima mfano wa mawimbi makubwa, na vichaka vilitapakaa huko na huko.

Wakati huo wote nchi ilikuwa imeinuka taratibu na kwa kweli ni mwinuko moja kwa moja mpaka kufika chini ya safu ya milima mingi yenye theluji juu ya vilele vyake.

Tulikuwa tukiiendea milima hiyo, maana tumepata habari ya kuwa ndiko liliko lile ziwa la pili ambalo yule msafiri alisema halina mwisho wa kwenda chini.

Mwisho tulipafikia, na tulipohakikisha ya kuwa ziwa liko juu ya kilele cha mlima, tulipanda tena kadiri ya futi elfu tatu mpaka tulipofika kwenye genge linaloteremka ghafla.

Tukaona chini yetu kadiri ya futi elfu moja na mia tano, liko ziwa lenye umbo la mraba na upana na urefu wake ulipata kadiri ya maili ishirini, ambalo halitoshi ni shimo la volcano ya zamani.

Tuliona miji iko kando ya ziwa, basi tuliteremka kwa shida katika mwitu wa misonobari iliyofunika miteremko ya shimo lile, tukapokewa vizuri na wenyeji wa huko ambao ni watu wa amani. Wasiopata kuwaona watu

weupe mpaka wakati huo; wakatutendea kwa heshima na wema, wakatupa chakula na maziwa kadiri tuliyotaka.

Siku tatu za kwanza tulizokaa huko, ilinyesha mvua, na mvua hii ndiyo iliyoanzisha sumu ya mbung'o katika punda wetu waliobaki, na wote walikufa.

Msiba huu ulituweka katika shida, maana sasa tulikuwa hatuna njia ya kuchukulia mizigo yetu, lakini kwa kweli, hatukuwa na vitu vingi vilivyobaki kuchukuliwa. Tena, risasi na baruti zilikuwa zimepungua sana.

Tulikuwa na risasi kadiri ya mia moja na hamsini, na risasi za marisaa hamsini tu. Hatukujua namna ya kuendelea mbele, ikawa kama tumekwisha fika mwisho wa safari yetu.

Lakini hata kama tungekuwa na nia ya kuliacha kusudi letu la kugundua yale tuliyokuwa tunayatafuta, ingekuwa jambo la upuuzi kufikiri habari za kurudi nyuma mwendo wa maili mia saba mpaka kufika pwani, hali hatuna zana za safari;

Basi, kwa kuwa wenyeji wa hapa ni wema, tulifanya shauri kukaa hapo tulipo na kungojea mambo yatakayotokea, na huku tunatafuta habari za nchi zilizo mbele.

Basi, tulinunua mtumbwi mkubwa mzuri wa kutosha kutuchukua sisi sote pamoja na vitu vyetu vilivyobaki, kwa mkubwa wa kijiji tulimokaa, tukaanza kusafiri ziwani kutafuta mahali pazuri pa kupiga kambi.

Kwa kuwa hatukujua kama tutakirudia tena kile kijiji, tulipakia mizigo yetu yote katika mtumbwi ule tena, tulichukua kipande cha nyama tuliyopika tayari, tukaondoka.

Wenyeji wengine walikuwa wametutangulia ili kuwaarifu wenyeji wa miji mingine kuwa tunakuja.

Tulipokuwa tukipiga kafi kwa taratibu, Bwana Good alisema jinsi maji ya ziwa yalivyo na rangi ya samawati, akasema.

Wenyeji, ambao ni wavuvi stadi wamemwambia kuwa ziwa hilo lina kina kirefu sana, tena lina tundu chini yake na maji yanatoka huku na kwenda kuuzima moto mkubwa sana unaowaka chini ardhini.

Nilisema kuwa habari hizi alizosikia, bila shaka ni mapekeo ya zamani sana, yalioanza wakati volcano za pande hizi zilipokuwa zingali zikitoa moto bado.

Tulipofika ng'ambo ya ziwa, tuliona ya kuwa kingo zake ni genge la mwamba linalopanda juu sana, wala hapana mahali linapoteremka kwa taratibu, basi, tuliliambaa genge hilo tukiuendea mwisho wa ziwa, maana tulijua ya kuwa kuna mji mkubwa huko.

Tulipokuwa tukienda tulianza kupita chungu nyingi za matete na majani na mashina ya miti na takataka nyingi zinazoelea juu ya maji, na Sir Henry alionyesha kundi la mabata weupe wakubwa waliokuwa wametua juu ya chungu nyingine, na sasa wanakula.

Nilikuwa nimekwishaona mabata wanarukaruka juu, nami sijaona namna yake katika nchi ya Afrika, nikataka kumkamata mmoja ili nimtazame vizuri.

Nilikuwa nimewauliza wenyeji habari za mabata hao, wakaniambia kuwa huja kutoka upande wa pili wa mlima majira Fulani ya mwaka, nao huja asubuhi, na kwa kuwa wamechoka, ni kazi nyepesi kuwakamata.

Niliuliza walitoka nchi ipi, lakini waliyatikisa mabega yao tu, wakasema kuwa juu ya genge lile ni nchi ya ukiwa, na kupita huko ni milima yenye theluji, imejaa wanyama wakali, wala hapana watu wanaokaa huko, na kupita milima ile ni mwitu mnene wa maili mia nyingi wa miti yenye miiba, hata tembo hawawezi kuupita, licha ya wanadamu.

Niliwauliza kama wamepata kusikia habari za watu weupe wanaokaa huko kupita milima na mwitu mnene wa miiba, wakanicheka tu.

Lakini baadaye mwanamke mzee sana alikuja akaniambia ya kuwa alipokuwa mtoto mdogo sana, babu yake alimwambia ya kuwa alipokuwa kijana, babu yake yeye alilivuka lile jangwa na milima, akaupenya mwitu

ule mnene wa miiba, akaona watu weupe waliokuwa wakikaa katika nyumba za mawe.

Lakini wakati ule aliosimulia yule mwanamke mzee ulikuwa zamani za miaka kadiri ya mia mbili na hamsini, na habari hazikuwa dhahiri sana lakini hata hivyo, habari zilikuwa zimetajwa tena, na nilipofikiri, niliona hakika habari nyingine tulizokwisha zisikia ni za kweli, nikakaza nia yangu lazima niigundue siri hii.

Wakati huo, sikusikia namna kusudi langu litakavyotimizwa kwa njia iliyokuwa kama muujiza.

Basi, tulianza kuwasaka wale mabata ambao walizidi kulikaribia lile genge, na mwishowe tulipeleka mtumbwi nyuma ya chungu ya takataka kadiri ya mwendo wa yadi arobaini kutoka mahali walipokuwapo, na Sir Henry aliitwaa bunduki yake ya marisaa, akailenga, akapiga wawili shingoni, wakafa.

Mara wale wengine waliopata thelathini au zaidi waliondoka kwa kishindo kikubwa na walipofanya hivyo alipiga tena, na mwingine alianguka amevunjika mbawa.

Basi, tulikwenda tukawaokota wale wawili waliouawa, tukaanza kumsaka Yule aliyeangushwa akawahi kupita juu ya chungu ya takataka na kuingia katika maji wazi tena.

Kwa kuwa tuliona shida kupenya zile taka taka kwa mtumbwi wetu, nilimwambia yule Mkazi aliyebaki, ambaye nilijua kuwa anaweza kuogelea vizuri, apige mbizi chini ya chungu ile ya takataka akamkamate yule bata, maana nilijua hakuna mamba katika ziwa hilo, naye hawezi kudhurika.

Basi, yeye aliona kama ni mchezo tu akajitosa majini akamfuata yule bata, na alipokuwa akimfuatia alilikaribia lile genge.

Mara nilimwona anaacha kuogelea kumfuata Yule bata, akaanza kupiga yowe ya kuwa anachukuliwa na maji na kweli tuliona yakuwa ingawa anaogelea kwa nguvu zake zote, lakini anavutwa kulikaribia lile genge.

Tulipiga kafi kwa nguvu tukapenya ile chungu ya takataka, tukamfuata kadiri tulivyoweza, lakini ingawa tulikwenda upesi sana, yeye alichukuliwa upesi zaidi kulikaribia lile genge.

Mara niliona mbele yetu kadiri ya nchi kumi na nane juu ya uso wa maji, liko tao kama ni mlango wa kuingilia pango linalopenya lile genge.

Basi, maskini mtumishi wetu alikuwa anavutwa na maji kuliendea pango lile kwa nguvu nyingi.

Nilipoliona lile pango, yeye alikuwa mbali nalo kadiri ya futi sitini, na sisi mbali kadiri ya futi mia moja na ishirini, na mtumbwi wetu ulikuwa unavutwa kasi bila sisi kutumia nguvu nyingi.

Alishindana kwa uhodari sana, nikadhani tutaweza kumuokoa, lakini mara niliona kuwa uso wake ya kuwa amekata tamaa , na mbele ya macho yetu alivutiwa katika lile pango akatoweka.

Mara ile he! Niliona kama kwamba mtumbwi wetu umeshikwa na mkono wenye nguvu nyingi mno na kuvutwa kwa nguvu isiyoweza kushindika kuliendea lile genge.

Sasa tuliona hatari iliyo mbele yetu, tukavuta kafi kwa nguvu ili tujiokoe tusivutwe katika maji yaliyokuwa yakizungukazunguka mbele ya mdomo wa pango.

Lakini juhudi yetu ilikuwa bure, na mara ile tulikuwa tunavutwa kuliendea lile pango kama mshale unaotoka kwenye upinde, nikafikiri tumekwisha potea.

Lakini kwa bahati sikushikwa na mfadhaiko, nikalia, ‘’Laleni chini!’’ nikajitupa chini katika mtumbwi, na wote walikuwa na akili kufanya vilevile.

Sasa tulisikia sauti ya kukwaruza, na mtumbwi ulisukumwa chini mpaka maji yalianza kuingia juu ya mbavu zake, nikafikiri huu ndiyo mwisho wetu, lakini kwa ghafla sauti ile ilikoma, nikaona kuwa mtumbwi ungali unaendele mbele.

Nilikigeuza kichwa changu kidogo sikuthubutu kukiinua nikatazama juu. Kwa mwangaza kidogo uliokuwako, niliona tumo pangoni, na juu yake ni mwamba wenye umbo la tao.

Baada ya kupita dakika, kama tano sikuweza kuliona, maana mwangaza ulitoweka, tukawa katika giza tupu.

Basi, kwa muda wa saa moja hivi tulilala, wala hatukuthubutu kuviinua vichwa vyetu visije vikapiga mwamba wa juu, nasi hata kusema hatukuweza kusema kwa sababu sauti ya maji yaliyokuwa yakipita kasi ilizimeza sauti zetu.

Na kwa kweli hatukuwa na moyo wa kusema, hali tumeshikwa na mashaka kwa hatari tuliyomo, na hofu ya kufa wakati wowote ama kwa kutupwa kwa nguvu kando ya pango, ama kuvutiwa chini katika maji yanayozunguka zunguka kwa nguvu, ama kusongwa kwa kutokuweza kuvuta pumzi.

Basi, namna hizi za kufa na nyingine nyingi zilipita katika fikra zangu nilipokuwa nimelala chini katika mtumbwi, nilisikiliza sauti kubwa ya maji yaliyokuwa yakienda kasi, sipajui wapi. Kweli hali zetu ilizipoozesha akili zangu, nikaanza kufikiri nimeshikwa na jinamizi la kutisha sana.

SURA YA KUMI

Mbele, mbele tukaendelea mbio sana, tunavutwa na mkondo wenye nguvu hata halafu nilisikia sauti ya maji imepungua sana, nikafahamu ni kwa sababu iko nafasi zaidi na sauti imeenea.

Basi, nilijiinua pole pole na kwa uangalifu sana mpaka nikafanikiwa kupiga magoti, nikaunyosha mkono wangu juu, nisiweze kugusa kitu. Kisha, nilitwaa kafi nikaiinua juu, nisiguse kitu.

Tena, nililipeleka upande wa kuume na wa kushoto, lakini sikuweza kugusa kitu ila maji tu. Ndipo nilipokumbuka ya kuwa ipo taa na debe la mafuta katika mtumbwi, nikapapasa papasa huku na huko mpaka nikavipata, nikawasha kiberiti kwa uangalifu, nikaiwasha taa.

Nikatazama, nikamwona Bwana Good amelala chali anatazama juu tu, na Sir Henry amekiegemeza kichwa chake ubavuni mwa mtumbwi, na mkono wake umo majini akijaribu kuupima mwendo wa maji.

Lakini mwangaza ulipomwangazia Umslopogaas nilitaka kucheka. Nilisahau kusema ya kuwa tulichukua pande la nyama iliyopikwa, basi , tulipojitupa chini katika mtumbwi tusipigwe na mwamba wa juu, kichwa cha Umslopogaas kilifika karibu na ile nyama, na mara alipoizoea hali yetu aliona njaa.

Basi, hapo alilitwaa shoka lake akakata kipande cha nyama, na sasa anaila kwa raha. Alieleza baadaye, ya kuwa, katika kwenda safari ndefu, hupenda kushiba kwanza!

Wenzangu walipoona nimeiwasha taa, tulianza kufanya shauri juu ya hali zetu kadiri tulivyoweza.

Kwanza kwa shauri la Bwana Good tulizifunga kafi mbili pamoja, tukazisimamisha ka mlingoti katika omo la mtumbwi ili tupate habari mara ile ikiwa mwamba wa juu kama sehemu nyingi ni fupi kwa kimo tusije tukajigonga.

Ilikuwa dhahiri ya kuwa tumo katika mto unaopita chini ya ardhi unaochukua maji ya ziwa yanapozidi.

Mito ya namna hiyo ipo katika nchi nyingi, lakini nadhani wasafiri wachache wamepata bahati mbaya ya kusafiri ndani yake.

Kwa mwangaza wa taa yetu tuliweza kufahamu ya kuwa mto ni mpana, maana nuru ya taa haikuweza kufika mpaka mwisho wa kando zake.

Mara kwa mara mkondo wa maji ulituchukua karibu na ng'ambo hii au hii, tukaona ni mwamba ambao, kadiri tulivyoweza kuona, unafanya namna ya tao kiasi cha futi ishirini na tano juu yetu.

Ingawa mwamba ulikuwa juu hivyo, tuliona ni afandali tuweke mtu mmoja mbele katika mtumbwi ashike zamu, ana taa na podo tayari kuzuia mtumbwi usisetwe kando ya mto, wala kupigwa na mwamba ukiwa mmoja unatokeza mahali.

Kwa kuwa Umslopogaas tayari amekula, yeye alishika zamu ya kwanza, hapo tulikula nyama kidogo tu, maana hatujui chakula chetu kitachukua muda gani.

Ndipo tulipochangamka kidogo, nikatoa shauri langu ya kuwa hali yetu si hali ya kukata tamaa kabisa, ila labda mto huu utoweke kabisa katikati ya dunia, kama walivyosema wale wenyeji.

Kama hautoweki, basi lazima utatokea mahali, labda upande wa pili wa milima, na kama ni hivyo, basi hatuna budi kujiokoa maisha yetu mpaka tufike huko.

Lakini Bwana Good alisema labda tutapatikana na hatari na vitisho vingi sana au labda mto huu utatambaa chini ya ardhi mpaka ukauke, na kama ni hivyo, basi ajali yetu itakuwa mbaya kabisa.

Basi, Sir Henry, ambaye siku zote ni mchangamshi, na kwa kweli yu kama nguzo yenye nguvu wakati wa shida, akasema, ‘’Basi, imetupasa tuamini kuwa mambo yatatokea vizuri, au kujitengeneza tuwe tayari ikiwa yatatokea vibaya.

Tumetoka katika shida nyingi pamoja, nami nadhani tutatoka katika shida hii pia.

Ilikuwa karibu saa sita tulipovutiwa chini ya ardhi, na mtu wa zamu ya kwanza aliwekwa saa nane, tukapatana ya kuwa kila zamu itakuwa kwa muda wa saa tano.

Umslopogaas na Bwana Good walishika zamu ya kwanza. Basi, ilipofika saa moja ya usiku, Sir Henry na mimi tulishika zamu, na wale wawili wengine walilala.

Kwa muda wa saa tatu mambo yalikwenda vizuri ndipo nilipoanza kuona joto linazidi. Kwanza sikufikiri neno lakini baada ya kupita nusu saa tena niliona joto linazidi sana, nikamwita Sir Henry, nikamuuliza kama na yeye anaona joto, au kama ni mimi tu ninayeona hivyo. Akajibu, ‘’Ndiyo, jasho linanitoka kwa wingi sana.’’

Basi, hapa wenzetu waliamka wanatweta kwa joto, tukaona ni lazima tuzivue nguo zetu, isipokuwa Umslopogaas aliyekuwa amevaa ngozi.

Joto likazidi mno, na jasho lilitutoka kama maji yanavyo miminika. Baada ya kupita nusu saa tena, ingawa tulikuwa tupu, tuliona shida kuvumilia joto kwa jinsi lilivyozidi.

Nikauchovya mkono wangu majini, nikautoa haraka, nikataka kupiga kelele, maana maji yalikuwa moto sana, karibu kuchemka.

Sir Henry akasema kuwa, labda tunapita juu ya mahali penye moto wa volcano chini yake, nami nadhani alisema kweli na hasa kwa sababu ya mambo yaliyotokea baadaye.

Sasa taabu yetu ilizidi hata nashindwa kuieleza, maana hatukutoka jasho tena kwa sababu jasho lote limekwisha kututoka, na sasa tumelala tu chini mtumbwini, tukauacha uchukuliwe na maji tukajiona kama kwamba tu makaa ya moto.

Ngozi yetu ilianza kupasuka, na damu ilipigana katika mishipa ya vichwa vyetu. Basi, mambo yaliendelea hivyo hivyo kwa muda, ndipo mto

ulipopinda kidogo, nikamsikia Sir Henry anatoa sauti ya kushtuka, nikatazama mbele nikaona jambo la ajabu na la kufadhaisha kabisa.

Kadiri ya nusu ya maili mbele yetu, na kwa upande wa kushoto wa katikati ya mto, tuliona nguzo ya moto mweupe unabubujika katika mto na kupanda juu kadiri ya futi hamsini, ulikuwa ukiupiga mwamba wa juu na kutawanyika mpaka kuwa mkubwa sana, kadiri ya futi arobaini kuuzunguka, kisha ukarudishwa chini kama matao.

Nguzo hii ya moto ilionekana kama kwamba ni ua kubwa ajabu la moto linalotoka katika maji meusi ya mto.

Chini, nguzo ilifanana na kikonyo cha ua, kimenyoka vizuri, na unene wake ulipata futi moja au zaidi na matao ya juu yake yalifanana na majani ya ua kubwa la moto. Nani anayeweza kueleza jinsi lilivyokuwa zuri na lakutisha! Hakika mimi siwezi.

Ingawa tuko mbali kadiri ya yadi mia tano, moto huo ulilianga pango zima kama kwamba ni mchana. Basi, tulipelekwa mbele kasi kuiendea nguzo hiyo ya moto, na moto ulimeka kwa ukali kuliko tanuru yoyote iliyowashwa na mwanadamu.

Sir Henry akalia, ‘’Peleka mtumbwi kuume, Quatermain… kuume!’’ na mara ile nilimwona ameanguka chini katika mtumbwi amezirai. Bwana Good naye alizirai pia. Walilala wale kama kwamba wamekwisha kufa.

Umslopogaas na mimi tu ndiyo tuliokuwa na fahamu zetu. Sasa tulikaribia zaidi, kadiri ya yadi hamsini tu, nikaona kichwa cha yule Mzulu kinainamia mbele katika mikono yake. Yeye naye amekwisha zirai, na mimi nimebaki peke yangu.

Sikuweza kuvuta pumzi moto mkali ulikuwa umenikausha kabisa. Mwamba wote uliozunguka mto, pale moto ulipokuwapo, ulikuwa unameka wekundu na mti wa mtumbwi wetu ukataka kuungua.

Nikaona manyoya ya bata mmoja katika wale tuliowaua yanasinyaa na kuungua lakini sikukubali kushindwa.

Nilijua ya kuwa mimi nikishindwa, basi tutakuwa tumekwisha, maana tutapita katika mwendo wa yadi tatu au nne wa moto ule na kuangamia kwa maumivu makali kabisa.

Basi, nilitia kafi majini ili kuupinda mtumbwi wetu upite mbali na moto kadiri nilivyoweza, nikaizuia kwa nguvu. Macho yangu yalikuwa kama yanatoka kichwani, na ingawa niliyafumba, niliweza kuuona mwangaza mkali wa moto.

Sasa tulikuwa karibu kuukabili; ulinguruma kama moto wa jehanamu, na maji yaliyozunguka yalikuwa yanachemka kwa hasira sana.

Nukta tano zaidi zilipita. Basi, tumeupita nikasikia muungurumo wake nyuma yangu.

Ndipo na mimi pia nilipoanguka chini mtumbwini, nimezirai.

Nilipopata akili zangu tena, niliona upepo unaupepea uso wangu. Nikayafumbua macho yangu kwa shida, nikatazama juu.

Juu, juu sana, niliona mwangaza, ingawa giza lilinizunguka pande zote. Ndipo nilipopata fahamu, nikatazama.

Mtumbwi ungali unaelea katika mto, na katika mtumbwi, chini, wenzangu wamelala tupu. Nikawaza, ‘’Je, wamekwisha kufa nini? Je, niko peke yangu katika mahali hapa pa kutisha’’ Sikujua.

Ndipo nilipoanza kuona kiu imenishika. Niliuchovya mkono wangu majini, nikauvutia ndani tena kwa haraka sana na huku ninalia. Maana karibu ngozi yote ilikuwa. Imebabuka. Lakini maji yalikuwa baridi sana, badaye nikayatwa nikanywa sana, nikajimiminia maji.

Mwili wangu ulikuwa kama kwamba unapapa maji kama kiambaza kinavyopapa mvua baada ya wakati wa jua kali lakini pale nilipoungua palinichoma mno.

Ndipo nilipowakumbuka wenzangu, nikajivuta karibu nao kwa shida nyingi, nikawanyunyuzia maji, nikafurahi sana, maana walianza kuamka

kwanza Umslopogaas, halafu na wale wengine.

Kisha, na wao walikunywa maji mengi. Sasa walianza kuona baridi kinyume kabisa cha hali yetu ya karibuni tukaanza kuvaa kadiri tulivyoweza, maana tulikuwa tumeungua sana.

Tulipokuwa tukifanya hivyo, Bwana Good alionyesha namna ubavu wa kushoto wa mtumbwi ulivyoungua kwa moto.

Moto ule wa kutisha ulikuwa nini sijapata kujua, lakini nadhani haukosi uko ufa ardhini chini ya mto, na moto ule unatoka katikati ya dunia.

Mara tulipovaa nguo na kupata nguvu kidogo, tulianza kujaribu kutambua tuko wapi sasa. Nilisema ya kuwa niliweza kuona mwangaza kwa juu sana, na tulipoutazama, tulitambua kuwa ni mbingu.

tukatambua ya kuwa mto ulikuwa chini ya ardhi, na sasa umetokea tena, nao unapita katikati ya magenge marefu kadiri ya futi elfu mbili kwenda juu.

Juu sana tuliona mbingu ni nyeupe, lakini hapo tulipo ni nusu giza, kama katika chumba kilichofungwa milango na madirisha wakati wa mchana.

Kando ya maji palikuwa na ukingo upana wa yadi saba au nane wenye mawe yaliyoviringana kwa kusukumwa na maji.

Basi, tulikusudia kuteremka hapa ili tupumzike kidogo baada ya hatari zote zilizotupata, na kuvinyoosha viungo vyetu.

Mahali hapa palikuwa pa kutisha sana, lakini panafaa kupumzikia katika hatari na vitisho vya mto, na kutupa nafasi ya kupanga vizuri vitu vilivyomo mtumbwini.

Basi, tulichagua mahali, tukaupweleza mtumbwi kwa shida, kisha tukateremka katika mawe yale.

Bwana Good alishuka ukingoni kwanza, akasema kwa sauti kubwa, ‘’Lo, ama mahali hapa pabaya mno! Panatosha kumtia mtu kifafa,’’ akacheka.

Mara ile sauti kubwa ilikariri maneno yake, ikayazidisha mara nyingi sana. ‘’Kifafa ho!ho!ho!- Kifafa ho!ho!ho!’’ na sauti nyingine ikaitikia juu sana katika genge, ‘’Kifafa! Kifafa! Kifafa!’’ na sauti ilifuata, sauti ikachanganyika pamoja na sauti ya kucheka, mpaka mahali pote palilia, kisha ikatulia tena ghafla kama ilivyoanza.

Umslopogaas akasema kwa utulivu, ‘’Ah! Naona ya kuwa mashetani wako hapa, na kweli mahali hapa paonekana kama ni mahali pa mashetani.’’ Nilijaribu kueleza ya kuwa sauti zile tulizozisikia ni mwangwi tu, lakini hakusadiki.

Akasema, ‘’La mimi naweza kuutambua mwangwi niusikiapo. Mmoja ulikaa karibu na nyumba yangu huko katika nchi ya Umla na vijana wa kike walizoea kuongea nao. Lakini kama huu ni mwangwi, basi ule wa kwetu ulikuwa mtoto wa mwangwi tu! La, la, ni mashetani.

Lakini hata hivi naona si mashetani kitu,’’ akanusa tumbako, ‘’wanaweza kukariri maneno ya mtu, lakini hawawezi kusema maneno yao wenyewe, tena, hawathubutu kujionyesha’’. Akanyamaza, kama kwamba anawadharau mashetani hao.

Baada ya hayo tuliongea kwa sauti ya kunong’ona, maana tulichukizwa kusikia kila neno tunalolisema linatupwa huko na huko kama mpira katika mchezo.

Lakini hata sauti za kunong’ona zilitambaa katika magenge kama sauti za siri, mpaka zilipofifia kama mivumo ya upepo.

Mara tulipotua juu ya mawe yale, tuliyaosha na kuyaganga majeraha yetu ya kuunguzwa moto kadiri tulivyoweza.

Tulikuwa na mafuta kidogo kwa taa yetu, kwa hivi hatukuweza kuyatumia kuyatibu majeraha yetu, basi, tulimnyonyoa bata mmoja, tukatumia mafuta ya kidari chake, yakatufaa sana.

Kisha, tuliviweka vitu vyetu vizuri katika mtumbwi, tukaanza kula, nasi tulikuwa na njaa sana ya chakula, maana tulikuwa tumezirai kwa muda wa saa nyingi, na sasa ilipata saa sita.

Basi, tulikaa tukaanza kula nyama baridi, lakini tulikuwa dhaifu tukataka kutapika, tena, vichwa vilituuma kwa ajili ya taabu za usiku.

Halafu kidogo. Niligeuka nitazame nyuma yangu, nimevutwaa na sauti niliyosikia kama kwamba kitu kinatambaa juu ya mawe, nikaona kaa mkubwa sana wa maji baridi amekaa juu ya mwamba. Alikuwa mkubwa sana kama bata watano kiasi cha bata wakawaida.

Mnyama huyu wa kuchukiza alikuwa na macho yaliyotokeza, yakawa kama yananiangalia, tena, alikuwa na mikono mirefu na magando makubwa sana.

Basi, hapo wanyama wengi kama huyo walitoka kila upande, labda walivutwa na harufu ya chakula, wakatoka nyuma ya mawe na katika matundu ya mwamba.

Wengine walitukaribia sana. Mara ile mmoja alimuuma Bwana Good kwa nguvu sana, akalia kwa sauti kubwa, kisha kwa mara nyingine tena mwangwi uliirudiarudia sauti ile.

Umslopogaas alilitwaa shoka lake akamvunja yule kaa, na mara ile yule kaa alilia kwa sauti kubwa, na mwangwi uliirudisha sauti yake iliyo chukiza sana. Mara akaanza kutoa povu kinywani, na wengi wengine wakaja kutoka kila mahali.

Wale walipoona ya kuwa mwenzao ameumia, walimrukia wakaanza kumraruararua kwa magando yao makubwa, wakavitia vipande vya nyama yake vinywani mwao.

Basi, tulishika vitu vyovyote tulivyoweza kupata, tukaanza kupigana nao. Walizidi kujazana tele, wakatoa harufu mbaya sana.

Kila tulipomuua mmoja, wenziwe walimrukia wakamraruararua na huku akitoa povu kinywani mwake tena kila walipopata nafasi walituuma na sisi pia, wakajaribu kuiba chakula chetu.

Mmoja mkubwa sana alimrukia bata mmoja tuliyemnyonyoa, akajaribu kumchukua, na mara ile wengi sana walijitupa juu yake wakaanza kulialia na kutoa povu vinywani wakaila nyama yake na huku wakiraruana pia.

Basi, hapa Bwana Good akasema, ‘’Haraka tuondoke hapa au kweli tutashikwa na wazimu.’’

Basi, tuliusukuma mtumbwi wetu ambao ulizungukwa na wanyama hao wengi sana, tukaushusha mtoni, tukaingia ndani, tukatoka pale tukawaacha wanyama hao wanalialia na kutoa povu linalo nuka vibaya.

Umslopogaas akasema, ‘’Wale ni mashetani wa mahali hapa.’’ Na sisi tulielekea kuyakubali maneno yake.

Sir Henry akasema, ‘’Na sasa tutafanya nini?’’ Nikajibu, ‘’Tuache mtumbwi uchukuliwe na maji tu.’’ Basi, tukauacha uchukuliwe tangu mchana hata jioni, wala hatuna habari kuwa usiku unaingia kwa sababu ya giza la mahali hapo, mpaka Bwana Good alipoonyesha juu tukaona nyota angani.

Basi, kwa kuwa hatuna la kufanya, tulikaa tukiiangalia ile nyota, na mara ilitoweka, na giza likazidi tena, tukaanza kusikia muungurumo wa maji tena, nikaguna nikasema, ‘’Tumeingia chini ya ardhi tena.’’ Nikaangaza taa.

Ndiyo, bila shaka, tumekwisha ingia chini tena tukaweza kuona mwamba wa juu ya mto. Basi usiku mwingine wa hatari na hofu ukaanza.

Sitaweza kuyaeleza mambo yaliyotokea tutachoshana tu, basi, yatosha kusema ya kuwa ilipopata karibu na saa sita ya usiku, tulipiga mwamba uliotokeza katikati ya mto, tukawa karibu kupinduka na kutoswa majini.

Lakini tuliwahi kuutoa mtumbwi na kuendelea tena. Basi, hivi saa zilipita mpaka karibu na saa tisa.

Sir Henry na Bwana Good walikuwa wamelala, wamechoka kabisa, na Umslopogaas akawa amekaa mbele ameshika pondo, na mimi, nilikuwa nikiuongoza mtumbwi.

Mara nilimsikia Umslopogaas anatoa sauti, na mara ile nilisikia sauti ya kucharuka kama kwamba kitu kinapenya katika matawi ya miti, nikaona ya kuwa mtumbwi wetu unapenya kwa nguvu katika miti na matawi yanayotambaa.

Kisha, nikaona upepo mzuri unaupepea uso wangu, nikajua kuwa tumetoka tena katika chini ya ardhi na sasa tunaelea juu ya maji wazi.

Sikuweza kuona kitu kwa macho yangu kwa sababu ya giza la usiku, lakini nilifurahi kuona tumekwisha toka katika mto ule wa kutisha. Basi, nilikaa nikivuta hewa nzuri katika mapafu yangu, nikayangoja mapambazuko kwa saburi nilivyoweza.

SURA YA KUMI NA MOJA

Kwa muda wa saa nzima nilikaa tu nikiyangojea mapambazuko, na huku Umslopogaas pia alikuwa ameshikwa na usingizi.

Nikakaa mpaka upande wa mashariki ukageuka rangi ya kijivu, na ukungu ukatambaa juu ya uso wa maji kama vivuli vya mapambazuko yaliyo kwisha sahauliwa zamani, Ulikuwa unaotoka katika kitanda chake cha maji kuliamkia jua.

Kisha, rangi ya kijivu iligeuka ya manjano, na ya manjano ikageuka nyekundu.

Kisha, miali mizuri ya nuru ilitoka katika mbingu za mashariki, na sasa katikati yake dalili za mapambazuko zikaja mbio kama mishale, zikatawanya ukungu na vivuli na kuvigusa vilele vya milima ya mbali katika mwendo wake wa kuruka toka mlima mpaka mlima.

Ndipo milango ya dhahabu ikafunguliwa mbinguni na jua lenyewe likachomoza kwa utukufu na sherehe na uzuri na mng'ao wa mikuki mingi, likaufunika usiku kwa nuru na mwangaza, kukawa kweupe.

Mpaka sasa sikuweza kuona kitu ila mbingu zenye rangi ya samawati, maana ukungu mnene ulitanda juu ya uso wa maji, kama kwamba uso wake wote ulikuwa umefunikwa kwa utando wa pamba.

Lakini kidogo kidogo jua lilikunywa ukungu, ndipo nilipoona ya kuwa tunaelea juu ya ziwa kubwa la maji maangavu, ambalo kingo zake hazionekani.

Nyuma yetu kadiri ya maili kumi hivi, milima mirefu sana ilitanda upeo wa macho, ikafanya namna ya ukuta uliolizuia ziwa lile, nami sina shaka ya kuwa mto ule uliotuchukua unatoka mahali katika ukuta ule wa milima.

Na kwa hakika nilithibitisha habari hizi baadaye, na nguvu za mwendo wa mto ule zilikuwa dhahiri. Maana hata sasa mtumbwi wetu ulikuwa

ukipelekwa mbele kwa nguvu za maji.

Halafu kidogo wenzangu waliamka, wakafurahi mno walipoona kuwa tumetoka katika mto ule wa kutisha, na sasa tuko chini ya mbingu za samawati tena.

Ndipo tulipochangamka tukaanza kuongea na kufikiri shauri la kufanya, tukakusudia kuutafuta ukingo wa ziwa, maana tuna njaa sana, wala hatuna kitu cha kula isipokuwa vipande vichache vya nyama kavu.

Tulikuwa tumepoteza chakula chote kilivyoliwa na wale kaa wa kuchukiza. Basi, sasa shida nyingine ikazuka.

Hatujui bado ukingo wa ziwa u wapi, maana hatuwezi kuona kitu ila utando mkubwa wa maji maangavu yenye rangi ya samawati na milima ile tulikotokea.

Lakini tuliona ndege maji wengine wanaruka toka upande wa kushoto, tukabahatisha ya kuwa wanatoka mahali pao kando ya ziwa wanapokula chakula ili wakashinde ziwani mchana, na kwa hivi tulielekea upande huo, tukaanza kupiga kafi.

Baada ya kupita kitambo, upepo ulianza kuvuma kwa nguvu na kutupeleka huko tulipotaka kuendeea.

Basi, tulitengeneza tanga kwa blanketi na mti, tukapelekwa mbele vizuri. Kisha, tulikula vile vipande vya nyama kavu vilivyosalia, tukanywa maji matamu ya ziwani, tukatia moto viko vyetu, tukangojea mambo yatakayotokea.

Tulipokuwa tumekwenda muda wa saa moja, Bwana Good ambaye alikuwa akitazama huko na huko kwa darubini, akasema kuwa anaweza kuona nchi kavu, akaeleza kwa kuwa jinsi rangi ya maji inavyobadilika inaonyesha kuwa tunakaribia mlango wa kuingilia mtoni.

Halafu kidogo tukaona kuba kubwa lenye rangi ya dhahabu linatokeza katika ukungu, na mara ile Bwana Good akatoa habari kubwa zaidi, yaani anaweza kuona mashua ndogo yenye tanga inatujia.

Habari hii, ambayo tuliweza kuihakikisha kwa macho yetu baadaye kidogo, ilitutatiza sana, yaani kufikiri kuwa wenyeji wa ziwa hii lisilojulikana wanajua jinsi ya kuendesha mashua kwa matanga.

Baada ya kupita muda kidogo ilikuwa dhahiri ya kuwa watu wale waliomo katika mashua wamekwisha tuona. Kwa muda kidogo walisita kama kwamba wanaona shaka, kisha, mashua ilitujia mbio mnoo.

Katika muda wa dakika kumi ilikuwa imekwisha tukaribia, na sasa ni mwendo wa yadi mia moja tu kutoka mtumbwi wetu, tukaona si mtumbwi ila ni mashua ndogo nzuri iliyoundwa kwa mbao, nayo ina tanga.

Lakini mara macho yetu yalivutwa kuwatazama waliomo ndani yake, ni mwanaume na mwanamke, nao rangi yao ni nyeupe, tulitazamana kwa ushangao tukifikiri macho yetu yamedanganyika, lakini sivyo, bila shaka ni kweli, hawakuwa weupe kama sisi, lakini hata hivyo si weusi.

Basi, kumbe, habari zile tulizozisikia zilikuwa kweli kabisa, nasi tumeongozwa kwa njia ya ajabu kuligundua lile taifa la watu weupe.

Nilitaka kupiga ukelele wa furaha nilipokumbuka ukuu wa ajabu ya jambo hili, tukapeana mikono, tukafurahi kwa sababu safari yetu imesitawi kupita tulivyoweza kutumaini.

Maisha yangu yote nilikuwa nimesikia tetesi tu ya habari za taifa hili la watu weupe wanaoishia katika milima ya ndani ya nchi hii kubwa, nikatamani kuwaona kwa macho yangu, mwenyewe na kuithibitisha habari na sasa nimekwisha waona nimetosheka kabisa.

Yule mwanaume aliyekuwa ndani ya mashua alikuwa ana umbo zuri, ila si zuri kupita kawaida ya wanadamu, na nywele zake ni nyeusi za singa, uso wake ni mng’avu na wa kipanga.

Alikuwa amevaa namna ya gwanda rangi ya kahawia na namna ya shuka, Fupi ya kitambaa kile kile miguu yake ilikuwa mitupu.

Katika mkono wake wa kuume na wa kushoto amevaa bangili nene za madini ya rangi ya manjano nikaikisia ni dhahabu.

Yule mwanamke alikuwa mzuri wa kupendeza, na macho yake ni makubwa, na nywele zake ni za kuviringana zenye rangi ya kahawia.

Mavazi yake ni ya kitambaa cha namna ile ile ya yule mwanaume na baadaye nilipata kujua ya kuwa wanawake huvaa namna ya gwanda inayofika magotini.

Kisha kitambaa kirefu upana wake futi nne na urefu wake futi kumi na tano, kinachotandwa mwilini kwa mapindo ya kupendeza macho, na pindo lake lilitiwa rangi ya bluu au hudhurungi au rangi nyingine kulingana na cheo chake.

Vazi hilo hutupiwa begani na kuangukia mbele na mkono na ziwa la kuume huachwa wazi.

Mavazi hayo hupendeza sana hasa kama yule aliyevaa ni kijana mzuri kama mwanamke huyu alivyokuwa.

Huko nyuma ilikuwa sisi tunawashangaa wao na wao pia wameshangaa zaidi kutuona sisi.

Yule mwanaume alikuwa kama kwamba ameduwaa kwa kuwa na hofu, na kwa muda alisita kuja karibu na mtumbwi wetu asiukaribie zaidi. Halafu kidogo alitukaribia, akaanza kutuita kwa maneno ya lugha yenye sauti nyororo ya kupendeza masikio, lakini hatukuweza kufahamu hata neno moja.

Basi tulimwita kwa Kiingereza na kwa lugha nyinginezo tulizozijua, lakini hakuweza kufahamu hata neno moja. Ikaonekana kwamba sauti zetu zinamtia ushangao zaidi.

Yule mwanamke alikuwa anatuangalia sana. Basi, alipoona kuwa hawezi kutufahamu aliigeuza mashua yake akaanza kuiendea ng’ambo ya ziwa, na mashua yake ilikwenda mbio kama mbayuwayu.

Nikasema, ‘’Ni dhahiri yule mtu atarudi upesi pamoja na wenzake, basi afadhali tufanye shauri jinsi tutakavyo wapokea.’’

Sir Henry akasema, ‘’Mimi naona hakuna shauri ila jinsi wao watakavyo tupokea sisi’’

Bwana Good hakusema neno, ila alianza kushughulika na kutoa sanduku la chuma katika mizigo yetu.

Sir Henry akamuuliza, ‘’Je, unataka kufanya nini sasa?’’

Akajibu, ‘’Nataka kuvaa sasa. Je, wataka nionekane katika nchi mpya hali nimevaa nguo hizi?’’ Akaonyesha nguo zake jinsi zilivyokuwa zimechakaa na kuchafuka.

Basi, tulilishusha tanga, tukaoga ziwani tukarudi mtumbwini tena tumeburudishwa kabisa, tukakaa tukaota jua, na Bwana Good alilifungua sanduku lake akatoa nguo safi zake za kimanowari akazivaa.

Tulipomwona amevaa hivyo, sisi pia tuliona hamu ya kubadili nguo zetu, tukaanza kujitengeneza kadiri tulivyoweza, huku nyuma tulikuwa tunaikaribia ng’ambo ya ziwa polepole, maana mara tulipokwisha oga, tulilitweka tanga tena.

Baada ya saa moja na nusu tangu tulipoachana na yule mtu, tuliona namna ya jahazi na mashua nyingi zinatoka mtoni au bandarini. Katika vyombo hivyo kimoja kilikuwa kikiendeshwa kwa makasia ishirini na manne, lakini vingi katika vile vingine viliendeshwa kwa matanga.

Tulipoangalia kwa darubini, tuliona ya kuwa kile chombo kinaendeshwa kwa makasia kinaonekana kama kwamba ni chombo cha serikali, maana mabaharia zake wote wamevaa mavazi ya namna moja na mwanaume mzee mwenye ndevu nyeupe ndefu alikuwa amesimama mbele juu ya sitaha kama ni mkubwa wa chombo, nae amevaa upanga kiunoni.

Ni dhahiri watu waliomo katika vyombo vingine wamevutwa kwa udadisi, nao walikuwa wanatujia upesi walivyoweza.

Nilisema, ‘’Sasa tutaona Je, watakuwa marafiki au watatumaliza?’’ Hapana aliyeweza kujibu swali hilo, tukaona shaka kwa jinsi Yule mzee mwenye upanga alivyoonekana kuwa mtu wa vita.

Ndipo Bwana Good alipoona kundi la viboko majini kadiri ya yadi mia mbili toka mahali tulipo, akasema kuwa labda ni shauri jema kuwaonyesha wenyeji wale nguvu zetu kwa kuwapiga viboko hawa, yaani ikiwezekana.

Kwa bahati mbaya, hata na sisi tuliona ni shauri jema, basi, tulitwaa bunduki zetu kubwa tukaanza kujiweka tayari. Walikuwapo viboko wanne, dume mkubwa mmoja jike mmoja na watoto wakubwa wawili.

Tuliwakaribia bila udhia, na wale wanyama wakubwa walikuwa kama hawashuku hatari, walizama na kuibuka tena mbali kidogo tu, na kwa hakika niliona ni ajabu jinsi walivyokuwa kama wamefugwa. Basi, vyombo vile vilipotukaribia kadiri ya yadi mia tano.

Sir Henry alianza, akampiga mtoto wa kiboko. Risasi ilimpata katikati ya jicho, ikapita katika kichwa chake ikamuua akazama na kuacha mstari mrefu wa damu majini.

Mara ile mimi nilimwelekezea yule jike, na Bwana Good alijaribu kumpiga yule dume.

Risasi yangu ilipiga, lakini haikumuua, na yule kiboko alizama kwa kishindo kikubwa, akaibuka tena akinguruma na kutoa pumzi kwa nguvu, na kuyatia maji yaliyomzunguka rangi ya damu yake. Ndipo nilipompiga risasi nyingine nikamuua.

Lakini Bwana Good hana shabaha hata kidogo! Alikikosa kichwa cha yule dume, na risasi yake ikampaza tu uso alipokuwa akipita.

Nilipoangalia baada ya kupiga ile risasi ya pili, niliona kuwa wale wenyeji hawana habari za bunduki, maana vishindo vyake na jinsi viboko wale walivyopigwa viliwajaza ushangao na fadhaa. Watu wengine walilia kwa sauti za hofu na wengine walianza kurudi nyuma haraka.

Hata Yule mzee mwenye upanga alikuwa kama kwamba ameduwaa na kuona hofu, akakisimamisha chombo chake.

Lakini hatukupata wasaa kutazama sana, maana mara ile yule kiboko dume aliyekuwa amekasirika sana kwa ajili ya jeraha lililompata, aliibuka tena

karibu nasi, akatutazama kwa ukali mno.

Sote tulipiga bunduki zetu, tukampiga huko na huko, akazama tena amejeruhiwa vibaya. Sasa udadisi ulikuwa umewashika wenyeji wale ukauondoa woga wao, na wengine walitukaribia zaidi, na miongoni mwao ni yule mwanaume na mwanamke tuliowaona kwanza.

Hao walitukaribia sana. Mara ile yule kiboko dume aliibuka karibu na mashua yao, akakifunua kinywa chake, akanguruma kwa ghadhabu, akaishambulia mashua yao.

Yule mwanamke akapiga yowe, na Yule mwanaume akajaribu kuipeleka mashua upande, asiweze. Basi, sasa kinywa kikubwa chekundu cha kiboko chenye meno yanayong'aa kiliiuma mashua ile ndogo, kikaimega kipande kikubwa cha ubavu wake, na kuipindua.

Basi, mashua ilizama, na watu wale walibaki wanatapatapa majini. Kabla hatujaweza kufanya jambo la kuwaokoa, yule mnyama mkali aliibuka tena, akamshambuli kinywa wazi Yule mwanamke aliyekuwa akishindana na maji.

Mara kinywa chake kilipotaka kumuuma, nililenga bunduki yangu, nikapeleka risasi juu ya kichwa cha yule mwanamke, ikaingia sawasawa kinywani mwa yule kiboko.

Lo! Alipinduka, akaanza kuzunguka zunguka majini na huku anakoroma na kutoa damu nyingi puani, kabla hajajiweza tena, nilimpiga upande wa shingo, na risasi ikamuua.

Hakujimudu hata kujisogeza tena akazama pale pale. Sasa ikawa kazi ya kumwokoa yule mwanamke, maana yule mwanaume alikuwa ameogelea mpaka katika chombo kingine, tukamtoa katika maji tukamvutia katika mtumbwi wetu, na huku watu wanapiga kelele. Yule mwanamke alikuwa amechoka na kuogopa lakini hakuumia.

Huku nyuma vyombo vilikuwa vimesongana mahali pamoja, na wenyeji waliogopa sana, tukatambua kuwa wanashauriana.

Tulifikiri labda shauri lao litakuwa baya kwetu, kwa hivi tulizishika kafi zetu tukapiga kuwaendea mbele ili wasipate nafasi kulimaliza shauri lao.

Vyombo vingine vilirudi nyuma, na vingine vilikaa palepale, na kile cha yule mzee kikaja kutulaki.

Halafu tukiwa karibu sana, nikaona ya kuwa ameshangaa kutuona namna tulivyo, tena anaona hofu kidogo. Alikuwa amevaa mavazi kama yale ya yule mtu tuliyemwona kwanza, isipokuwa ngwanda lake ni la kitambaa cheupe chenye mapindo ya hudhurungi.

Bwana Good alivua kofia yake kumwamkia, akasema naye kwa Kiingereza, na yule mzee aliviweka vidole viwili mdomoni mwake, tukafahamu ni namna yao ya kuamkia, kisha alianza kusema maneno kwa sauti nzuri laini.

Lakini tulifanya ishara kumjulisha ya kwamba maneno yake hatuwezi kuyafahamu. Basi, hapa hatukuweza kufanya neno, nami kwa kuwa niliona njaa nikafikiri nimjulishe hivi, nikakifungua kinywa changu nikakielekeza kidole, kisha ninalisugua tumbo langu.

Basi, yule mzee alizifahamu ishara hizo, hapo akakielekeza kidole chake bandarini, na mtu mmoja katika chombo chake alitutupia kamba akatuashiria tuifungie mtumbwini mwetu, tukaifunga.

Basi chombo kile kikakivuta chetu kuiendea bandari kwa wepesi na vyombo vingine vilitufuatia.

Baada ya dakika ishirini tulifika mlangoni pa bandari, tukaona imejaa vyombo vilivyojaa watu waliokuja kutuangalia.

Tuliona ya kuwa watu wote ni wa namna ile ile, ila wengine ni weupe kupita wenzao. Basi baada ya kwenda mbele kidogo, mto ulipinda tukafanya sauti ya furaha na ya kushangaa, maana mbele yetu tuliona kwa mara ya kwanza mji wao ambao baadaye tuliambiwa unaitwa Milosis.

Mwendo upatao yadi mia tano tukafika kando ya mto, palikuwa na genge la miamba lililopanda ghafla kadiri ya futi mia mbili, na sehemu ya mbele ilitengenezwa iwe magadi ya vyombo.

Juu ya genge hilo palikuwa na jumba kubwa sana ambalo limejengwa kwa mawe ya namna ile ile ya miamba ya genge lile.

Jumba hilo lilikuwa limejengwa katika pande tatu za kiwanja chenye umbo la mraba, na upande wa nne wa kiwanja ulizibwa kwa ukuta mrefu wenye mlango mdogo tu wa kuingilia kiwanjani.

Baadaye tuligundua ya kuwa jumba hilo ni la malkia wawili wa nchi hii. Nyuma ya jumba, mji ulikuwa katika mwinuko wa mlima unaopanda taratibu mpaka juu yake, na huko palikuwa na jumba jingine la marumaru nyeupe lenye kuba ya dhahabu juu yake, ndilo kuba tulililoliona tulipokuwa tupo mbali bado.

Nyumba zote za mji zilijengwa kwa mawe mekundu isipokuwa jumba hilo, nazo zilikuwa zimepangwa kwa utaratibu na njia zake zilikuwa pana, nzuri.

Kadiri, tulivyoweza kuona, nyumba zote zilikuwa hazina ghorofa, na kila moja ilisimama peke yake imezungukwa na bustani.

Nyuma ya jumba la malkia, palikuwa na njia pana sana iliyopanda ule mwinuko kwa mwendo wa maili moja na nusu, mpaka kufikia kiwanja kilichokuwa mbele ya jumba lile la marumaru nyeupe lililosimama juu ya mlima.

Lakini mbele ya macho yetu tuliona kitu cha ajabu cha Milosis, ndiyo ngazi kuu ya kupandia genge mpaka jumbani kwa malkia, ambayo uzuri wake ulitushangaza sana.

Kutoka upande huu mpaka upande huu wa ngazi, ulikuwa uzio wa futi sitini na tano nayo ilikuwa imejengwa sehemu mbili; kila sehemu ilikuwa na vipandio mia moja na ishirini na tano, na kila kipandio kilikuwa cha mawe ukubwa wake inchi nane kwenda juu na futi tatu kwa upana.

Kweli ngazi hiyo ilikuwa kazi kubwa ya ustadi nasi tuliambiwa ya kuwa ngazi ilianzishwa zamani sana, ikaachwa mara nne kwa muda wa miaka mia nyingi kwa sababu wale waliojaribu kuijenga walishindwa, hata kijana mmoja jina lake Rademas alisema ya kuwa ataijenga, ama sivyo basi

atakubali kutupwa chini toka juu ya lile genge; lakini akishinda, basi lazima apewe binti wa mfalme amwoe.

Alipewa muda wa miaka mitano kumaliza kazi zote na alipata majengo na watu wa kazi kadiri alivyotaka.

Mara tatu alijaribu kujenga lakini ngazi iliporomoka , hata mwishowe yule kijana alitambua kuwa ameshindwa, alikusudia kujiua siku iliyofuata ile ilipoporomoka mara ya tano.

Lakini ilitokea usiku uleule alipokuwa amelala usingizini aliota ndoto na katika ndoto akaona mwanamke mzuri sana amekuja akamgusa pajini akayafunua macho yake, kumbe, aliona kama kazi zote zimekwisha.

Alioteshwa jinsi ya kuifanya, na kuzishinda shida zote alizokuwa nazo.

Basi, aliamka na mara ile alianza kufanya kazi kwa jinsi nyingine kabisa, na mwishowe alishinda, na siku ya mwisho ya miaka ile mitano aliyopewa alimwongoza binti wa mfalme kuipanda ngazi kuu ile mpaka katika jumba la juu.

Basi, baadaye aliurithi ufalme kwa haki ya mke wake akaanzisha ukoo wa wafalme wa huko, ukaitwa ‘’ukoo wa ngazi kuu.’’

Ndipo alipofanya ukumbusho wa kazi yake, akachora sanamu ya mawe ya yeye mwenyewe hali amelala usingizi akiota, na yule mwanamke mzuri anamwinamia na kumgusa paji la uso. Akaisimamisha sanamu hiyo katika sebule kubwa ya jumba, nayo imo humo hata leo.

SURA YA KUMI NA MBILI

Kile chombo kilichoendeshwa kwa makasia kilikuwa kinakimbia sana hadi kufika karibu na chini ya ile ngazi kuu.

Hapo Yule mzee aliteremka pwani akatuashiria tuteremke.

Hatukuwa na njia nyingine ila kutii, tena kwa kuwa tulikuwa nusura kufa kwa njaa, tulimtii bila kusita, lakini tulizichukua bunduki zetu pamoja nasi.

Tulipokuwa tukiteremka, Yule kiongozi wetu alijiinamisha na kuweka vidole viwili juu pa mdomo wake ili kutusalimu, na huku akawaamrisha watu wote waliokusanyika kututazama warudi nyuma watuachie nafasi.

Aliyekuwa wa mwisho kutoka katika mtumbwi ni Yule mwanamke tuliyemtoa katika maji, ambaye mwenzake alikuwa anamngojea, kabla hajaondoka alikuja akanibusu mkono yangu, nikafahamu anataka kunishukuru kwa kumwokoa katika hatari ya yule kiboko. Ikaoneka kwamba hofu imekwisha mwondokea.

Mara tulipoteremka kando ya ziwa, mabaharia wengine katika wale waliopiga makasia ya chombo kile, waliibeba mizigo yetu, wakaanza kupanda nayo katika ngazi ile kubwa, na kiongozi wetu alituashiria ya kuwa tupo salama.

Kisha aligeuka upande wa kuume akatuongoza katika nyumba, ambayo baadaye tulipata kujua ni nyumba ya wageni.

Tuliingia katika chumba kikubwa tukaona chakula kimeandaliwa tayari. Basi, kiongozi alituashiria tukae mezani.

Wala hatukungoja atukaribishe tena, ila tulikaa tukaanza kula kama watu wenye njaa walavyo, Chakula kilipakuliwa, katika sahani za mbao.

Tulikula nyama baridi ya mbuzi iliyofungwa katika majani ya namna yaliyoifanya iwe na ladha nzuri sana, na mboga ya namna, na mkate

mweusi; tena tulikunywa divai katika vikombe vilivyotengenezwa kwa pembe za wanyama.

Basi, baada ya kukaa na kula kwa muda wa dakika ishirini tuliondoka kama kwamba tu watu wapya.

Baada ya mambo yaliyotupata, tulikuwa na haja mbili, ndizo chakula na kupumzika, na chakula peke yake kilikuwa kama baraka kwetu.

Vijana wawili wanawake wazuri walitungojea mezani, nao walituhudumia vizuri sana.

Wote wawili walivaa mavazi ya namna ile niliyokwisha eleza.

Basi, mara tulipokwisha kula, mzee kiongozi wetu ambaye wakati huo wote alikuwa amesimama, alitutazama akamwashiria Bwana Good ambaye alimfikiria ni mkubwa wetu kwa ajili ya mavazi yake mazuri, akatuongoza chini ya ngazi ile kubwa.

Hapo tulisimama kidogo ili kustaajabia sanamu mbili za simba zilizochorwa kwa mapande makubwa ya marumaru nyeusi, moja upande huu wa chini ya ngazi na moja upande huu, Sanamu hizo za simba ni kazi ya ustadi mno, husemwa zilichorwa na yule mfalme mkuu Rademas aliyeijenga ile ngazi kuu.

Kisha tuliipanda ile ngazi ya ajabu na huku tunaishangilia. Hata Umslopogaas ambaye amezoea kutodhihirisha ushangao wake, alishtuka akauliza kama ‘’ngazi hii ilijengwa na wanadamu ama mashetani.’’

Basi, tulipanda sehemu ya kwanza ya ngazi, yaani vipangalio mia moja na ishirini na vitano, tukapita katika daraja kubwa kidogo lililoziunganisha sehemu zake mbili, tukasimama kidogo kustajabia nchi tuliyoiona chini yetu imepakana na kando ya ziwa la maji yenye rangi ya samawati.

Kisha tulipanda sehemu ya pili mpaka kufika juu kabisa, huko tuliona kiwanja chenye milango mitatu.

Milango miwili ilikuwa ya kuingilia njia nyembamba iliyozunguka nje ya ukuta wa jumba na kuteremkia mjini.

Njia hiyo hutumiwa na watu waendao bandarini. Milango hii ni ya shaba nyeusi, na sehemu ya njia iliyo karibu nayo inaweza kuteremshwa na kuacha nafasi wazi, ili kuzuia adui wasipite.

Mbele ya mlango wa tatu, ambao ulikuwa wa kuingilia ukuta wa jumba, palikuwa na ngazi nyingine yenye vipandio kumi vya marumaru nyeusi.

Ukuta wa jumba ulikuwa kazi ya sanaa kabisa, Ulijengwa kwa mapande makubwa ya mawe magumu na kimo chake kilipata futi arobaini na uso wake ulikuwa na uvungu, kwa hiyo haukuweza kupandika.

Basi, kiongozi wetu alituongoza mpaka mlango huo wa tatu, Mlango huu ni wa mbao nzito sana, na mbele yake uko mlango mwingine wa shaba nyeusi, ambao ulikuwa umefungwa lakini tulipoukaribia mara ulifunguliwa wazi, tukakuta askari wa zamu amesimama.

Silaha zake zilikuwa mkuki mzito uliofanana kidogo na singe, na upanga, naye alikuwa amevaa vipande vya ngozi ya kiboko vilivyotengenezwa vizuri, kifuani na mgongoni, tena, alikuwa ameshika ngao ya ngozi ya namna ile ile.

Upanga wake ulituvuta macho yetu, maana ulikuwa wa namna ile ile ya ule alioupata Bwana Mackenzie kwa Yule maskini msafiri.

Basi, ilidhihirika ya kuwa Yule mtu alikuwa amesema kweli. Kiongozi wetu alitaja neno ili aruhusiwe kupita mlangoni, na yule askari aiitikia kwa kupiga mpini wa mkuki wake chini kwa kishindo, tukapita mlangoni tukaingia katika ua wa jumba.

Ua ulipata kadiri ya upana na urefu wa yadi arobaini, nao ulikuwa umetengenezwa kama bustani nzuri ya miti midogo na maua.

Njia pana ilipita katikati ya ua, tukaifuata njia hiyo mpaka tukafikia mlango mwingine wenye tao juu lililotundikwa pazia zito, tukapita katika kichochoro kifupi tukaingi katika sebule kubwa ya jumba.

Tukastajabu tena kuona jinsi ilivyo nzuri ajabu, urefu wa sebule ni futi mia moja na hamsini, na upana wake ni futi themanini, na dari yake ni kuba la mbao zilizotiwa nakshi.

Mwisho wa sebule iko sanamu ile niliyotaja iliyotengenezwa kuwa ukumbusho wa kazi aliyofanya mfalme Rademas kuijenga ile ngazi kuu, na tulipopata nafasi kuitazama vizuri, uzuri wake ulitufanya kuwa kama mabubu.

Katikati kabisa ya sebule kulikuwa na mwamba wa marumaru nyeusi uliofanana kidogo na kiti.

Baadaye tulipata habari kuwa mwamba huu ni mwamba mtakatifu wa taifa hilo la ajabu, na wafalme huweka mkono juu yake waishapo kutawazwa, na kuapa kwa jua kuulinda ufalme na kuzihifadhi desturi na mapokeo na sheria zake.

Tuliambiwa habari za ubashiri wa kigeni juu ya mwamba huo, yaani utakapovunjiliwa mbali, mfalme wa taifa geni ataitawala nchi.

Mwisho wa sebule kulikuwa kuna namna ya jukwaa lililotandazwa mazulia mazuri, na viti viwili vya kifalme vya dhahabu tupu vilikuwa vimewekwa pamoja juu yake.

Viti hivyo vilikuwa vimetiwa matakia mazuri, na sehemu za kuegemeza migongo zilizochorwa sanamu ya jua linalotoa miali yake huko na huko kila upande.

Sehemu ya chini ya kuwekea miguu ni sanamu mbili za simba waliolala, na macho yao ni vito vyenye rangi ya kimanjano.

Sebule iliangazwa kwa madirisha membamba mengi yaliyokuwa juu sana ukutani, lakini hayakutiwa vioo.

Basi, ndivyo ilivyokuwa ile sebule kubwa ya jumba tuliyoiona, lakini hatukujua mambo hayo yote mpaka baadaye, maana hatukupata nafasi nyingi kuiangalia wakati huo, kwa sababu tulipoingia tuliona wanaume

wengi wamekusanyika mbele ya viti vile vya kifalme ambavyo vilikuwa vitupu.

Watu wakuu katika hao walikuwa wamekaa katika viti vya nakshi vilivyowekwa vingine upande wa kuume na vingine upande wa kushoto, lakini viti havikuwekwa mbele ya viti vile vya kifalme.

Watu hao walikuwa wamevaa namna ya magwanda meupe yenye nakshi za rangi mbalimbali, na walikuwa na panga zilizotiwa temsi za namna ya ule nilioutaja.

Wote walioneka kama ni watu wenye madaraja ya juu na nyuma yao wafuasi wachache walisimama wawangojee.

Kwa upande wa kushoto wa viti vya kifalme watu sita wa namna nyingine walikuwa wamekaa pekee yao.

Nao badala ya kuvaa shuka walikuwa wamevaa namna ya kanzu ndefu nyeupe za katani na kifuani zilipambwa kwa sanamu ya jua kwa nakshi ya zari, kama zile zilizochorwa katika viti vya kifalme.

Kila mmoja wao alikuwa amevaa mahazamu yenye vipande vya dhahabu kama magamba ya samaki vilivyoning'inia, vikang'aa katika mwangaza wa jua na kufanya sauti kila walipojongea.

Watu hao wote walikuwa wazee kidogo walionekana kuwa ni wenye fikra, na nyuso zao zilikuwa za namna nyingine, na tofauti baina yao na watu wengine ilizidi kwa sababu walikuwa na ndevu ndefu sana.

Lakini mtu mmoja katika watu hao aliyevuta macho yetu kuliko wengine. Alikuwa mzee sana, apata miaka themanini au zaidi, mrefu sana na ndevu zake zilikuwa nyeupe kabisa zilizofika mpaka tumboni.

Uso wake ulikuwa mkali, na macho yake yalikuwa ya kijivu na baridi sana tena yana sisimua kabisa.

Watu wote wengine walikuwa vichwa wazi, ila yeye alikuwa amevaa kofia iliyonakshiwa kwa zari, na kwa hiyo tulifikiri haikosi ni mtu mwenye cheo

kikubwa.

Na baadaye tulipata kujua ya kuwa ni Agon, kuhani mkuu wa nchi hii. Tulipokaribia wote na makuhani pia, waliondoka katika viti vyao wakajiinamisha kwa adabu, na huku wameweka vidole viwili mbele ya midomo yao kutusalimu.

Kisha watu wengine walitoka nyuma ya nguzo za sebule, wakaleta viti wakavipanga mstari mmoja mbele ya viti vya kifalme.

Tukakaa katika viti hivyo, ila Umslopogaas alisimama nyuma yetu. Mara tulipokaa tulisikia sauti ya panda ikitoka upande wa kuume, kisha sauti nyingine ya panda ikatoka upande wa kushoto.

Kisha mtu mmoja aliyeshika fimbo ya pembe nyeupe alisimama mbele ya kiti cha kifalme cha upande wa kuume.

Akasema maneno kwa sauti kubwa, na neno la mwisho ni Nyleptha, akalitaja mara tatu; kisha, mtu mwingine kama Yule akasimama mbele ya kiti cha kifalme cha upande wa kushoto, akasema maneno kama hayo, ile neno la mwisho lilikuwa Sorais, akalitaja mara tatu.

Ndipo tuliposikia vishindo vya watu wanaokuja toka upande huu na upande huu, na skari ishirini wenye silala waliingia toka upande wa kuume, na ishirini wakaingia toka upande wa kushoto, wakajipanga kuvizunguka viti vile vya kifalme, wakaikita mikuki yao chini kwa kishindo.

Kisha, tulisikia sauti mbili za panda tena, na Malkia wa Zuvendi waliingia, mmoja kutoka upande wa kuume na mmoja kutoka upande wa kushoto, kila mmoja amefuatana na mabibi sita, na watu wote sebuleni walisimama kama heshima kwao.

Nimeona wanawake wazuri katika maisha yangu, lakini maneno yangu hayawezi kabisa kuueleza uzuri wa maumbu Malkia hawa.

Wote wawili walikuwa vijana labda walikuwa na umri wa miaka ishirini na mitano wote wawili walikuwa warefu na wenye maumbo mazuri sana, lakini hapo basi, waliachana kabisa kwa namna uzuri wao ulivyo.

Mmoja wao, yaani Nyleptha alikuwa mweupe sana mwenye nywele za rangi ya dhahabu zilizoviringana kichwani, lakini ndugu pacha aitwaye Sorais alikuwa mzuri kwa namna nyingine, maana nywele zake zilikuwa nyeusi kabisa, na ngozi yake haikuwa nyeupe sana ila nyeusi kidogo.

Basi, wote wawili walipita kuviendea viti vyao vya kifalme, na walipokuwa wakipita nilifikiri jinsi walivyoonekana kuwa Malkia halisi.

Lakini hata hivyo, walikuwa wanawake zaidi ya Malkia, nao waliona udadisi, maana walipokuwa wakipita niliona ya kuwa wanayatupa macho yao upesi kututazama. Niliona macho yao hayakunitazama mimi sana, labda hawakupendezwa kuona mzee kama mimi.

Kisha, walimtazama Umslopogaas kwa ushangao! Naye akaliinua shoka lake kuwasalimu.

Kisha walimtazama Bwana Good, wakavutwa na mavazi yake mazuri, kisha walimtazama Sir Henry aliyesimama na huku mwangaza wa jua unazing'arisha nywele na ndevu zake.

Sir Henry aliyainua macho yake yakakutana na macho ya Nyleptha, na hivyo kwa mara ya kwanza mwanaume mzuri kupita wote na mwanamke mzuri kupita wote niliopata kuwaona walionana.

Nikafikiri moyoni, ‘’Sasa nadhali wanawake wameyaingilia matata yetu, basi pengine mambo yataenda vizuri zaidi,’’ Nikaguna kimya nikijua ya kuwa uzuri wa mwanamke ni kama uzuri wa umeme kitu kinachoharibu na kufanya ukiwa.

Basi nilipokwisha kufikiri hivyo, Malkia wote wawili walikuwa wamekwisha kaa vitini mwao, na panda zililia tena, na watu wote walikaa, na Malkia Sorais alituashiria tufanye vile vile.

Kisha, yule mtu aliyetuongoza ambaye alikuwa amerudi nyuma katika kundi la watu, alijitokeza amemshika mkono yule mwanamke tuliyemtoa katika hatari ya kiboko.

Alijiinamisha mbele ya Malkia, kisha alianza kusema. Hakosi alikuwa anasimulia habari za namna walivyotukuta.

Lilikuwa jambo la kuchekesha kuzitazama nyuso za Malkia walipokuwa wakisikiliza habari hizo, na namna zilivyoonyesha ushangao na hofu.

Ikawa dhahiri kuwa hawakufahamu namna tulivyolifikia ziwa lile na kuonekana tunaelea juu yake, wakaelekea kusadiki kuwa hatukufika kwa njia za kibinadamu.

Basi, yule kiongozi aliendelea kusimulia habari, na kwa jinsi alivyomuuliza yule mwanamke mara kwa mara nilitambua ya kuwa anasimulia habari za jinsi tulivyowapiga viboko wale.

Nikaona ya kuwa mambo yamekwenda upande wa habari za viboko, maana wale makuhani walidakiza maneno mara kwa mara kama kwamba wameudhika sana, na wale Malkia wawili walisikiliza na huku nyuso zao zimejaa ushangao, na hasa yule kiongozi alipowaonyesha bunduki zetu na kueleza ya kuwa ndizo zilizowaua wale viboko.

Basi, ni afadhali nieleze hapa ya kuwa Wazuvendi huliabudu jua, na yakuwa viboko ni mwiko kwao, wanahifadhiwa nao.

Si kwamba hawawauwi viboko, bali pengine huwaua wengi sana nao hutumia ngozi zao kufanyia ngao za askari.

Basi, kwa bahati mbaya, wale viboko tuliowaua walikuwa wamefungwa, nao walikaa mlangoni mwa bandari na kulishwa kila mara na makuhani ambao ulikuwa wajibu wao kuwaangalia.

Tulipokuwa tuna wapiga niliona kuwa walionekana kama kwamba ni wakufugwa, basi hii ndiyo iliyokuwa sababu yake.

Hivyo katika matendo yetu ya kuwaonyesha wenyeji nguvu zetu, kumbe, tumefanya jambo la kufukuru kuu kabisa.

Basi, kiongozi wetu alipokwisha simulia habari, yule kuhani mkuu Agon alisimama akatoa hotuba ndefu ya hasira.

Sikupenda namna alivyotukazia macho yake baridi ya kijivu, na kwakweli ningalimchukia zaidi kama ningalifahamu ya kuwa anadai kwa jina la Mungu wao, ya kuwa lazima tutolewe kafara kwa kuchomwa moto tungali hai.

Alipokwisha sema, Malkia Sorais alisema naye kwa sauti nzuri ya upole ikawa kama kwamba anashindana naye na kumweleza upande mwingine wa jambo.

Kisha Nyleptha, akasema kwa sauti nzuri, lakini hatukujua ya kuwa anasihi kwa ajili ya maisha yetu, ndipo pale alipo akasema na mtu mrefu mwenye umbo la kiaskari, ana ndevu nyeusi na upanga mrefu, ambaye tulipata kujua baadaye jina lake ni Nasta.

Naye ni mkuu wa nchi kubwa, akawa kama anamsihi amsaidie. Lakini ilitokea ya kuwa Sir Henry alipomtazama Nyleptha rangi ya uso wake iligeuka, na Nasta aliliona jambo hilo, akajiuma mdomo akaushika upanga wake imara zaidi.

Baadaye tulipata habari ya kuwa Nasta anataka kumwoa yule Malkia. Basi, ni dhahiri si mtu wa kumwomba msaada, na alipojibu alisema kwa sauti nzito kama kwamba anakubali shauri la kuhani mkuu Agon.

Alipokuwa akisema, Sorais alikuwa amekaa na huku ameshika tama, akamtazama Nasta na huku anacheka kidogo kama kwamba anazijua fikira zake, naye amekaza nia asishindwe naye.

Lakini Nyleptha alikasirika, na uso wake ulibadilika, na macho yake yaling'aa. Kisha aligeuka akamtazama Agon, ikaonekana kwamba anayakubali kidogo maneno yake, maana alikiinamisha kichwa chake; na alipokuwa akisema alipunga mikono yake ili kuyakaza zaidi maneno yake, na huku Sorais amekaa vile vile anacheka kidogo.

Kisha, Nyleptha alifanya ishara ghafla na panda zililia tena, na watu wote walisimama wakatoka sebuleni isipokuwa sisi na askari walinzi, maana alifanya ishara sisi tukae.

Walipokwisha toka, alijiinamisha mbele akacheka vizuri na kwa sauti na ishara alitufahamisha kwamba anataka kujua mahali tulipotoka.

Shida ilikuwa namna ya kuelezana, lakini nilipata akili. Katika mfuko wangu nilikuwa na kitabu cha kuandikia na kalamu, nikavitoa, nikachora ramani ya ziwa, na kwa namna nilivyoweza nilichora picha ya mto chini ya ardhi na ziwa upande mwingine wa mlima.

Basi, nilipofanya hivyo alifahamu, akapiga makofi kwa furaha, akashuka katika kiti chake akakipeleka kitabu kwa dada yake Sorais, na yeye pia alifahamu.

Kisha, akaitwaa kalamu na baada ya kuitazama kwa udadisi, alianza kuchora picha ndogo ndogo.

Picha ya kwanza ilifanana na yeye mwenyewe ameinyosha mikono yake kutupokea, na mtu mwingine aliyefanana na Sir Henry, anaipokea mikono yake.

Kisha, alichora picha ya kiboko anagaagaa majini kama anakufa, na ya mtu aliyefanana na kuhani mkuu Agon ameiinua mikono yake kwa ghadhabu amesimama kando ya ziwa.

Kisha, alichora picha ya moto mkubwa unaowaka, na ya Yule Agon anatuchochea katika moto kwa fimbo.

Basi, picha hizo zilitujaza kihoro, lakini nilitulia kidogo alipoanza kuchora picha nyingine ya mtu kama Sir Henry, na ya wanawake wawili niliowatambua kuwa ni yeye mwenyewe na dada yake Sorais.

Na kila mmoja ameuweka mkono mmoja kumkumbatia Bwana Henry, na kwa mkono mwingine wameushika upanga ili kumlinda.

Basi, Sorais aliyekuwa akituangalia sote, na hata Sir Henry, akafanya ishara kuonyesha kuwa fikira zake zinapatana na zile za dada yake.

Nyleptha alichora picha ya jua linaloanza kuchomoza, akafanya ishara ya kuwa sasa lazima aende, na ya kuwa tutaonana tena asubuhi.

Basi, hapo uso wa Sir Henry ulikunjamana, na Nyleptha alimpa mkono wake aubusu ili kumfariji akaubusu kwa heshima.

Basi, huku Sorais ambaye Bwana Good alikuwa anamtazama tokea mwanzo, alimpa mkono wake aubusu, lakini macho yake, yalikuwa yanamtazama Sir Henry tu.

Nafurahi kusema ya kuwa mimi sikuwamo katika mambo hayo, wala hakuna mmojawapo aliyenipa mkono wake niubusu.

Kisha, Nyleptha aligeuka akasema na uule mkubwa wa askari walinzi, ikaonekana kwa namna alivyopokea maneno kwa heshima, ya kuwa anatoa amri yenye nguvu; kisha, alituchekea akatoka sebuleni amefuatana na Sorais na wengine wa askari wa zamu.

Malkia walipokuwa wamekwisha toka, yule askari mkubwa aliyepewa amri za Nyleptha alikuja mbele na kwa ishara nyingi za heshima alituongoza kutoka sebuleni, na katika vichochoro vinginevyo mpaka katika vyumba vingine vyenye vyombo vizuri sana na mazulia na vitanda vizuri vizuri.

Vyakula vilikuwa vimeandaliwa mezani katikati ya chumba, na meza ilipambwa kwa maua.

Watumishi wanaume na wanawake walikuwapo kutuhudumia na huku kinanda kilikuwa kinapigwa mahali nje, tukajiona kama kwamba tu katika pepo ya duniani, na jambo tu lililotuudhi ni kufikiri ya kuwa yule kuhani mkuu anataka kukutupa motoni.

Lakini tulikuwa tumechoka sana hata tuliona shida tusishikwe na usingizi wakati tunapokula, na mara tulipokwisha kula tulifanya ishara ya kuwa tunataka kulala.

Basi, walituongoza wakataka kutupa kila mtu chumba chake peke yake, lakini tuliwaashiria ya kuwa tulala wote chumba kimoja.

Tena ili tusije tukashambuliwa ghafla, Umslopogaas alilala pamoja na shoka lake katika chumba kilichokuwa jirani.

Basi tulivua nguo zetu isipokuwa deraya za chuma tulizokuwa tumevaa ndani ya nguo zetu, tukajitupa vitandani tukajifunika kwa mashuka ya Hariri yenye nakshi.

Nilikuwa karibu kupata usingizi nilipoamshwa na sauti ya Bwana Good akasema, ‘’Je, Quatermain, ulipata kuyaona macho kama yale’’ nikajibu kwa haraka, ‘’Macho! Macho gani’’ akajibu, ‘’Macho ya Malkia. Macho ya Sorais!’’ nikapiga miayo nikasema, ‘’Sijui mimi, sikuyaangalia sana, labda ni macho mazuri.’’

Basi, baada ya dakika tano hivi niliamshwa tena kwa sauti yake, ananiita tena.

Nikasema, na sasa nimekasirika sana kuamshwa hivi, ‘’Je, unataka nini sasa’’

Akajibu, ‘’Je, ulipata kuona visigino vya miguu yake namna vilivyo vizuri .’’

Basi, hapa upuuzi wake ulinichosha kabisa. Nilikuwa nimeviweka viatu vyangu vizito karibu na kitanda nilicholalia, basi nilivitwaa nikavitupa vikampiga Bwana Good barabara. Baada ya hayo nililala sana.

Sijui habari za Bwana Good, sijui kama alilala au kama aliendelea kuota habari za uzuri wa Sorais.

SURA YA KUMI NA TATU

Sasa nitatoa habari kidogo za watu hawa tuliowafikia. Habari hizi tulizijua kwa maarifa tuliyoyapata baadaye.

Nchi hii huitwa Zuvendi, na jina lake hutokana na Zu, maana yake ‘’rangi ya kimanjano’’ na ‘’Vendi’’ maana yake ‘’mahali au ‘’nchi.’’

Sikuweza kupata kujua sababu huitwa nchi ya Kimanjano, wala wenyeji wenyewe hawajui. Lakini hutaja sababu tatu, na mojawapo yoyote inatosha kulieleza jina lake.

Kwanza husemwa nchi ilipata jina hili kwa wingi wa dhahabu iliyopo; sababu ya pili ni kwa kuwa majani ya nchi, ambayo ni mazuri na matamu, hugeuka rangi ya kimanjano katika majira moja ya mwaka na sababu ya tatu inatoka katika hadithi ya kuwa zamani wenyeji walikuwa wenye rangi ya kimanjano, ikageuka kuwa nyeupe baada ya kukaa miaka mingi katika nchi za juu.

Nchi ya Zuvendi imezungukwa pande zote na misitu minene ya miiba, na kupita misitu hiyo ni maili nyingi za mabwawa na majangwa na milima mirefu. Kwa kifupi ni kama meza kubwa iliyoinuka juu ya nchi ya katikati ya Afrika.

Nchi yenyewe haina joto jingi na ardhi yake ni nzuri sana, na namna zote za nafaka na matunda na miti husitawi sana, na katika mabonde namna moja ya miwa huota.

Kila namna ya madini inapatikana kwa wingi humo, isipokuwa fedha ambayo ni kidogo tu katika milima ya kaskazini.

Ina maziwa makubwa matatu, lililo kuu ni lile tulilotokea ambalo huitwa Milosis, sawasawa na jina la mji mkuu tena yamo maziwa madogo mengi, mengine yana maji ya chumvi.

Wenyeji ni wengi, wapata milioni kumi au kumi na mbili, na walio wengi ni wakulima. Asili ya watu hawa siwezi kujua hakika, na maandiko ya habari zao ambazo huendelea kwa muda wa miaka elfu moja hayataji asili yao.

Ingawa watu walio wengi ni wakulima, lakini pamoja na hayo ni watu wapendao vita pia, na ingawa kwa namna nchi yao ilivyo hawawezi kupigana na mataifa mengine, lakini hupigana wao kwa wao mara kwa mara.

Kwa desturi mfalme au malkia huitawala nchi lakini makuhani wana nguvu nyingi, pia baraza ya wakuu lina nguvu, na kama ilivyo katika nchi nyingi za dunia, amri ya mtawala pengine inapingwa na wakuu wenye raia wengi chini yao.

Wakuu hao hupingana wao kwa wao au kufanya amani na wenzao kadiri wapendavyo, na pengine hata hugombana na watawala wao na kujifungia katika ngome zao mbali na mji mkuu wa Milosis, nao hushindana na watawala wao kwa muda wa miaka mingi.

Sisi tulipofika, mfalme alikuwa amekufa zamani za miaka miwili, naye alikuwa mfalme wenye nguvu nyingi akazipunguza nguvu za makuhani na wakuu.

Alipokufa watoto wake wanawake mapacha walitawazwa kama ilivyo desturi ya nchi hiyo, maana kama mmoja tu angalitawazwa, raia wengine wangalifanya ghasia.

Lakini watu wengi walifikiri ya kuwa shauri hili si zuri, wala haliwezi kudumu. Na kwa kweli wakuu wengine waliotamani uwezo zaidi walikuwa wakifanya hila kumuoa mmoja wapo wa malkia, ikadhaniwa kwamba vita vitatokea kwa sababu hiyo kabla hazijapita siku nyingi.

Sasa nitasimulia kidogo juu ya dini ya Zuvendi, ambayo ni kuliabudu jua tu. Dini hii ya kuliabudu jua inaingia katika desturi zote za Zuvendi, nayo hupeleka mizizi yake katika kila sheria na mila ya nchi.

Toka kuzaliwa kwao mpaka kufa kwao Wazuvendi hulifuata jua kwa kila jambo. Watoto wachanga huinuliwa na kuonyeshwa jua na kuwekwa wakfu

kwa ajili yake, ambalo ni ‘’dalili ya wema, asili ya nguvu, na tumaini la milele.’’

Wazazi, huwaonyesha watoto wachanga jua na kuwaambia ya kuwa ni mungu mkarimu, nao huliabudu linapotoka na linaposhuka.

Tena, wanapokuwa wangali wadogo bado huchukuliwa na mama zao mpaka katika hekalu la jua lililo karibu.

Na huko, kwenye saa sita, miali ya jua inapoiangaza madhabahu ya dhahabu ya katikati na kuufifisha moto unaowaka huko, husikia makuhani waliovaa mavazi meupe wakiimba sifa za jua, na kuwaona watu wote wakisujudu na huku panda zinalia na kafara hutupwa katika moto ulio chini ya madhabahu.

Tena, wakiisha kua, ‘Huja hapa kutangazwa na makuhani kuwa sasa ni watu wazima, na kuwekwa wakfu kufanya matendo mema na vita; tena, ni hapa wanapowaleta mabibi arusi wao; tena ni hapa wanapowaleta kuachana nao kama hawawezi kupatana katika nyumba zao.

Basi, vivyo hivyo tokea mwanzo mpaka mwisho wa maisha yao, ndipo wanapoletwa juu ya jeneza na kuwekwa juu ya milango inayofunguliwa kuingilia chini mbele ya madhahabu ya mashariki, na miali ya mwisho ya jua linaposhuka na kuwaangazia nyusoni, makomeo huvutwa na mlango hufunguka; nao huanguka chini katika moto, ndio mwisho wao.

Makuhani wa Jua hawaoi. Huchaguliwa katika vijana waliowekwa wakfu na wazazi wao kufanya kazi hizo, nao hupewa riziki zao Serikalini.

Watu wenye daraja kubwa katika ukuhani huchaguliwa na mtawala, lakini wakisha pewa daraja, basi hawawezi kutolewa tena.

Na kwa kweli hao ndiyo wanaoitawala nchi. Makuhani ni chama kilichounganishwa imara, nao huapishwa kutii, tena huapa ya kuwa hawatatoa nje habari zozote za kazi yao, kwa hivi’.

Amri inayotolewa na kuhani mkuu huko Milosis hufuatwa mara ile bila kusita na kuhani wa mji wowote hata kama ni mbali mwendo wa maili mia

tatu au nne.

Makuhani ni mahakimu na makadhi wa nchi, nao wakiisha kukata shauri haliwezi kupelekwa mbele isipokuwa mbele ya mkuu wa sehemu ile ya nchi, na toka kwake, hupelekwa mbele, ya mtawala mwenyewe nao wanazo nguvu juu ya mambo yote ya dini.

Pamoja na nguvu za kuharamisha watu ambayo ni nguvu kubwa sana.

Msingi mwingine wa nguvu za makuhani ni elimu, maana karibu elimu zote za nchi zi katika mikono yao tu!

Nao wanazo elimu nyingi za nyota pia, na kwa hivyo wanazo nguvu juu ya watu kwasababu wanaweza kubashiri habari ya kupatwa kwa mwezi na jua. Na pia habari za nyota nyingine zenye mikia.

Wako wakuu wachache tu wanaoweza kusoma na kuandika, lakini karibu makuhani wote wanaweza, na kwa hiyo watu huwadhania kuwa ni watu wenye elimu nyingi.

Kwa jumla yake, sheria za nchi ni za haki tena zina huruma, lakini zimeachana na zile za nchi zilizostarabika kwa namna nyinginezo.

Adhabu ya kifo inatokana kwa kumwasi mtawala au kujaribu kuikimbia nchi ambayo huhesabiwa kuwa ni kumwasi mtawala kwahiyo adhabu yake huwa ni hukumu ya kifo. Na kwa kudanganya yatima na wajane hukumu yake huwa ni kifo.

Namna ya kuwaua wakosaji hao ni moja tu! Nayo ni ya kutisha sana. Mkosaji hutupwa angali hai katika moto mkali ulio chini ya madhahabu mojawapo ya jua.

Kwa makosa yote mengine, pamoja na lile la kuwa mvivu, adhabu ni kupelekwa kufanya kazi katika majengo ya Serikali ambayo siku zote yanajengwa huko na huko katika nchi, nao pia hupingwa mara kwa mara kadiri ya makosa yao waliyoyafanya.

Wenyeji wanaruhusiwa kuoa zaidi ya mke mmoja, lakini kwa kawaida huoa mke mmoja tu kwa sababu ya gharama. Kwa sheria mwanaumume lazima ampe kila mke nyumba ya peke yake.

Mke wa kwanza ni mke wa sheria, na watoto wake husemwa kuwa ni wa nyumba ya baba.

Watoto wa wake wengine huitwa watoto wa nyumba za mama zao. Lakini desturi hii si kuwatia aibu wale watoto wala mama zao. Tena, mke wa kwanza anaweza kufanya sharti anapoolewa ya kuwa mume wake hana ruhusa ya kuoa mke mwingine.

Lakini hawafanyi hivyo mara nyingi, bali ni wanawake walio na bidii katika desturi hii ya kutaka waume wao kuoa wake wengine, maana wanawake ni wengi kuliko wanaume, tena, yule mke wa kwanza huwa kama ni mkubwa wa nyumba nyingi.

Kwa kawaida Wazuvendi ni watu wapole, wachangamshi, na wakarimu. Si stadi katika kufanya biashara, wala hawafikiri sana habari za fedha, hufanya kazi tu kupata chakula cha kutosha kuwasitawisha katika hali waliyozaliwa nayo. Biashara ya kawaida ni kubadilishana vitu.

Kazi iliyo kubwa ni kulima, lakini pia hufuga ng'ombe na farasi kwa uangalifu sana. Watu hutozwa kodi kubwa sana.

Serikali hutwaa theluthi ya mshahara wa kila mtu, na makuhani kadiri ya sehemu ishirini kwa moja ya ule uliobaki.

Lakini mtu ye yote akipatikana na misiba, basi, serikali humtunza kwa kadiri ya hali yake. Lakini kama ni mvivu , hupelekwa kufanya kazi ya serikali, na wakati huo serikali huwatunza wake zake na watoto wake.

Serikali hutengeneza njia na barabara zote na kujenga nyumba zote na kuzipangisha kwa watu.

Sasa je, watu hawa wamestarabika ama sivyo? Ni vigumu kusema kwa hakika. Majengo yao na sanamu zao ni nzuri kabisa nafikiri hakuna watu duniani wanaoweza kuwashinda kwa kazi hiyo.

Lakini hawana habari za kazi za sanaa nyingine zilizo katika nchi zilizostarabika. Vyombo vyao vya kufinyanga si vizuri, wala hawana habari za nguvu za mvuke wa maji, wala za umeme, wala za baruti, wala hawajui namna ya kupiga chapa vitabu.

Juu ya habari za dini yao, kweli pengine huliita jua ‘’Vazi la Roho’’ lakini kwa kweli huliabudu jua lenyewe.

Tena huliita ‘’Tumaini la milele ,’’ lakini naona maana yake si dhahiri. Wengine wao huamini kuwa kuna hukumu inayofuata baada ya kufa najua ndivyo anavyosadiki Nyleptha lakini ni dini ya moyo wake yeye, wala si kanuni ya dini ya nchi.

SURA YA KUMI NA NNE

Nilipoamka asubuhi baada ya kufika Milosis, saa yangu ilikuwa saa mbili na nusu. Nilikuwa nimelala muda wa saa kumi na mbili, nikaona nafuu kabisa.

Kweli, usingizi ni kitu cha Baraka sana! Ni tofauti hiyo inayofanyika kwenye usingizi wa saa kumi na mbili baada ya siku nyingi za kazi ngumu na hatari ni kama kulala hujifai kabisa na ukiamka tena umekuwa mtu mpya.

Niliketi kitandani, na kitu cha kwanza nilichoona ni rodi ya Bwana Good inanitazama. Nilijua ya kuwa amekwisha amka, anangoja niamke tu apate kuongea.

Hakika, alianza kusema, lakini hapa tulisikia panzia likivutwa na mtumishi aliingia chumbani, akafanya ishara kutujulisha ya kuwa amekuja kutuongoza kwenye mahali pa kuogea.

Tukamfuata kwa furaha, tukapelekwa kwenye hamam ya marumaru yenye maji maangavu yaliyo katikati yake, tukajitumbukiza ndani mara ile.

Tulipokwisha oga tulirudi chumbani tukavaa tukaenda chumba cha katikati tulimokula jioni, tukaona chakula kimeandaliwa tayari.

Kilikuwa chakula kizuri sana, ingawa siwezi kuieleza namna yake. Baada ya kula , tulitembea huko na huko kufurahia mazulia, na sanamu zililozochorwa katika mawe, tukifikiri mambo gani tena, yatakayo fuata!!

Basi, tulipokuwa tukifanya hivyo, askari mkubwa yule aliyewekwa kutuangalia alifika, akatuamkia na kufanya ishara tumfuate, tukamfuata na huku tuna mashaka mengi moyoni, maana tulisikia ya kuwa wakati umewadia wa kufika mbele ya kuhani mkuu kutoa sababu ya kuwaua wale viboko.

Lakini hatukuwa na njia nyingine ila kumfuata, na mimi niliona faraja nyingi kwa vile wale Malkia pacha walivyotuhaidi kutuokoa, nikijua ya kuwa wanawake kwa jinsi walivyo na mapenzi ya dhati, basi hawakosi njia ya kuyatimiza mapenzi yao.

Basi, tukamfuata kama kwamba tunapenda. Baada ya kupita katika vichochoro na katika ua wa nje tukafika kwenye milango ya jumba ya kuingilia barabara kubwa inayopanda kilima katikati ya Milosis na Hekalu la jua mwendo wa maili moja, kisha inakwendea upande wa pili wa hekalu mpaka kwenye ukuta wa nje wa mji…

Milango hii ni mikubwa sana ya shaba iliyonakshiwa vizuri. Katikati ya milango hii maana iko miwili pana handaki kadiri ya futi arobaini na tano lililojaa maji, lenye daraja la kulivukia. Daraja hilo linaweza kuinuliwa na liinuliwapo, jumba huwa mfano wa kisiwa kisichofikika.

Tulipotoka milangoni mara magari manne yakaja mbio, na kila gari lilikuwa likikokotwa na farasi wawili weupe.

Magari hayo ni ya mbao yenye magurudumu mawili yaliyozungushiwa chuma. Saisi hukaa katika kiti mbele, na ndani ya gari vimo viti vitatu.

Magari hayo ni mepesi lakini ni imara sana, na farasi ni wazuri mno, si wakubwa sana, ila ni wenye nguvu nyingi. Gari la kwanza na la mwisho yalikuwa na askari ndani yake.

Lakini yale mawili mengine yaliyokuwa katikati yalikuwa hayana mtu ndani isipokuwa saisi wanaoyaendesha. Basi, tulipelekwa kwenye magari hayo, tukaingia ndani, na mara ile yakaanza kwende mbio sana.

Baadaye kidogo tukaona Hekalu la jua, zuri ajabu, ambalo linaheshimiwa sana na Wazuvendi.

Utajiri na ustadi na kazi za vizazi vingi zilitumika kulijenga jengo hilo la ajabu, nalo lilikuwa limemalizwa zamani za miaka hamsini tu.

Hakuna kitu kilichomo katika nchi kilichotakiwa kulikamilisha hekalu hilo kisicholetwa na kutumika na jengo kwa kweli lilistahili bidii yote

iliyotumika kulijenga.

Si kwa sababu ya ukubwa wake, maana yako majengo makubwa zaidi duniani, ila kwa sababu ya ukamilifu wa malingano yake, ukamilifu wa uzuri wa vitu vilivyotumika na ukamilifu wa sanaa za kazi.

Hekalu limesimama peke yake juu ya kilima, na kuzunguka ziko nyumba wanamokaa makuhani, na umbo la jengo lake ni la ua kubwa.

Sehemu ya katika ina dari ya kuba iliyofanana na jicho la ua, na katika pande zake ziko sehemu kumi na mbili zilizofanana na majani ya maua yanayotoka katika jicho lake, na kila sehemu imewekwa wakfu kwa ajili ya mwezi mmoja wapo wa mwaka, na ndani yake huwekwa sanamu za ukumbusho wa watu maarufu waliokufa.

Upana wa duara iliyo chini ya kuba ni futi mia tatu, na urefu wa kwenda juu ya kuba ni futi mia nne, na urefu wa kila sehemu inayotoka katika sehemu hiyo ya katikati ni futi mia moja na hamsini, na urefu wa dari zake ni futi mia tatu; basi ile sehemu ya katikati iliyo kama jicho la ua imeinuka juu zaidi ya sehemu nyingine.

Mawe ya majengo ni marumaru nyeupe iliyolainishwa mpaka kung'aa, nayo yaonekana vizuri sana kwa sababu mawe ya nyumba na majengo ya mji ni mekundu.

Sehemu ya nje ya kuba, na dari za sehemu za hekalu zimefunikwa kwa mabati ya dhahabu na nchani kabisa mwa kila dari iko sanamu ya dhahabu ya mtu mwenye mabawa aliyeshika panda mkononi mwake, amesimama kama kwamba yu tayari kuruka juu angani.

Madhabahu kubwa iko katikati chini ya kuba, na madhabahu nyingine ziko, moja upande wa magharibi, na moja upande wa mashariki.

Madhabahu ya katikati ni ya marumaru iliyofunikwa kwa dhahabu. Sura yake ni kama jua, na urefu wake kwenda juu ni futi nne, na uzingo wake ni futi thelathini na sita.

Katika pande zake iko namna ya milango kumi na miwili iliyopangwa kufanana na majani ya ua kuizunguka madhabahu ambayo ni kama jicho la ua.

Milango hiyo imefungwa kwa bawabu chini ya madhabahu, nayo hurudishwa na kufungwa juu ya madhabahu saa zote isipokuwa muda mfupi tu, yaani jua linapopenya katika tundu lililo katikati ya kuba.

Saa sita ya mchana, na kuangazia madhabahu katikati, basi, hapo milango hufunguka na madhabahu hufanana na ua lililochanua, na jua liishapo kupita, basi milango hufungiwa juu tena, liko neno jingine juu habari za madhabahu hiyo.

Hapa afadhali nieleze ya kuwa kila siku miali ya jua liangaziapo katikati ya madhabahu kuu, panda hupigwa, na jua hutolewa kafara iliyochomwa moto, pengine ni mzoga wa kondoo au wa ng'ombe, au pengine ni matunda au nafaka.

Madhabahu ya magharibi na ya mashariki zina sura ya nusu ya duara; zimewekwa kusimama karibu na ukuta wa hekalu.

Madhabahu hizi si nzuri kama ile ya katikati, ila hata hivyo ni za dhahabu ; na moto uliowekwa wakfu unawaka juu ya kila moja, na sanamu ya mtu mwenye mabawa imewekwa upande huu na huu wa kila madhabahu.

Nyuma ya madhabahu ya magharibi na ya mashariki ipo miali miwili ya dhahabu ukutani, na katikati yake liko dirisha jembamba refu.

Basi, jua litokapo asubuhi, miali yake ya kwanza hupenya katika dirisha lililo nyuma ya madhabahu ya mashariki na kupita mpaka katika madhabahu kuu na kuing'arisha dhahabu yake, kisha hupita na kuiangaza madhabahu ya magharibi.

Vile vile, jua lishukapo jioni, miali ya mwisho hupenya kati dirisha lililo katika ukuta nyuma ya madhabahu ya magharibi.

Na huing'arisha madhabahu ya katikati kisha hutua kwa muda kidogo juu ya madhabahu ya mashariki. Ni kama ahadi inayoweka mapambazuko kwa

jioni, na ahadi inayoweka jioni kwa mapambazuko.

Isipokuwa kwa madhabahu hizi tatu, nafasi iliyo chini ya kuba hili kubwa ni wazi kabisa, bila pambano lolote.

Basi, hili ndiyo namna lilivyo hekalu lile zuri, lakini siwezi kulieleza zaidi jinsi lilivyo la ajabu na utukufu.

Mlangoni pa hekalu, tulipokewa na kundi la skari walio onekana kuwa wapo chini ya amri ya kuhani. Tuka pelekwa katika sehemu moja ya hekalu tukaachwa humo muda wa nusu saa.

Hapa tulifanya shauri pamoja, tukatambua ya kuwa tumo katika hatari ya kupoteza maisha yetu, tukakusudia kujilinda tuwezavyo na kuyapigania vikali maisha yetu.

Umslopogaas alisema kuwa yeye atamuua yule kuhani mkuu Agon kwa kumpasulia mbali kichwa kwa Inkosikazi.

Mahali tuliposimama tuliweza kuona umati wa watu waliokuwa wakihudhuria hekaluni, kama kwamba wanatazamia jambo kuu, nikahofia ya kuwa sisi tumo katika jambo hilo.

Basi, karibu na saa sita, kuhani alikuja akafanya ishara, na mkubwa wa askari alituashiria ya kuwa tunatakiwa kwenda mbele, tukaenda mbele kwa ujasiri tulivyoweza.

Mara tulitoka katika ile sehemu ya hekalu, tukapita katikati ya umati mkubwa wa watu waliokuwa wamehudhuria, mpaka tukawa tumesimama juu ya utando wa shaba ulio katika sakafu mbele ya madhabahu kuu kwa upande wake wa mashariki.

Kwa kadiri ya futi thelathini kuizunguka madhabahu, kamba zilifungwa ili kufanya nafasi na kuwazuia watu wasiingie ndani.

Na katika nafasi hiyo makuhani wengine walipangwa mfano wa duara, wameshika panda mikononi mwao, wamevaa mavazi meupe yenye mahazamu ya dhahabu, na mbele yetu, Agon kuhani mkuu, alikuwa

amesimama amevaa kofia yake ya nakshi na urembo. Yeye pekee alikuwa amevaa kofia, bali wote wengine walikuwa vichwa wazi.

Tulisimama juu ya sehemu ile ya shaba, wala hatuna habari hata kidogo kuna nini chini yake kilichotengenezwa kwa ajili yetu.

Nilisikia sauti ikitoka chini sakafuni, lakini sikuweza kukisia ni kitu gani.

Basi, hapa kukawa kimya, nikatazama huku na huko niwaone wale Malkia wawili Nyleptha na Sorais. Nisiwaone.

Lakini niliona nafasi ipo wazi upande wa kulia, nikakisia ya kuwa nafasi ile imewekwa kwa ajili yao.

Tulingoja, na halafu tulisikia panda inalia mbali sana juu katika kuba. Kisha, tulisikia mnong'ono wa watu waliokuwapo, tukatazama tukaona Malkia wale wawili wanakuja pamoja.

Nyuma yao wakuu wengine waliandamana nikamwona Yule Nasta, na nyuma yao askari wapatao hamsini walifuata.

Nilifurahi sana nilipowaona askari wale. Basi, baada ya muda mfupi, walikuwa wamekwisha fika na kusimama mahali pao, Malkia wawili kwa mbele, na wakuu kwa upande wa kuume na wa kushoto, na askari wamejipanga katika mfano wa nusu duara nyuma yao.

Kasha, kukawa kimya kwa muda mrefu, na Nyleptha alinitazama; nikafikiri ya kuwa anajaribu kunijulisha habari, nikamwangalia sana.

Jicho lake lilitazama jicho langu, kasha likajongea, na kutazama ile sehemu ya shaba ambayo tulikuwa tumesimama juu yake, kasha, alikijongeza kichwa chake polepole upande.

Sikufahamu maana yake, akaifanya ishara ile ile tena. Ndipo nilipofahamu ya kuwa anatuonya tusisimame juu ya mlango huo wa shaba.

Akatazama tena, nikaona kuwa ndiyo maana yake hakika, yaani ya kuwa ipo hatari katika kusimama juu ya mlango huo.

Sir Henry alikuwa amesimama upande wangu mmoja na Umslopogaas upande wa pili.

Basi, niliyakaza macho sawasawa mbele yangu, lakini niling'ona kwa sauti ndogo sana kwanza kwa Kizulu, kisha kwa Kiingereza nikawaambia warudi nyuma kidogo kidogo mpaka wawe wamesimama juu ya sakafu wala si juu ya mlango wa shaba.

Basi, sote tulianza kujongea polepole kabisa polepole wala hapana mtu aliyetuona isipokuwa Nyleptha na Sorais tu.

Kisha, nilimtazama tena Nyleptha nika mwona anakiinamisha kichwa chake kidogo sana kama kwamba ananijulisha ya kuwa nimefanya alivyotaka.

Basi, huku nyuma macho ya Agon yalikuwa yamekazwa mbele kuitazama madhabahu, kama kwamba ametoa kila wazo katika akili zake isipokuwa la kazi iliyoko mbele yake! Na macho yangu yalikuwa yamekazwa kuutazama mgongo wake.

Halafu alianza kuipunga mikono yake, akaanza kuimba kwa sauti iliyosikika hekaluni mwote.

Maneno aliyoimba yalikuwa yakulisifu jua.

Yalikuwa kama haya yanayofuata:

Kuna kimya juu ya uso wa Dunia na wa maji yake, Ndiyo kimya imeukalia uso wa maji kama ndege akaaye juu ya kiota chake.

Na kimya imekali kifua cha giza nene, juu sana angani tu nyota zinasema na nyota.

Dunia anataka kuzimia kwa kutamani na machozi yake yanatoka kwa ajili ya tamaa yake.

Usiku mwenye ukanda wa nyota huikumbatia isiridhike.

Imelala imefunikwa kwa ukungu kama maiti katika sanda, Imeinyosha mikono yake kuendelea masharikini.

Tazama! Mbali masharini iko dalili ya mwangaza.

Dunia imeiona na kujiinua, Inatazama toka chini ya kitanga cha mkono wake.

Ndipo malaika wako wakuu hutoka katika mahali pako Patakatifu, ee jua.

Huzitupa panga zao zenye moto katika jua na kuliunguza.

Hupanda mbinguni na kuzitupa chini nyota toka viti vyao vya kifalme.

Ndiyo, huzirudisha nyota ziinemetazo katika giza la usiku.

Hufanya mwezi kufifia kama uso wa mtu anayekufa.

Na tazama! Utukufu wako huja, ee jua!

Ee wewe uliye mzuri, hujivika kwa moto.

Mbingu pana ni njia yako, hupita juu yake kama gari.

Dunia ni bibi arusi wako. Huikumbatia nayo huzaa watoto, ndiyo, humpendeza naye hutoa mazao yake.

Wewe ni Baba wa wote na mtoaji uzima ee jua.

Watoto wadogo huinyosha mikono yao na kukua katika mwangaza wake, Wazee nao hutokea na wakikuona hukumbuka nguvu zao.

Wafu tu, ndio wanaokusahau, ee jua.

Ukasirikapo ndipo huficha uso wako.

Hujifunika na pazia la vivuli.

Ndipo Dunia huona baridi na Mbingu hufadhaika; Hutetemeka, na sauti yake ni kama sauti ya ngurumo Hulia, na machozi yao humiminika katika mvua;

Huguna, na pepo kali ni sauti ya kuguna kwao.

Maua hufifia, mashamba yenye mauuno husinyaa na kunyauka.

Wazee na watoto huenda mahali panapo wahusu.

Uchapo mwangaza wako, ee jua!

‘’Sema, u nini, ee uzuri usio na mfano nani aliyekuweka juu sana, ee kitisho cha joto?

Ulianza lini, na siku ya mwisho wako itakuwa lini?

Wewe ni vazi la roho mwenye uhai.

Hakuna aliyekuweka juu maana wewe ndiyo mwanzo.

Huna mwisho hata watoto wako watakapo sahauliwa.

Ndiyo, huna mwisho kabisa, maana wakati wako ni wa milele.

Umekaa juu katika nyumba yako ya dhahabu na kupima wakati.

Ee Baba Wa Uzima! Ee Jua Mfukuzaji wa Giza!’’

Basi, aliacha kuimba na ingawa maneno niliyotafsiri huonekana kama si mazuri sana, lakini yale aliyoyasema yalikuwa mazuri ajabu; kisha, akatazama juu katika kipepeo cha kuba, akasema.

‘’Ee jua, ushuke juu ya madhabahu yako!’’

Aliposema maneno hayo, jambo zuri la ajabu lilitokea.

Mwali mmoja wa nuru ulipenya lile tundu katika kuba kama upanga wa moto mkali.

Ulitua juu ya milango ya dhahabu iliyofungwa juu ya madhabahu, ukatiririka juu yake, na ua lile tukufu lilifunuka kama kwamba limefunuliwa na mwangaza wake.

Lilifunuka polepole na milango ile ilipokuwa ikifunuliwa, na kuonyesha madhabahu ya dhahabu ambayo juu yake moto huwaka daima, makuhani walipiga panda zao, na watu wote walipaaza sauti zao, na sauti zao za kusifu zikapanda juu zikapiga kuba ya dari zikarudishwa tena katika kuta za marumaru.

Sasa madhabahu ya ua ilikuwa imefunuka, mwangaza wa jua ulitua juu ya ulimi wa moto mtakatifu, ukaupiga chini hata ukapepesuka na kuzama na kutoweka katika shimo ulimotokea.

Ulipokuwa ukitoweka , sauti za panda zilipaa tena, na yule kuhani mzee aliinua mikono yake juu tena, akasema kwa sauti kubwa

‘’Twakutolea kafara ee Jua!’’

Nilimtazama Nyleptha tena; nikaona ya kuwa macho yake yamekazwa kuutazama mlango ule wa shaba wa chini, mbele ya madhabahu.

Nikasema, ‘’Jihadharini!’’ na nilipokuwa nikisema, nilimwona Agon anainama mbele na kugusa kitu juu ya madhabahu.

Na alipofanya hivyo, nyuso za watu wote ziligeuka nyekundu, kisha zikageuka nyeupe tena, nikasikia sauti ya kuvuta pumzi kutoka kwa watu wote.

Nyleptha aliinama mbele, akajificha macho yake kwa mikono yake kama hawezi kujizuia.

Sorais aligeuka akamnong’oneza mkubwa wa walinzi wa kifalme, ndipo sauti ya kukwaruza ilisikika, na mlango ule wa shaba katika sakafu ulifunguka mbele ya miguu yetu, na mahali pake palikuwapo shimo lenye moto mkubwa mkali sana chini ya madhabahu.

Tulitoa sauti ya hofu, tukaruka nyuma. Mara kukawa na ghasia nyingi sana, na sisi tulijipanga mgongo kwa mgongo.

Sote tulikuwa na bastola maana ingawa tulipokuwa tukitoka jumbani, tulinyang’anywa bunduki zetu, bastola tulikuwa nazo maungoni mwetu.

Watu hawa hawakujua bastola ni kitu gani. Tena, Umslopogaas alikuwa na shoka lake la vita, na sasa alilizungusha kichwani akatoa ukulele wa vita wa Kizulu uliozunguka zunguka hekaluni.

Basi, hapa makuhani ambao walikuwa wamenyang'anywa mawindo yao walifuta panga zao toka chini ya mavazi yao meupe, wakaturukia kama mbwa mwitu wanavyowarukia wanyama wanaojitetea.

Nikatambua ya kuwa ingawa iko hatari katika kutenda jambo lolote, lakini hata hivyo, lazima tujaribu kujitetea au tupotee.

Basi, mtu wa kwanza alipotujia naye alikuwa mtu mrefu mkubwa nilimpiga risasi ikampata, akaanguka mbele ya lile shimo la moto, akatumbukia ndani ya lile shimo la moto tulilowekewa sisi, na huku anapiga kelele.

Sijui kama ilikuwa kwa sababu ya kelele alizofanya au kwa sababu ya kishindo cha bastola na matokeo yake wale makuhani wengine walisimama kama wamepooza na kufadhaika kabisa.

Na kabla hawajaweza kujongea mbele tena, Sorais alitoa amri, na mara ile sisi pamoja na Malkia wawili na watu wakuu tulizungukwa na kundi la askari wenye silaha.

Basi, hata hapo makuhani walisita, na watu wote walisimama kama wanyama walioshtushwa, wasifanye hivi wala vile.

Sauti ya mwisho ya Yule kuhani aliyeangukia motoni ilififia, kukawa kimya kabisa katika hekalu.

Ndipo kuhani mkuu Agon alipogeuka, na uso wake ulikuwa kama wa shetani! Akawapigia ukulele wale Malkia akasema, ‘’Kafara itolewe.

Kufuru iliyotendeka na wageni hawa haitoshi na ninyi Malkia mtaingia nyinyi kama mnataka kuwaokoa watu hawa walio tenda uovu ule wa kuwaua wanyama wale waliowekwa wakfu.

Na sasa kuhani wa Jua pia amekufa, wamemuuawa kwa uchawi wao. Wageni hawa waliofika kama pepo za mbinguni toka wapi hatujui, wala

hatuwajui ni nani!

Jihadharini ninyi Malkia namna mnavyojiingiza na kushughulika na utukufu wa mungu, hata mbele ya madhabahu yake.

Iko nguvu iliyo kuu kuliko nguvu zenu; iko haki iliyo juu kuliko haki yenu. Jihadharini wala msiinue mikono ya kufuru kuzipinga. Enyi Malkia, kafara itolewe.''

Ndipo Sorais alijibu, na sauti yake ilikuwa ya utulivu, na kama ilivyokuwa siku zote kama kwamba anadhihaki: ''Ee Agon umesema kama ulivyotaka, nawe umesema kweli. Lakini ni wewe unayetaka kuinua mkono wa kufuru juu ya haki ya Mungu.

Kafara ya saa sita imekwisha timizwa! Jua limechagua kuhani wake awe kafara.''

Basi, wazo hili lilikuwa la kigeni, na watu wote wakalikubali.

Sorais akaendelea: ''Watu hawa ni nani? Ni wageni walioonekana wanaelea juu ya ziwa. Nani amewaleta hapa? Walifika hapa namna gani? Unajuaje ya kuwa si watumishi wa Jua?

Je, huu ndio ukarimu unaotaka taifa letu liwape watu ambao bahati imewaleta kwetu, Je, ni vyema kuwatupa motoni? Ole wako! Ole wako! Ukarimu ni nini? Kumpokea mgeni na kumkaribisha vizuri! Kuyaganga majeraha yake, kumpa mahali pa kulala, na chakula.

Lakini malazi yako ni shimo la moto, na chakula chako ni joto la moto. Ole wako, nasema!''

Hapa alinyamaza kidogo ili aone namna watu wanavyoyapokea maneno yake, na alipoona wanayapokea vizuri, akabadili usemi wake, na sasa ulikuwa wa kutoa amri.

''Haya! Jitengeni; wapisheni Malkia na wale wanao funikwa na mavazi ya Malkia.''

Agon akayakaza meno yake, akasema: ''Je, ee Malkia nikikataa?''

Sorais akajibu kwa kiburi: ‘’Basi hapo nitakata njia kwa walinzi wangu, ndiyo, hata mbele ya madhabahu takatifu na katikati ya miili ya makuhani wako.’’

Agon akafura kwa gadhabu ya kushindwa. Akawatazama watu kama kwamba anawasii wamsaidie, lakini aliona ya kuwa wako upande wa Malkia.

Wazuvendi ni watu wenye udadisi, tena wakarimu, ingawa walifikiri ya kuwa kuwapiga wale viboko waliowekwa wakfu ni kosa kubwa, lakini hawakutaka wageni wa kwanza walioonekana katika nchi yao watupwe katika shimo la moto, na kwa hivyo kukomesha nafasi ya kupata habari zetu kwa kuzungumza juu yetu.

Agon alipoona hivyo akasita, kisha, Nyleptha alisema kwa sauti yake nzuri, akasema: ‘’Kumbuka Agon, kama dada yangu Malkia alivyosema, labda, watu hawa pia ni watumishi wa Jua.

Wao hawawezi kujitetea maana ndimi zao zimefungwa. Mambo haya yawekwe mpaka watakapojifunza lugha yetu.

Nani anayeweza kuhukumiwa bila kusikilizwa? Watu hawa watakapoweza kujitetea, basi hapo tutaweza kuwahukumu.’’

Basi, hii ilikuwa njia ya akili ya kuokoka ingawa yule mzee mkali kuhani hakuipenda, hana njia nyingine, akasema: ‘’Vyema, Ee Malkia.

Watu na waende kwa amani, nao watakapo weza kusema lugha yetu watapata nafasi ya kujitetea. Na mimi, hata mimi, nitaomba mbele ya madhabahu maradhi yasiingie katika nchi yetu kwa ajili ya kufuru iliyotendeka.’’

Basi maneno yake yalikubaliwa na wote, tukatoka hekaluni tumezungukwa na askari wa kifalme.

Lakini hatukupata kujua kwa siku nyingi habari za mambo yaliyotokea siku ile, na jinsi maisha yetu yalivyookolewa kwa shida nyingi kwa mikono ya

ukatili ya makuhani wa Zuvendi, ambao wana nguvu hata karibu kuzishinda nguvu za Malkia.

Kama Malkia hawakufanya bidii kutulinda, tungaliuawa hata kabla hatujaingi katika hekalu la Jua.

Ile hila ya kututumbukiza katika shimo la moto tuwe kafara, ilibuniwa baada ya kujaribu kutuangamiza kwa njia nyingi nyingine ambayo sisi hatukuwa na habari nazo.

SURA YA KUMI NA TANO

Tulipokwisha okolewa katika mikono ya Agon na watu wake wa dini, tulirudi katika vyumba vyetu katika jumba la Malkia tukawa katika hali njema, Malkia wawili, watu wakuu na watu wenyewe walishindana wao kwa wao kutupa heshima na zawadi, jambo lile la kuwaua viboko lilisahauliwa, wala hatukutaka kuwakumbusha watu habari zake.

Asubuhi iliyofuata mambo yale yaliotokea hekaluni, walimu watatu wenye vitabu vya maandiko ya mkono na wino na kalamu wakaja wakatuashiria kuwa wameletwa kutufundisha.

Basi, tulijitahidi sana kujifunza kila siku muda wa saa nne. isipokuwa Umslopogaas, Umslopogaas alikataa kabisa, akasema kuwa yeye hataki kujifunza lugha ya kike.

Na mwalimu mmoja alipomwendea na kitabu na wino na kuvipunga mbele yake, ili kumvuta macho, aliondoka kwa ukali akapunga Inkosikazi mbele ya macho ya yule mwalimu, na huu ulikuwa mwisho wa kujaribu kumshawishi kumfundisha lugha ya Kizuvendi.

Kila sehemu watu walikuja kutuamkia na kutazama bunduki na nguo zetu na vyombo vyetu, na hasa saa zetu zilizowafurahisha sana. Watu wengine, hasa vijana maridadi waliyaiga mavazi yetu.

Basi baada ya haya, tulianza kuvaa mavazi ya kienyeji kwa sababu hatukutaka, Kuendelea kuwavuta watu kututazama.

Tena na pia nguo zetu zilianza kuchakaa. Umslopogaas tu hakukubali kubadili namna ya mavazi yake. Tena tulijitahadi katika kujifunza lugha ya nchi, tukaendelea vizuri.

Basi, hivyo kila asubuhi tulitumia wakati wetu katika kujifunza na baada ya saa sita tulitumia wakati kujiburudisha.

Pengine tulikwenda kutazama mashimo ya kuchimbua dhahabu na marumaru, na pengine tulikwenda mwituni kuwinda pamoja na mbwa waliofugwa na walio fundishwa kwa ajili hiyo.

Siku nyingine tulikwenda kuwaamkia mabwana wakuu katika ngome zao, tukaiona miji ya wenyeji. Jioni tulikwenda kula pamoja na Malkia, si kila siku ila labda mara tatu nne kila jioni na, walipokuwa hawana wageni wengi, wala shughuli iliyohusu utawala.

Nadhani tabia ya kupendeza ya Nyleptha ilikuwa upole na kwa sababu alipenda kujua habari za mambo madogo madogo ya mtu mzuri kupita wote nishajua lakini hata hivi, kwa kweli nimwanamke anayependa kujifunza mambo mapya.

‘’Basi, vivyo hivyo miezi mitatu mingine ilipita sasa tulikuwa tumekwisha jua lugha ya Kizuvendi kwa kadiri, maana si lugha ngumu.

Na huku nyuma tulikuwa tunapendwa na watu wote na pia watu wa jumbani mwa Malkia walitupenda kirafiki, tukapata sifa ya kuwa watu wenye ustadi na busara.

Sir Henry aliweza kuwaonyesha namna ya kutengeneza kioo, na kwa msaada wa kitabu tulichokuwa nacho chenye habari za jua na mwezi na nyota, tuliweza kupata habari za namna nyota zitakavyo pangwa siku fulani habari hizi ziliwashinda wanajimu wao.

Tena tuliita mkutano wa watu wenye elimu tukawaonyesha namna, nguvu iliyomo katika mvuke wa maji inavyofanya kazi, na namna mashine za mvuke zinavyotengenezwa, watu hao wenye elimu walishangaa ushangao mkuu! Tukatengeneza vinu vingine vya namna ile ile.

Basi, kwa sababu ya mambo hayo wenyeji walikusudia tusiruhusiwe kabisa kutoka katika nchi yao, tutakaa ya kuwa hata kama tukitaka kutoka, hatutaweza.

Tena, tulipewa heshima, tukapewa vyeo katika askari walinzi wa Malkia, tukapata vyumba maalum katika jumba la Malkia, tukapewa nafasi ya kutoa ushauri katika mambo ya utawala wa nchi.

Lakini ingawa anga ilionekana kuwa na rangi ya samawati, lakini kulikuwa na wingu kubwa kwenye upeo wa macho yetu.

Kweli, tulikuwa hatukusikia habari za viboko wale tena, lakini tulijua kuwa habari za kufuru yetu hazikusahauliwa, wala hasira na uadui ulioongozwa na kuhani mkuu Agon haujatulia bado.

Na kwa kweli ulikuwa unawaka kwa ukali zaidi kwa kuzidishwa na wivu. Maana tangu hapo makuhani walifikiriwa kuwa watu wenye elimu kubwa katika nchi.

Lakini watu walipoyaona maarifa yetu, nguvu zao zilielekea kuvunjika. Tena, hatari nyingine ilikwepo maana wakuu wengine wakiongozwa na Nasta walituonea wivu sana, na uadui wao ulielekea kububujika kabisa.

Nasta alikuwa ametumaini kwa muda wa miaka mingi kumwoa Nyleptha, lakini sasa mambo yamebadilika.

Nyleptha moyo wake haukwepo tena kwake! Na Nasta alikuwa mwepesi kutambua sababu yake ni nini.

Basi, katika hasira yake alimgeukia Sorais, akaona kuwa ni bora zaidi kuposa mlima kuliko Sorais! Kwakweli Sorais alikuwa mzuri sana na pia ni jasiri lakini uliochangajika na uovu.

Basi, Nasta aliwakumbuka watu wake elfu thelathini wenye panga walio tayari kufuata amri zake kutoka chini yake milimani na kuushambulia mji wa Milosis.

Lakini kwanza alikusudia kujaribu tena kumposa Nyleptha! Akafanya shauri la kumposa mbele ya baraza ya mwaka inayofanywa ili Malkia watie sahihi sheria zote zilizoamriwa nao, katika muda wa mwaka ule.

Basi, Nyleptha akapata habari, akatuambia usiku kabla ya siku ile ya kutia sahihi, na ingawa alifanya kama si kitu, nilitambua ya kuwa anaona hofu.

Sir Henry alijiuma midomo na kujaribu awezavyo lakini hakuweza kuficha fadhaa aliyoisikia. Nikamuuliza Nyleptha kama kwa udadisi, ‘’ Malkia

atamjibu nini bwana Nasta?’’

Malkia akajikunia mabega. Akasema, ‘’Nitamjibuje Makumazahn? (maana tulijulikana kwa majina yetu ya kienyeji).

Sijui Mwanamke dhaifu anaweza kufanya nini na hali anajua kuwa yule atakaye kumposa anao watu elfu thelathini wenye panga kuhimiza posa yake?’’ Akamchungulia Sir Henry katika kope zake ndefu.

Basi, hapo tuliondoka mezani kwenda katika chumba kingine, Sir Henry akanijia, akasema ‘’Njoo upesi Quatermain, nataka shauri lako. Sikiliza, Ingawa sijasema neno, hukosi umeona kuwa nampenda sana Nyleptha. Je, nifanye nini?’’

Kwa bahati nilikuwa nimekwisha yafikiri mambo hayo, nikaweza kumjibu upesi, nikasema, ‘’Lazima useme na Nyleptha usiku huu huu. Wakati wako ni sasa, ama sivyo, hutapata nafasi tena.

Sikiliza, Tuendapo katika chumba kile cha maongezi, umkaribie umnong’oneze umwambie akukute saa sita usiku karibu na sanamu ya Rademas mwisho wa sebule kuu. Mimi nitakuwapo kushika zamu, basi, wasaa ni sasa ama haupatikani tena.’’

Basi, tulikwenda katika chumba kingine. Nyleptha alikuwa amekaa ameiweka mikono yake mbele yake, na uso wake ulikuwa wa kuhuzunisha sana. Mbali kidogo Sorais alikaa anazungumza na Bwana Good kwa sauti yake ya pole pole.

Sasa wakati ulikuwa ukipita, nikajua ya kuwa baada ya dakika kumi na tano Malkia wataondoka kama ilivyo desturi yao, na Sir Henry bado hajapata nafasi ya kusema na Nyleptha kwa faragha, maana ingawa tulionana na Malkia mara nyingi, ilikuwa shida kuweza kusema na mmoja wao peke yake.

Nilifikiri sana kisha nikapata akili nikamwendea Sorais, nilijiinamisha mbele yake, nikasema, ‘’Tafadhali, Malkia, utuimbie watumishi wako.

Mioyo yetu ni mizito leo, utuimbie ewe bibi wa usiku.'' (Ndilo jina wanalomwita wenyeji.) akajibu, ''Nyimbo zangu hazielekei kuuondoa uzito wa mioyo yenu Makumazahn. Lakini ukitaka nitaimba.

Akaondoka akaenda mezani akaichukua gambusi akaanza kuipiga kivivuvivu. Ndipo alipoanza kuimba, na sauti yake ilikuwa nzuri kama sauti ya ndege, lakini wimbo ulikuwa wa kuhuzunisha kabisa, na kiitikio chake pia kilikuwa cha huzuni sana.

Sauti yake ilipanda juu ikawa kama inayeyuka kwa mbali sana. Kisha, ilizidi tena, ikasafiri kama imejaa huzuni yote ya ulimwengu na taabu zote za wote waliopotea.

Ulikuwa wimbo wa ajabu mno, lakini sikupata nafasi nyingi ya kuusikiliza vizuri. Walakini baadaye niliyaandika maneno yake, nikajaribu kuyatafsiri. Kadiri nilivyoweza kuyatafsiri, ni kama haya yanayofuata:

Wimbo wa Sorais

Kama ndege mwenda pweke aliyepotea anavyoruka gizani.

Kama mkono ulioinuka buree kuikinga mauti wakati wa kufa.

Ndivyo yalivyo maisha! Maisha yanayotia upendo na pumzi wimboni.

Kama wimbo wa ndege uliojaa utamu usiotamkikana.

Kama roho inayofungulia milango mbinguni kwa ishara.

Ndivyo ulivyo upendo! Upendo utakaoanguka ukiisha vunjika..

Kama vishindo vya hatua za mashujaa wanaokwenda vitani.

Kama sauti ya ngurumo za umeme unapopasua mawinguni,

Ndivyo ulivyo uwezo! Uwezo utakaoanguka mavumbini mwishoni.

Maisha ni mafupi: hata hivyo vitu vyote vyaweza kutuacha.

Ni ndoto chungu usingizini wala hakuna awezaye kutuamsha,

Mpaka hatua za mauti! Mauti asubuhi au jioni zatupata.

Kiitikio.

Ndiyo, dunia ni nzuri asubuhi asubuhi asubuhi.

Lakini jua jekundu huzama damuni jua jekundu huzama damuni.

Basi Sorais alipoanza kuimba ubeti wa pili wa wimbo wake, niligeuka, nikamwambia Sir Henry kwa sauti ‘’Haya sasa nenda,’’ nilimwambia.

Niliweza kusikia kila neno alilolisema, maana moyo wangu ulifadhaika sana na kwa hiyo nilikuwa na mang’amung’amu. Akasema, ‘’Nyleptha! Nyleptha, naomba nisema nawe usiku huu huu, nakuomba usikatae.’’

Akajibu, ‘’Nawezaje kusema nawe? Malkia si kama watu wengine, nimezungukwa na walinzi na kuangaliwa kila ni endapo.’’

Sir Henry akasema, ‘’Sikiliza Nyleptha. Nitakuwapo mbele ya sanamu ya Rademas karibu na sebule kuu saa sita usiku. Makumahn na Umslopogaas watakuwapo ili kutulinda. Usikatae eh Malkia wangu.’’

Akajibu, ‘’Haiwezekani, ikawa kesho?’’ Sir Henry akamsii, ‘’ Tafadhali nakuomba iwe leo Malkia wangu!’’

Basi, hapo itikio la wimbo lilianza kuishia, na Sorais aligeuka pole pole.

Hapo Nyleptha akasema kwa haraka; ‘’Vyema, nitakuwapo, nawe usikose kuwapo pia.’’

SURA YA KUMI NA SITA

Ulikuwa usiku mkubwa. Mji wa Milosis ulikuwa kimya kabisa, Sir Henry, Umslopogaas, na mimi tulifuatana pole pole kama watenda uovu, tulipita katika vichochoro kuelekea sebule kuu.

Njiani tulikutana na askari wa zamu, lakini nilitoa neno la zamu ili tupate kupita na yule askari aliukita chini mkuki wake akatupisha. Tena, kwa kuwa tu wakuu walinzi wa Malkia, tulikuwa na haki kupita bila kuzuiwa.

Tulifika sebuleni salama. Mahali palikuwa kimya sana, na tulipokuwa tumekwisha pita, vishindo vya hatua zetu vilirudishwa na kufanya mwangwi juu ya dari iliyonakshiwa, kama vipigo vya hatua za watu waliokwisha kufa na sasa wamerudi kupatazama mahali walipokanyaga zamani.

Mahali hapo palinitisha sana. Mwezi ulikuwa mpevu, ukatupa miali mikubwa ya mwangaza katika madirisha membamba katika kuta ikalala juu ya weusi wa sakafu kama maua meupe.

Mmojawapo wa miali hiyo ya fedha uliiangaza sanamu la Rademas na yule mwanamke mzuri aliyemwinamia ukafanya duara ya nuru kuizunguka.

Basi hapo karibu ya sanamu tulisimama, tukangoja. Sir Henry na mimi karibu karibu na Umslopogaas hatua chache katika giza hata tuliweza kuliona umbo lake refu kwa shida, ameliegemea shoka lake.

Tulingoja sana hadi nikataka kusinzia nikiegemea ukuta wa marumaru japokuwa ulikuwa baridi sikuona shida kwa jinsi nilivyo choka, lakini mara niliamshwa kumsikia Sir Henry akivuta pumzi.

Ndipo kwa mbali sauti ndogo ilitokea kanakwamba sanamu zilizosimama ukutani zinanong’onezana habari za miaka mingi iliyopita.

Sauti ilikuwa kama sauti ya kuchakura ya mavazi ya mwanamke, Ilikaribia! Ikazidi kukaribia zaidi. Tukaona mtu anajongea taratibu toka kivuli mpaka

kivuli, tukasikia vishindo vidogo vya viatu vyake.

Mara nilimwona mzee Umslopogaas akiuinua mkono wake kuamkia bila kufanya kelele, na Nyleptha akasimama mbele yetu.

Akanong'ona, ‘’Nimekuja lakini ilikuwa hatari sana. Hamjui jinsi ninavyoangaliwa! Makuhani huniangalia, Sorais huniangalia kwa macho yake makubwa. Hata walinzi wangu nao pia hunivizia ! Nasta naye hunivizia.’’

Akaupiga mguu wake chini kwa hasira. Na ajihadhari! Mimi ni mwanamke mgumu, na kwa hiyo sishawishiki ki rahisi.

Tena, ni Malkia , nami naweza kujilipiza kisasi. Na ajihadhari nisije nikamkata kichwa badala ya kumpa mkono wangu.’’

Akalia kidogo, kisha akacheka akatutazama.

‘’Uliniita Bwana wangu Inkubu. Bila shaka unalo shauri juu ya ufalme wangu unalotaka kuniambia, maana najua ya kuwa siku zote unafikiri juu ya ustawi wangu na watu wangu. Nami nimekuja ingawa naogopa giza.’’

Basi, hapo nilitaka kujijongeza kidogo nisiyasikie maneno yao. Lakini alifanya ishara nisiondoke, akasema kuwa anaogopa watu watawatokea ghafula.

Basi, nilisimama, na haya ndiyo nilivyoyasikia katika maneno yao. Sir Henry akasema, ‘’Wewe unajua Nyleptha ya kuwa sikutaka uje mahali hapa pa faragha kwa habari za ufalme wala za watu wako. Nyleptha usipoteze wakati bure, unisikilize, maana nakupenda.’’

Aliposema maneno hayo, niliuona, uso wa Nyleptha umebadilika. Ubishi ulimtoka, na badala yake uso wake ulijaa nuru ya mapenzi yaliyofanana na ule uso wa sanamu ile ya marumaru ya yule mwanamke mzuri iliyokuwa imesimama karibu.

Akasema, ‘’Wasema kuwa wanipenda, na sauti yako inaonyesha ukweli wa maneno yako, lakini nitajuaje ya kuwa unasema kweli? Au nitajuaje kuwa

unanipenda? Nitajuaje ya kuwa hutanichoka wala hutaniacha uende katika nchi ile uliyotoka na kuniacha mpweke?

Nani anayeweza kuniambia kama huko kuna mwanamke mwingine unayempenda, mwanamke mwingine mzuri nisiyemjua mimi, ambaye anakaa mahali pengine anakusubiri, na hata sasa hivi anavuta pumzi chini ya mwezi huu unaoniangazia usiku huu? Niambie nitajuaje?''

Akainyosha mikono yake akamtazama kama mtu anayesihi. Sir Henry akasema, ‘’Nyleptha, nimekuambia nakupenda! Nawezaje kukuambia zaidi jinsi ninavyokupenda? Je, kiko kipimo cha kupimia mapenzi!? lakini hata hivyo nitajaribu.

Sisemi ya kuwa sijatazama mwanamke mwingine kwa mapenzi, lakini nitasema kuwa nakupenda kwa dhati kabisa tena kwa maisha yangu yote na kwa nguvu zangu zote, nitakupenda!

Sauti yako ni wimbo masikioni mwangu, na mguso wako ni kama maji katika nchi iliyokauka nikuonapo dunia huwa nzuri, lakini nisipokuona ni kama kwamba nuru imekufa.

‘’Mpenzi Nyleptha sitakuacha hapa kamwe! Na sasa kwa ajili yako nitasahau watu wangu na nyumba ya baba yangu, ndiyo, nitawasahau wote. Nitakaa pamoja nawe, Nyleptha, na pamoja nawe nitakufa.''

Nyleptha alikiinua kichwa chake polepole, akamkazia macho yake ya ajabu yanayong’aa kwa wingi wa mapenzi yake. Kama kwamba anajaribu kuisoma roho yake. Ndipo aliposema kwa sauti ndogo lakini ilikuwa kama mlio wa kengele ya fedha.

‘’Kweli mimi nimekuwa mwanamke dhaifu, lakini na sina budi nisikuamini. Na sasa nisikilize ee mwanaume uliyefika hapa toka mbali kuuiba moyo wangu na kunifanya niwe mateka wako.

Nauweka mkono wangu juu ya mkono wako hivi, na mimi, ambaye sijambusu mtu yeyote mpaka sasa, nakubusu pajini na sasa kwa mkono huu wangu na lile busu takatifu la kwanza, na kwa ustawi wa watu wangu, na

kwa kiti changu cha kifalme, na kwa jina la ukoo wangu, na kwa mwamba mtakatifu, na kwa utukufu wa milele wa jua.

Naapa ya kuwa nitaishi kwa ajili yako na kufa kwa ajili yako.

Naapa ya kuwa nitakupenda wewe! Wewe tu pekee yako mpaka kifo, ndiyo, na baada ya kufa, yaani ikiwa upo uhai baada ya kufa na mapenzi yako yatakuwa mapenzi yangu, na njia zako ni njia zangu.

‘’Tazama bwana wangu! Hujui jinsi mwenye upendo alivyo mnyenyekevu, mimi ambaye ni Malkia, napiga magoti mbele yako, hata miguuni pako kukuheshimu,’’ basi hapo yule mwanamke mzuri akajitupa miguuni sakafuni mbele yake.

Baada ya hayo sijui yaliyotokea, maana sikuweza kuvumilia zaidi nikajijongeza mbali kidogo pale aliposimama Umslopogaas, nikawaacha wayatengeneze mashauri yao, nao walichukua wakati mwingi.

Nilimkuta yule mzee Umslopogaas ameegemea Inkosikazi kama ilivyokuwa desturi yake, anatazama kwa kicheko mambo yanayotokea.

Akasema, ‘’Ee Makumazahn, naona labda ni kwa sababu ninaanza kuwa mzee, lakini nadhani sitasahau kabisa mambo ya ninyi watu weupe. Tazama wale nakusihi, ni jozi la hua wazuri mno, lakini matata ya nini?

Mume anamtaka mke, na mke anamtaka mume, basi kwa nini halipi ng’ombe kama mwamume na kumaliza shauri? Ingemaliza matata mengi, na sisi tungepata usingizi wetu.

Lakini maneno, maneno, maneno na kubusiana busiana tu! Kama watu wenye wazimu. Upuuzi kabisa.’’

Basi baada ya kupita kadiri ya saa moja kasoro robo ‘’jozi la hua’’ wale ilitujia, Sir Henry alikuwa kama aonaye haya, na Nyleptha ametulia kabisa, akasema kuwa mbalamwezi inaing’arisha marumaru vizuri sana.

Kisha akaushika mkono wangu akasema kuwa mimi ni rafiki mpenzi wa bwana wake na kwa hivyo ni rafiki mpenzi wake.

Kisha, akalishika shoka la Umslopogaas akalitazama sana, akasema ya kuwa labda itampasa alitumie kumlinda yeye hivi karibuni. Kisha, akakiinamisha kichwa chake, akamtazama mpenzi wake tena, akatoweka katika giza kama ndoto nzuri.

Asubuhi yake Bwana Good aliambiwa habari zilizotokea usiku, akafurahi sana. Hakufurahi kwa sababu ya mambo yalivyompita ila ni kwa sababu ya shauri lake mwenyewe.

Yeye naye anampenda Sorais kama Sir Henry anavyompenda Nyleptha, na shauri lake halijastawi vizuri bado. Kwa kweli ilionekana kwamba Sorais pia anampenda Sir Henry kuliko anavyompenda Bwana Good.

Basi, Bwana Good alifurahi kwa sababu mshindani wake amekwishapatikana na mwingine.

Lakini hakufurahi alipoambiwa kuwa mambo hayo ni ya siri na hasa Soras asizijue habari hizo, maana habari kama hizo zikitangazwa sasa pengine mambo ya ufalme yatavurugika.

Na labda Nyleptha atatolewa katika kiti chake cha kifalme katika ghasia. Asubuhi ile tulihudhuria tena katika sebule kubwa, nikataka kucheka nilipofikiri juu ya mambo yaliotokea hapo usiku.

Walikuwapo watu wengi sana, maana pamoja na shauri la kutia sahihi sheria za mwaka, watu walikuwa wamepata habari kuwa Nasta atamposa Nyleptha mbele ya watu wote, kwa hivyo sebule ilijaa kabisa.

Makuhani wengi walikuwamo na Agon aliwasimamia, alitutazama kwa macho yake ya chuki. Tena, mabwana wakuu wengi walikuwamo na kila mmoja alikuwa amefuatana na wafuasi wake waliovalia mavazi mazuri.

Nasta naye alikuwamo anazipapasa ndevu zake nyeusi, na uso wake ulikuwa umekunjamana kuliko kawaida.

Ilikuwa shani kubwa kuwaona wote. Na hapo mkuu mmoja aliposoma kila sheria na alipomaliza kuzisoma akaweka hati mbele ya Malkia wazitie

sahihi na huku panda zinalia. Na askari walinzi walipiga chini mikuki yao kwa kishindo.

Kazi ya kusoma na kutia sahihi sheria zote ilichukua wakati mwingi lakini hatimaye sheria moja ya mwisho ilisomwa.

‘’Kwa kuwa wageni mashuhuri wengine na kadhalika ikatupa kila mmoja cheo cha heshima pamoja na amri katika majeshi na sehemu kubwa ya nchi.

Zawadi ya Malkia Iliposomwa, panda zililia na mikuki ilipigwa chini kwa kishindo kama desturi, lakini niliona kuwa wakuu wengine waligeuka waka nong’onezana na Nasta aliyeyasaga meno yake kwa hasira.

Hawakupendezwa na heshima tuyopewa, na kwa hakika kadiri mambo yalivyokuwa. Walikuwa na haki ya kutopendezwa.

Basi, hapa kukawa kimya kidogo, kisha Nasta alisimama mbele akajiinamisha kwa unyenyekevu, ingawa macho yake hayakuwa ya unyenyekevu, akaomba fadhili kwa mkono wa Malkia Nyleptha.

Nyleptha aligeuka rangi kidogo, lakini aliinama kwa madaha, akamwambia aeleze haja yake, ndipo aliposema maneno ya posa kwa usemi thabiti kama inavyompasa askari.

Kabla Nyleptha hajapata nafasi kujibu, kuhani mkuu Agon akaanza kutoa hotuba nzuri sana tena kwa ufasaha kabisa! Akaeleza jinsi kuoana kwa watu wawili hawa kutakavyousaidia ufalme na kuziunganisha sehemu zote za nchi pamoja.

Alieleza ya kuwa shauri hili litamweka Malkia imara katika kiti chake cha kifalme, na yakuwa ndoa hii itapata Baraka za jua, yaani za makuhani na kadhalika.

Maneno mengi aliyosema yalikuwa ya haki na ya maana kabisa, yaani kwa upande wa ufalme na serikali, lakini si rahisi kuugeuza moyo wa mwanamke aliyezama mapenzini.

Alipokwisha toa hotuba, Nyleptha alijifanya tayari kujibu, lakini kabla hajawahi, Sorais aliinama mbele akamwambia kwa sauti ndogo, lakini niliweza kuisikia, akasema, ‘’Fikiri sana dada yangu kabla hujajibu, maana naona ya kuwa utawala wetu unayategemea majibu yako.’’

Nyleptha hakumjibu neno, na Sorais alikaa anasikiliza tu. Ndipo Nyleptha alipojibu, akasema, ‘’Kweli nimefanyiwa heshima kubwa sana, ya kuwa mkono wangu dhaifu hautakiwi katika ndoa tu, ila Agon pia anafanya haraka kuipa ndoa Baraka za jua.

Nadhani angaliendelea dakika moja tu zaidi, angalinioza papo hapo kabla bibi harusi hajapata nafasi au kukubali ama kukataa.

Nasta, nakushukuru sana, nami nitayafikiri maneno yako, lakini kwa sasa hivi sina nia ya kuolewa. Nakushukuru tena Nasta.’’ Akafanya kama anayetaka kuondoka.

Uso wa Nasta uligeuka ukawa mweusi kama mtu aliye kufa kwa hasira! Maana alibaini ya kuwa maneno ya Malkia ni maneno ya kumkataa kabisa.

Akajitutumua kwa shida, kisha akasema ‘’Asante sana ee Malkia kwa maneno yako ya ufadhili, moyo wangu utayaweka kama kwamba ni hazina.

Na sasa naomba neno jingine, yaani unipe ruhusa kwenda katika miji yangu ya kaskazini nikangoje huko mpaka utakapokuwa na jibu la kunipa, na labda Malkia atapendezwa kufika huko kuja kunitazama na kuleta pamoja naye mabwana hawa wageni.

Ni nchi maskini tu, lakini watu wangu wana nguvu nyingi kwa kuzoea kupanda milima, naye akifika watakuwapo watu elfu thelathini wenye panga kumshangilia.’’

Aliyasema maneno hayo kwa sauti ya dharau, ikawa kama anamwarifu Malkia kuwa amekusudia kujitenga naye na kuasi.

Lakini Nyleptha aliyasikiliza, akatoa jibu thabiti, akasema: ‘’Hakika, Nasta, nitakuja na kuwaleta wageni hawa pamoja nami, na kwa kila mmoja wa watu wa milima yako anayekuita mkuu, mimi nitaleta wawili toka

uwandani wanaoniita Malkia, nasi tutaona watu gani ni wenye nguvu zaidi. Kwa heri mpaka siku hiyo.’’

Basi, panda zililia, na Malkia wale wawili wakaondoka na mkutano ukafumuka kwa ghasia na mivumo ya sauti.

Mimi, nilirudi chumbani, na moyo wangu ulikuwa mzito maana niliweza kubashiri vita vya kindanindani.

Baada ya hayo mambo yalitulia kwa muda wa majuma machache.

Sir Henry na Malkia hawakuonana mara nyingi, wakazificha sana habari za uchumba wao; lakini hata hivyo penzi la kweli huwa si rahisi kufichika. Minong’ono ilianza kusikika! Wala ilikotokea hatukujua.

SURA YA KUMI NA SABA

Basi sasa udhia ule ambao mpaka sasa ulikuwa kama wingu dogo tu! Ulianza kudhihirika kabisa, ndiyo pengo alilo nalo Sorais kwa Sir Henry.

Nyleptha alikuwa mwenye tabia ya wivu sana, alikua anaudhika mno kila mara Sorais alipomfanyia Sir Henry fadhili, lakini hata hivyo hakukubali Sir Henry amwambie Sorais ya kuwa anataka kumwoa dada yake.

Angalimruhusu labda mambo yangalitokea vingine. Tena, Sir Henry alijua kuwa Bwana Good anampenda Sorais, na kwa kweli alikuwa ameanza kudhoofu kwa ajili ya kumpenda.

Mambo yaliendelea hivyo, ikawa jinsi Sir Henry anavyojaribu kumwepuka Sorais, ndivyo Sorais, alivyozidi kumfuata nakumwonyesha jinsi gani anavyo mpenda, mpaka mambo yakawa mabaya sana.

Ilikuwa kama kwamba Sorais hana habari ya kuwa Sir Henry anampenda Nyleptha, nikaihofia sana siku atakayoamka na kuyatambua hayo.

Maana Sorais ni mwanamke mwenye tabia ya ukatili sana. Basi, wakati niliouhofia ukawadia kama nilivyojua kuwa lazima utafika.

Siku moja Bwana Good alikuwa anakwenda kuwinda, na Sir Henry na mimi tulikuwa tunazungumza, mara tarishi wa jumbani alileta barua kumwambia Sir Henry afuatane naye mpaka chumbani kwa Malkia Sorais.

Sir Henry aliguna, akasema, ‘’Je, wewe huwezi kwenda mahali pangu?’’ Nikamjibu, ‘’La, mimi siendi, afadhali kumkabili tembo aliyejeruhiwa kwa bunduki ya marisaa kuliko kumkabili Sorais.

Mimi simo! Kama wewe ni mzuri hata kuwafanya wanawake wakupapatikie, basi matokeo yake ni juu yako mwenyewe.’’

Mimi sikubali kuwa mahali pako hata kama utanipa ufalme.’’

Basi, aliondoka akamfuata Yule tarishi, na mimi nilibaki nikimngojea.

Baada ya kupita muda wa dakika arobaini na tano, alirudi amefadhaika sana. Nikamuuliza habari za huko, akasema na sauti yake ilipwaya , ‘’Habari ni mbaya! Kweli matata yapo karibu sasa.

Nilipomfuata yule tarishi, alinichukua mpaka chumbani kwa Sorais, nika mkuta peke yake ameketi kitandani anapiga gambusi.

Nilisimama mbele yake, na kwa muda kidogo hakuniangalia ila aliendelea kupiga gambusi na kuimba tu, kisha alinitazama na kucheka. Akasema, umekuja.

Nilifikiri labda umeenda kushughulika na mambo ya dada yangu Nyleptha. Maana siku zote unashughulika naye, nami naona bila shaka kuwa wewe ni mtumishi mwema na mwaminifu.

Basi, sikusema neno, ila nilikiinamisha kichwa tu. Akasema ‘’Nataka kusema nawe, basi keti ustarehe’’ akajijongeza kitandani afanye nafasi niketi. Nikasema ya kuwa sistahili kuketi pamoja na Malkia.

Akasema, ‘’Keti.’’

Basi, nikaketi, akaanza kinitazama sana kwa macho yake makubwa meusi, kisha akasema, ‘Inkubu, unapenda uwezo?’ Nikamjibu ya kuwa nadhani wanaume wote hupenda uwezo wa namna namna.

Akasema, ‘Utaupata. Unapenda utajiri?’ Nikamjibu ya kuwa napenda utajiri kwa ajili ya vitu vinavyoletwa nao.

Akasema, ‘Utaupata.unapenda uzuri?’ Nikajibu kuwa napenda kazi za sanaa na za ustadi na kadhalika.

Akaukunja uso wake. Basi,ikawa sasa nimefadhaika hata nilikuwa ninatetemeka, nikajua ya kuwa mambo mabaya yatatokea, maana nilikuwa kama nimeduwaa, wala sikujiweza.

Mwisho akasema, Inkubu, wataka kuwa mfalme ‘’Tazama u mgeni, mimi ninafikiri kukufanya mfalme wa Wazuvendi wote, na mume wake Sorais.

La! Nyamaza kwanza unisikilize vyema. Siwezi kuthubutu kumwambia hivyo hata mtu mmoja katika watu wangu hisia za moyo wangu. Lakini wewe ni mgeni na kwa hivi nimeweza kusema nawe bila kuona haya.

Tena nakumbuka yote ninayoweza kukupa, na kutambua jinsi ilivyo vigumu kwako kuniposa.

Tazama, ufalme umewekwa miguuni pako, Bwana wangu Inkubu, na pamoja na ufalme, mwanamke ambaye wengine wametamani kumposa. Na sasa nijibu, Ee mteule wangu, na maneno yako yatakuwa matamu masikioni mwangu.’’

‘’Nikasema, Ee Sorais, nakuomba usiseme namna hii, maana mambo hayo hayawezi kuwa. Nimekwisha mposa dada yako, nami nampenda yeye! Yeye tu.’’

Basi, nilipokuwa nikisema, Sorais aliuficha uso wake kwa mikono yake, na alipoyasikia maneno yangu, aliuinua uso wake pole pole, nilipouona uso wake nilifadhaika sana, maana uso wake ulikuwa mweupe kabisa na macho yake yaling’aa kama balbu.

Akaondoka, akasimama na kuvuta pumzi kama kwamba roho yake inataka kumtoka. Mara alikitazama kisu kilichokuwapo mezani, kisha akanitazama mimi kama kwamba anafikiri kuniua pale pale lakini hakukitwaa.

Mwishowe akasema neno moja tu, ‘Nenda!’ nikaondoka, nikashukuru kutoka chumbani humo salama.

Sasa je, nitafanya nini?’’ Nilikitikisa kichwa changu, maana mambo yamekwisha kuwa mabaya sana. Hata katika Jehanamu hakuna ukali kama wa mwanamke aliyekataliwa! Na hasa kama ni mwanamke kama Malkia Sorais. Nikahofia yale yatakayotokea, na pamoja nayo hatari ya maisha yetu.

Nikasema, ‘’Lazima Nyleptha aambiwe habari hizo haraka, nami naona afadhali nimwambie mimi; maana ukimwambie wewe haikosi atashuku neno. Nani mkubwa wa zamu usiku huu?’’

Akajibu Sir Henry ‘ni Kara’ Nikasema. ‘’Vyema, naona hapana anayeweza kumdhuru Nyleptha. Usishangae, maana mimi nadhani bila shaka Sorais atajaribu kumdhuru.

Je, tumwambie Bwana Good habari za mambo yaliyotokea?’’

Sir Henry akasema, ‘’Sijui, maana habari hizi ndizo zitamuumiza sana hasa kwa jinsi anavyompenda Sorais.’’

Nikasema, ‘’Kweli, na labda hapana haja kumwambia. Atapata habari mwenyewe upesi. Sasa, sikiliza maneno yangu! Bila shaka sasa Sorais atajipanga upande wa Nasta aliyenuna huko katika nchi yake ya kaskazini, na vita vitatokea ambavyo namna yake havijatokea katika nchi ya Zuvendi kwa miaka mingi.

Tazama! ‘’nikamwonyesha na tarishi wawili wanaotoka mbio chumbani mwa Sorais. Nikasema, ‘’Nifuate,’’ nikapanda ngazi ya kufikia juu ya mnara wa kulinda zamu, nikachukua darubini nikatizama juu ya ukuta wa jumba.

Tukamwona tarishi anakwenda mbio Hekaluni. Hakosi anampelekea habari kuhani mkuu, Agon. Sikumwona yule tarishi wa pili. Lakini halafu kidogo, niliona mpanda farasi anakwenda mbio sana kupita katika mlango wa bustanini wa mji, nikatambua ni yule tarishi wa pili.

Nikasema, ‘’Ah! Ama Sorais ni mwanamke wa juhudi. Anafanya mambo upesi, tena kwa ustadi na kwa nguvu.

Umefanya kama kumtukana, na sasa damu ya watu itamwagika kama mito kabla jua halijafutika , na damu yako pia akiweza kukushika.

Basi, nakwenda kumwambia Nyleptha. Wewe kaa hapa hapa ujaribu kutulia tena.’’

Nikaondoka.

Nilipata ruhusa kuonana na Nyleptha upesi. Alikuwa akimtazamia Sir Henry, na aliponiona mimi alisema, ‘’Bwana wangu mgonjwa?

Makumazanh! Hata haji kunitazama. Natumaini si mgonjwa.’’

Nikamwambia ya kuwa hajambo, ndipo nilipoanza kumwambia habari zile toka mwanzo mpaka mwisho.

Lo! Angalia basi jinsi alivyoghadhabika! Akasema,

‘’Umethubutuje kunijia na kuniambia hadithi ya uongo kama hii? Kusema kuwa Bwana wangu alikuwa akishughulika na dada yangu Sorais! Ni uongo kabisa.’’

Nikamjibu, ‘’Niwie radhi Malkia, nilisema kuwa Sorais ndiye aliyekuwa akishughulika na Bwana wako.’’

Akasema, ‘’Usinitandazie utando wa buibui wa maneno. Si mamoja pia? Mmoja hutoa, mwingine hupokea na zawadi hupitishwa, si haja kugundua mwenye hatia ni nani! Sorais! Ee jinsi ninavyomchukulia Sorais Malkia, tena ni dada yangu. Hakika hangalifanya mambo hayo kama asingalivutwa.’’

Nikajibu, ‘’Nyleptha, unajua kabisa kuwa maneno yako ni ya upuuzi mtupu, na wakati huu si wakati wa kufanya upuuzi.’’

Akaupiga mguu wake chini kwa hasira, akasema, ‘’Unathubutuje kusema maneno kama haya? Je, Bwana wangu mwongo amekutuma unitukane hata na mimi? Wewe ni nani? si mgeni! hata kuthubutu kusema na mimi Malkia, tena kwa maneno kama haya?’’

Nikajibu, ‘’Naam, nimethubutu. Sikiliza! Dakika hizi unazopoteza kwa ajili ya hasira zako za bure, zaweza kulipoteza taji lako, na maisha yetu pia.

Wapanda farasi wa Sorais wamekwisha kwenda kukusanya jeshi. Katika muda wa siku tatu. Nasta atajiamsha katika milima yake kama simba wakati wa jioni, na ngurumo zake zitasikika katika nchi ya kaskazini.

Sorais ana sauti tamu, naye hataitumia bure. Bendera yake itachukuliwa toka mlima mpaka mlima, na toka bonde mpaka bonde, na askari wataifuata kama mavumbi yanayofuata chamehela.

Nusu ya jeshi zima la nchi watamfuata na katika kila mji na kijiji makuhani watawasengenya wageni, nao watafanya vita hivi viwe vita vya kidini Nimesema Ee Malkia.’’

Nyleptha alikuwa ametulia sasa, hasira yake na wivu ulikuwa umitulia, akajibadili kabisa kwa haraka, na sasa si mwanamke yule mwenye wivu tena ila ni Malkia mwenye kuweza kazi na matendo.

Akasema, ‘’Maneno yako, Ee Makumazahn, ni ya busara. Nisamehe upuuzi wangu mahaba ni kama umeme. Ni mzuri mno nao huunganisha dunia na mbingu, lakini ole wetu, namna unavyoyapofua macho. Nawe unafikiri kuwa dada yangu Sorais atafanya vita nami. Basi, na afanye.

Hatanishinda ng’o. mimi pia ninao rafiki zangu na wafuasi wangu. Wako wengi watakao ziinua sauti zao na kuita ‘Nyletpha’, bendera yangu itakapotwekwa, na mioto yangu itakapowashwa karibu milima usiku huu kuwajulisha habari za vita vyangu.

Nitazivunja nguvu zake na kuwatawanya askari zake, na sehemu ya Sorais, ‘bibi wa usiku’ itakuwa usiku wa milele. Nipe karatasi na wino.

Asante. Sasa mwite mkubwa wa zamu, najua ni mtu mwaminifu.’’

Nilifanya kama alivyo niambia, na mkubwa wa zamu, mzee mtulivu jina lake Kara aliingia, akajiinamisha kwa heshima.

Nyleptha akampa karatasi ile akamwambia, ‘’Twaa hati hii, ni nguvu zako, weka watu kulinda kila mahali pa kutokea na kuingilia vyumbani mwa dada yangu Sorais, ‘bibi wa usiku.’ Watu wasipewe ruhusa kutoka wala kuingia, au maisha yako yatatozwa.’’

Yule mtu alishangaa mno, lakini hakusema neno ila ‘’Neno la Malkia litimizwe .’’ Akaondoka. Kisha, Nyleptha akatuma mtu kumwita Sir Henry , akaja anaona haya nyingi. Nilifikiri labda Nyleptha ataanza tena maneno yake ya wivu, lakini hakumtaja.

Basi, halafu kidogo, yule mkubwa wa zamu aliyetumwa, akarudi kupasha habari ya kuwa Sorais amekwisha ondoka. Alikuwa amekimbilia hekaluni.

Basi, hapo tukaanza kufanya mashauri.

Majemadari waliojulikana kuwa ni waaminifu wakaitwa, wakaambiwa habari, si zote, ila zilizotosha kufahamu mambo jinsi yalivyo, wakaamrishwa kukusanya watu wa vikosi vyao kadiri walivyoweza.

Nyleptha akawaambia wakuu wengine alioweza kuwatumaini, na wengine wao walitoka siku ile ile kwenda mahali pa mbali kuwakusanya wafuasi wao na watu wa makabila yao.

Basi, mchana kutwa na jioni tulifanya kazi ya kutuma matarishi huko na huko, wala hatukurudi vyumbani mwetu mpaka saa mbili za usiku. Kabla ya kulala, Sir Henry akafikiri ni vizuri kumwambia Umslopogaas alinde zamu karibu na chumba cha Nyleptha.

Umslopogaas alikuwa anajuana na watu wote wa jumbani, na Malkia walikuwa wamekwisha toa amri aruhusiwe kwenda popote apendapo, akazoea kutembea tembea usiku, kwa hiyo, hata kama akionekana anatembea karibu na chumba cha Malkia, watu hawatashuku jambo.

Basi, alilitwaa shoka lake, akaondoka, na sisi tukalala.

Ilikuwa kama kwamba nimelala dakika chache tu, nikaamshwa kwa kuona kama mambo si sawasawa.

Niliona kama kwamba yumo mtu chumbani ananitazama, mara ile niliketi kitandani, nikastajabu kuona kumekwisha pambazuka, na karibu na kitanda changu, Umslopogaas amesimama kama kivuli.

Nikamuuliza, ‘’Je, umesimama hapa kwa muda gani?’’

Akajibu ‘’Kadiri ya nusu saa Makumazahn.. nataka kusema nawe.’’

Basi, mara ile nilikuwa macho kabisa, nikamwambia aseme maneno yake.

Akasema, ‘’Kama nilivyoambiwa usiku, nilikwenda kulinda zamu karibu na chumba cha Malkia, basi nilijificha nyuma ya nguzo katika chumba kilicho karibu na chumba cha kulala cha Malkia, nikangoja.

Bougwan (Bwana Good) alikuwa peke yake katika chumba cha zamu, na nje ya chumba askari mmoja wa zamu alikuwa amesimama.

Nikataka kujua kama ninaweza kupita bila kuonekana, nikaweza, nikapita nyuma yao. Basi, hapo nilingoja saa kadha wa kadha, ndipo ghafla niliona mwanamke anakuja ameshika kisu mkonononi mwake.

Tena nilimwona Bougwan amevivua viatu vyake anamfuatia yule mwanamke. Yule mwanamke alipita karibu nami, nikamwona alikuwa ‘Bibi wa Usiku,’ Basi, nikangoja, na Bougwan naye alinipita pia.

Basi, vivyo hivyo tuliendelea pole pole kimya kabisa. Wa kwanza yule mwanamke, wa pili Bougwan na wa tatu mimi, ila yule mwanamke hakumwona Bougwan, na Bougwan naye hakuniona mimi.

‘’Basi, ‘Bibi wa Usiku ‘ alifika mpaka katika pazia la chumba cha Malkia Nyleptha, akapita ndani na Bougwan alimfuatia, na mimi niliwafuatia.

Mwisho wa chumba ni kitanda cha malkia, na Malkia alikuwa amelala usingizi.

‘Bibi wa Usiku’ alijikunia hivi na huku ameshika kisu tayari, akanyemelea mpaka kitandani pa Malkia. Alipokikaribia sana, Bougwan akamgusa mkono, na mara ile aligeuka akampiga kisu.

Kwa bahati Bougwan alikuwa amevaa deraya chini ya nguo zake, ama sivyo angalimdhuru. ndipo Bougwan alipomtambua yule mwanamke yu nani, akarudi nyuma ameshangaa asiweze kusema neno.

‘Bibi wa Usiku’ naye alishangaa, asiseme neno ila alikiweka kidole chake midomoni pake, akarudi , akapita katika pazia, na Bougwan alimfuatia.

Basi, hivyo walipita, nikamsikia yule mwanamke kama anamsihi, nayeye anajibu, Hapana! Hapana! Hapana.

Nikaona kuwa anataka kuwaita askari wa zamu, lakini Malkia Sorais aliacha kusema, akamkazia macho yake makubwa, nikaona ya kuwa Bougwan ameshindwa kujizuia kwa uzuri wake.

Kisha aliunyosha mkono wake na Boungwan aliubusu, nikajifanya tayari kumkamata, mara! Akatoweka.’

Nikasema, alitoweka?’’

Akajibu, ‘’Ndiyo, na Bougwan alisimama akimtizama ukutani kama kwamba ameshikwa na jinamizi la usingizi. Kisha, naye pia akaenda, na mimi nikaja hapa.’’

Nikamuuliza, ‘’Una hakika Umslopogaas ya kuwa hukua unaota ndoto ya mambo hayo?’’

Akaufumbua mkono wake, akanionyesha kipande cha chuma cha bapa la kisu, kadiri ya inchi tatu, akasema, ‘’Makumazahn, kama niliota ndoto, basi, tazama kitu nilichopewa kwenye hiyo ndoto.

Kisu kilivunjikia katika deraya za Bougwan, na nilipopita nilikiokota hiki katika chumba cha kulala cha Malkia Nyleptha.’’

SURA YA KUMI NA NANE

Basi nilimwambia Umslopogaas aningojee, nikavaa nguo zangu kwa haraka nikamchukua mpaka chumbani mwa Sir Henry, akaisimulia tena ile hadithi yake.

Uso wa Sir Henry uligeuka rangi alipoisikia, akasema, ‘’Ole wangu na mimi nilikuwa nimelala usingizi na huku Nyleptha alitaka kuuawa tena kwa ajili yangu pia.

Lo, angalia jinsi Yule Sorais alivyo mwovu. Ingekuwa haki yake Umslopogaas angalimuua kwa shoka lake.’’

Umslopogaas akasema, ‘’Ndiyo usiwe na shaka; ningalimuua kabla hajamuua dada yake. Nilikuwa tayari nikingojea.’’

Basi, alipokwisha kuisimulia hadithi yake, Umslopogaas alikwenda kula chakula chake cha asubuhi kama kwamba hakuna jambo lililotokea, na Sir Henry na mimi tukakaa tunazungumza.

Kwanza aliona uchungu kwa sababu ya Bwana Good, akasema kuwa hawezi kutumainiwa tena, kwa kuwa amemwacha Sorais atoke kwa njia ya siri badala ya kumkamata na kumfunga kama ilivyokuwa wajibu wake.

Nikasema, ‘’Usisahau ya kuwa wewe ulikutana na mwanamke yule, ukaona vigumu kujizuia usishindwe na uzuri wake.’’

Lakini ingawa nilisema haya, nilifikiri moyoni ya kuwa ingawa anampenda sana Sorais, Bwana Good amefanya jambo la aibu kumwacha aende zake. Maana alinuia kumuua dada yake, naye amemwacha huru.’

Halafu Bwana Good akaja na uso wake ulionyesha namna alivyokuwa akiona mashaka, na mara Umslopogaas alipomwona akasema,

‘’Ah Bougwan, salamu Mkuu! Kweli umechoka kwa kuwinda sana’’

Kisha, asingoje kujibiwa, akasema,

‘’Sikiliza Bougwan, nitakusimulia hadithi ni habari za mwanamke na kwa hiyo utazisikiliza sivyo.’’

‘’Palikuwa na ndugu wawili wanaume! Kaka mtu na mdogo wake, ikatokea mwanamke moja anampenda sana Yule ndugu mdogo, na yule ndugu mkubwa naye pia anampenda sana Yule mwanamke.

Lakini yule ndugu mdogo alikuwa na mke mwingine mpenzi wake, wala hakumpenda yule mwanamke, akamfanyia dhihaka. Basi, yule mwanamke kwa kuwa alikuwa mwerevu na mwenye moyo wa kutaka kisasi akafikiri moyoni, akamwambia yule ndugu mkubwa, ‘Nakupenda, na ukifanya vita juu ya ndugu yako nitakusaidia.’

Na yule ndugu mkubwa alijua kuwa ni uongo, lakini kwa kuwa alimpenda sana yule mwanamke aliyasikiliza maneno yake akafanya vita na ndugu yake.

Na baada ya kuuawa watu wengi, ndugu yake alimpelekea ujumbe kumuuliza’ mbona wataka kuniua?

Toka utoto wangu nimekupenda. Nimekudhuru namna gani? Ni ubaya gani niliokutendea kufikia kutaka kuniua? Ulipokuwa katika dhiki sikukuona hata nikakusaidia? Nasi hatukuenda pamoja kufanya vita! Tukagawanya mateka, mwanamke kwa mwanamke, ng’ombe kwa ng’ombe!

Basi, sasa mbona wataka kuniua ndugu yangu mpenzi?.

‘’Basi moyo wa yule ndugu mkubwa uliingia simanzi, akajiutia matendo yake maovu, akamwepuka yule mwanamke, akavikomesha vile vita, akakaa katika nyumba moja pamoja na ndugu yake.

Na baada ya muda kupita, Yule mwanamke akamjia tena Yule akasema, ‘’Na tuyasahau mambo yaliyopita, nitakuwa mke wako.’’ Na katika moyo wake alijua kuwa anasema uwongo, lakini kwa sababu alimpenda sana akamwoa.

‘’Na usiku ule ule waliooana, yule mwanaume alipokuwa amelala usingizi, yule mwanamke aliondoka kitandani akatwaa shoka lile analotumia mumewe, akanyemelea toka katika nyumba walimolala, akaingia chumbani mwa yule ndugu yake, akamuua pale pale alipokuwa usingizini.

Kisha akanyemelea akarudi chumbani tena kama simba aliyekwisha kula shibe yake, akaweka kitanzi cha kipini cha shoka lile lenye damu katika kiwiko cha mkono wa mume wake aliyekuwa bado amelala usingizi, akatoweka akaenda zake.’’

‘’Kulipo pambazuka, watu wa jumbani humo wakapiga ukelele ‘Lousta ameuawa usiku.’ Wakaja hata chumbani mwa yule mwanaume kumpasha habari, wakamkuta bado amelala, na karibu naye lipo lile shoka lenye damu limelala.

Ndipo walipovikumbuka vile vita, wakasema, ‘’Tazama! Hakika amemuua ndugu yake,’ wakataka kumuua, lakini alikuwa mwepesi kuwa toroka basi akakimbia, na alipokuwa akikimbia alimuona yule mwanamke akampitia na shoka lake na akamuua.’’

‘’Lakini mauti ya yule mwanamke haikuweza kuyafuta maovu yake aliyoyafanya, na uzito wa ile dhambi yake ulimkalia yule mwanaume. Kwa hivi ametupwa na watu wake, na jina lake ni twezo katikati ya watu wake maana mzigo wa dhambi aliyoitenda yule mwanamke umetwikwa juu yake peke yake.

Basi, sasa yule aliyekuwa mkuu hutembea tembea huko na huko mbali na kwao, hana nyumba wala mke, na kwa hiyo atakufa kama mnyama aliyepigwa , na jina lake limelaaniwa toka vizazi hata vizazi, kwa kuwa watu husema alimuua ndugu yake, Lousta, kwa hila wakati wa usiku.’’

Basi, yule mzee Mzulu akanyamaza kidogo, nikaona jinsi hadithi yake inavyomhuzunisha. Halafu alikiinua kichwa chake tena, akaendelea.

‘’Mimi ndiye huyo mtu, Bougwan. Ndiyo Mimi ni mtu Yule, na wewe unisikilize! Kama mimi nilivyo, hata na wewe ndivyo utakavyokuwa chombo,kitu cha kuchezea, ng’ombe achukuaye mzigo wa maovu ya mtu mwingine.

Sikiliza. Wewe uliponyemelea kumfuata, ‘Bibi wa Usiku’ mimi nilikuwa nikikufuatia wewe. Alipokupiga kisu katika chumba cha kulala cha Malkia Nyleptha, mimi nilikuwamo pia, ulipomwacha aende zake kama nyoka katika miamba, mimi nilikuona , nikajua ya kuwa amekuloga, na yakuwa mtu mwaminifu ametoka katika uaminifu wake, na yeye ambaye alipenda njia iliyonyooka, amechagua njia iliyopotoka.

Nisamehe baba yangu, kama maneno yangu ni makali, lakini yanatoka katika moyo uliojaa.

Usionane naye tena, na hivyo utashuka katika kaburi lako kwa heshima ama sivyo, labda wewe utakuwa kama mimi nilivyo, tena kwa haki kuliko mimi! Tena wengi wameangushwa kwa ajili ya uzuri wa mwanamke unaochakaa kama vazi lililokwisha valiwa,ujiepushe usizidishe hesabu yao. Nimesema!’’

Basi, wakati Umslopogaas alipokuwa akisema maneno hayo Bwana Good alisimama kimya kabisa, lakini hadithi ilipoanza kufanana na hali yake ilivyo, aligeuka rangi, na alipojua ya kuwa habari zile. Za yeye na Sorais zimebainika, alifadhaika sana.

Mwishowe, akaanza kusema, na sauti yake ilikuwa ya unyenyekevu, wala si kama yake ya desturi, akasema, ‘’Sijawahi kufikiri ya kuwa ipo siku nita fundishwa wajibu wangu na Mzulu lakini mambo yaonyesha namna tunavyoweza kushawishiwa.

Labda mtaweza kufahamu jinsi ninavyoona aibu, tena nimestahili kuaibika. Kweli ilikuwa wajibu wangu kumshika Sorais na kumweka katika mikono ya askari wa zamu, lakini sikuweza, basi.

Nilimwacha aende zake, nikaahidi sitaitoa nje habari hiyo, ndiyo aibu yangu, Aliniambia ya kuwa nikijipanga upande wake atakubali nimwoe na kunifanya mfalme wa nchi hii, lakini nashukuru ya kuwa nilikataa hata alipoahidi nimwoe, nikasema kuwa siwezi kuwahaini rafiki zangu,Basi,ndugu zangu mnaweza kufanya mnayotaka kunifanyia, nimeyastahili yote.

Nitasema haya nawaomba nanyi mjilinde msipende mwanamke kwa moyo wenu wote na kujaribiwa naye kama mimi nilivyojaribiwa,'' akageuka ili aende.

Sir Henry akasema, ''Mwenzangu, ngoja kwanza. Mimi nina hadithi ninayotaka kusimulia.''

Akamsimulia habari ya mambo yale yaliyotokea jana baina ya yeye na Sorais. Basi, habari za mambo yale zilimvunja moyo zaidi maskini Good. Akasema, ''Nadhani habari hizi zimekwisha niponya,'' akageuka akaenda zake, nami nilimsikitikia sana.

Siku ile ilikuwa siku ya baraza ambayo Malkia walizoea kukaa katika sebule kubwa na kusikiliza haja za watu, na kufanya mashauri mengineyo ya sheria na fedha, na mambo kadha wa kadha, basi baadaye kidogo tulikwenda sebuleni, na Bwana Good akafuatana nasi.

Tulipofika tulimkuta Nyleptha amekwisha kaa kitini pake, na mambo yanaendelea kama kawaida, amezungukwa na washauri, wakuu, wana sheria, makuhani, na jeshi kubwa kidogo la askari.

Lakini ilikuwa dhahiri kwa nyuso za watu na kwa namna watu walivyoongeaongea, ya kuwa hawaangalii mambo ya kawaida ila wanatazamia mengine, maana habari zimekwisha enea kuwa vita vya kindanindani vi karibu.

Basi, tukamwamkia Nyleptha, tukakaa katika mahali petu pa siku zote, pia muda mambo yaliendelea kama kawaida, mara tarumbeta zilianza kupigwa nje ya jumba, na mlio mkubwa uliwatoka umati wa watu waliokuwa wamehudhuria nje kutazama mambo yatakayotokea:

''Sorais! Sorais! Ndipo mingurumo ya magurudumu ya magari iliposikika na halafu pazia kubwa mwisho wa sebule lilivutwa upande, na Sorais ''Bibi wa Usiku'' aliingia, wala hakuja peke yake.

Agon kuhani mkuu alimtangulia amevalia mavazi yake yaliyo bora, na kila upande wake makuhani walishindamana.

Sababu ya kuwako makuhani ilikuwa dhahiri, maana kwa kuwa amefuatana nao, hawezi kuzuiliwa, kwa kuwa kuwazuia makuhani ni kufanya mambo ya kufuru. Nyuma yake walikuwako wakuu wengine na kundi la askari waliochaguliwa.

Kumtazama tu ikawa dhahiri kuwa Sorais hakuwa na amani, maana badala ya mavazi yake ya siku zote amevaa mavazi namna ya kiaskari, tena alikuwa amechukua mkuki mdogo wa fedha mkononi mwake.

Basi, alipita katikati ya sebule na watu walijitenga wampishe njia, na alipofika karibu na mwamba mtakatifu alisimama, akaweka mkono wake juu yake, akasema kwa sauti kubwa. ‘’Salamu, Ee Malkia!’’

Na Nyleptha akajibu ‘’Salamu dada yangu! Karibu usiogope hutadhurika.’’

Sorais hakusema neno, akapita mpaka akasimama mbele ya viti vya kifalme, kisha akasema, ‘’Nina haja Ee Malkia!’’

Nyleptha akajibu, ‘’Sema, dada yangu, kuna kitu gani zaidi ninachoweza kukupa nawe unao nusu ya ufalme wote.’’

Akajibu, ‘’Unaweza kuniambia mimi na watu wote wa Zuvendi habari za kweli. Utamtwaa yule mgeni mbwa mwitu kuwa mume wako ama sivyo?’’

Akamwelekezea mkuki wake mdogo Sir Henry.

Sir Henry akaukunja uso wake, akageuka akamwambia Sorais kwa sauti ndogo, ‘’Nakumbuka ya kuwa jana ulikuwa na majina mengine ya kuniita wala si mbwa mwitu, Ee Malkia.’’

Basi, hapo Nyleptha aliona mambo hayawezi kifichika tena, akaondoka, akashuka katika kiti chake, akaenda mpaka pale Sir Henry alipokuwepo, akasimama pale pamoja naye.

Akaiondoa bangili ya dhahabu mfano wa nyoka katika mkono wake, akamwambia Sir Henry apige magoti, akapiga goti moja, kisha, akaitwaa bangili ile ya dhahabu akaikunjua akaiweka shingoni mwa Sir Henry, akambusu pajini, akamwita ‘’Bwana mpenzi.’’

Kisha akasema, ‘’Waona, nimeiweka bangili yangu katika shingo ya mbwa mwitu, na tazama! Atakuwa mbwa wa kunilinda, ndilo jibu langu kwako wewe Malkia Sorais dada yangu, na kwa watu waliyofuatana nawe.’’

Kisha, akageuka akawaambia wote waliopo kwa sauti thabiti, ‘’Ndiyo, Bibi wa Usiku, na wakuu, na makuhani na watu wote mliopo , hii ndiyo dalili mbele yenu nyote, ya kuwa nimemtwaa mgeni huyu awe mume wangu.’’ Akamshika mkono wake akawatazama watu wote kwa ujasiri.

Tendo alilolitenda lilikuwa la uhodari, na Wazuvendi, kama watu wote walivyo, hupenda ujarisi, basi walipaza sauti zao kwa shangwe.

Lakini Sorais alisimama akitazama chini, maana hakuweza kustahimili kuiona furaha ya dada yake, na jinsi alivyomwibia mwanaume aliyetumaini kumpata, akatetemeka kwa hasira ya wivu aliouona.

Kisha, aliuinua uso wake, akaunyosha juu mkuki wake mdogo, akautikisa, akasema.

‘’Na wewe Nyleptha, unafikiri kuwa mimi Sorais, Malkia wa Zuvendi nitakubali mgeni huyo akikaliye kiti cha kifalme cha baba yangu? Hasha! Hasha! Kifua changu kingali na uzima ndani yake, na watu wangalipo wa kunifuata na mkuki upo wa kupigia, sitakubali! Nani, nani watakaonifuata mimi?

Sasa Nyleptha, mtoe mgeni mbwa mwitu na wale waliokuja pamoja naye wauawe kwa moto, maana sio hawa waliyofanya dhambi ya kufisha juu ya Jua kama sivyo, basi nitapigana vita! Vita vya damu! Nakuambia Nyleptha nitakubandua katika kiti chako, nawe utatupwa, utatupwa toka juu ya ngazi kuu mpaka chini yake, kwa sababu umetia aibu nyumba ya kifalme.

Na ninyi wageni, nawaambieni nyote isipokuwa Bougwan, ambaye kwa kuwa alinitumikia nitamwokoa akiwaacha wenzake, (na Bwana Good alikitikisa kichwa chake sana kukataa) nitawafunika kwa mabati ya dhahabu na kuwafungia minyororo mngali hai katika ncha za panda za sanamu zile nchani mwa dari, iliiwe dalili na maonyo kwa watu wote.

Na wewe Inkubu, wewe utakufa kwa namna nyingine ambayo sitakuambia sasa.’’

Basi, akanyamazana akitweta, maana ghadhabu yake ilimtikisa kama tufani, na mnong’ono wa nusu hofu na nusu kumsifu, ulivuma katika sebule.

Kisha, Nyleptha akajibu kwa madaha na utulivu, akasema, ‘’Dada yangu, heshima yangu ingevunjika kabisa kama ningesema maneno kama hayo uliyoyasema, na kuogofya kama wewe ulivyoogofya.

Lakini ukifanya vita, basi, mimi nitajaribu kupigana nawe, maana ingawa mikono yangu huonekana kuwa nyororo, lakini itakuwa kama chuma cha kukaba koo za jeshi lako. Sorais, sikuogopi!

Nahuzunika kwa mambo utakayoyaleta juu ya watu wetu na juu yako mwenyewe, lakini kwangu mimi, nasema, sikuogopi. Na wewe jana tu ulijaribu kumvuta Bwana wangu awe mpenzi wako na Bwana wako, ambaye leo unamwita mgeni mbwa mwitu.

Tena, usiku huu huu ulininyemelea kama nyoka mpaka katika chumba changu cha kulala kwa njia ya siri, nawe ulijaribu kuniua, mimi dada yako, katika usingizi wangu’’

Sauti ya Agon na watu wapatao ishirini wengine zililia, ‘’Uwongo! Uwongo!’’

Basi, hapo nilisimama mbele, na huku ninakiinua kile kipande cha kisu, nikasema, ‘’Si uwongo, je, kipini cha kisu hiki ki wapi Ee Sorais?’’

Na Bwana Good akajitokeza ili authibitishe uaminifu wake tena, akasema, ‘’Si uwongo. Nilimshika ‘Bibi wa Usiku’ pale kitandani pa Malkia Nyleptha, na kisu chake kilivunjikia kifuani pangu.’’

Basi Sorais aliona kuwa mioyo ya watu inageuka upande mwingine, akautikisa mkuki wake, akasema, ‘’Nani wako upande wangu? Je, Bougwan?’’ Hivi akageuka kumuuliza kwa sauti ndogo, kisha akaendelea.

‘’Wewe mwoga, kama ungalinifuata mimi ungeweza kuwa mfalme wangu na mume wangu’’

Akalia, ‘’Vita! Vita! Vita! Hapa nimesimama na mkono wangu juu ya mwamba mtakatifu utakaodumu mpaka Wazuvendi watakapojiinamisha chini ya mgeni. Nani watamfuata Sorais katika kushinda na kujipatia heshima.’’

Mara umati wa watu ulianza kufumukana kwa ghasia. Wengi waliokuwapo walijipanga upande wa Sorais, lakini wengine walitoka upande wake wakajipanga upande wetu. Katika hao waliotutoka, kiongozi mmoja wa askari wa Nyleptha aliyegeuka alijaribu kukimbia mlangoni walimopita watu wa Sorais.

Lakini Umslopogaas alikuwapo anatazama, akamshika, maana aliona kuwa akitoka, basi wengine watamfuata. Basi, Yule askari aliufuta upanga wake akajaribu kumpiga Umslopogaas.

Hapo, Mslopogaas alirudi nyuma kwa mlio mkali akauepuka upanga, akalizungusha shoka lake, akampiga, na Yule askari akaanguka chini amekufa.

Basi, hii ilikuwa damu ya kwanza kumwagika katika vita. Nikalia, ‘’Fungeni milango’’ nikifikiri kuwa labda tutaweza kumzuia Sorais, na kwa namna hii kuzuia matata.

Lakini tulichelewa; basi yeye na askari zake walikuwa katika kupita, na mara walikuwa wakienda mbio katika njia zao, zikajaa sauti za farasi na mingurumo ya magurudumu ya magari yake.

Basi, Sorais, akapita akivuta nusu ya watu nyuma yake kama chamchela katika mji, akashika njia yake kuiendea Marstuna iliyo ngome kadiri ya maili mia moja na thelathini upande wa kaskazini wa Milosis.

Baada ya hayo, mji ulijaa sauti za vishindo vya vikosi na matengenezo ya vita, Mzee Umslopogaas alianza tena kukaa katika jua na kuyanoa makali ya Inkosikazi.

SURA YA KUMI NA TISA

Lakini palikuwa na mtu mmoja ambaye hakuweza kutoka kwa haraka kabla milango haijafungwa, ndiye kuhani mkuu Agon, ambaye tulisadiki ya kuwa ni msaidizi mkuu na mwongozi wa kundi la Sorais.

Mtu mkali mwereve huyu alikuwa hajatusamehe jambo lile la kuwaua viboko, ndivyo alivyosema. Sirini kwa kweli hakuweza kustahimili tulete maarifa ya kigeni, yaani ikiwa anaweza kuyazuia.

Tena, alijua ya kuwa dini yetu si dini yake, naye hakosi aliogopa kuwa tutajaribu kuifundisha, dini yetu katika nchi ya Zuvendi. Siku moja aliniuliza kama iko dini katika nchi yetu, nikamwambia ya kuwa kadiri ninavyoweza kukumbuka yapo madhehebu ya dini zipatazo tisini na tano. Aliposikia hivyo alistaajabu sana.

Basi, tulipopata habari ya kuwa Agon amekamatwa, Nyleptha, na Sir Henry na mimi tulifanya shauri tumfanye nini? Mimi nilitaka kumfunga asiweze kutoka tena, lakini Nyleptha alikitikisa kichwa chake akasema tukifanya hivyo tutaleta ghasia katika nchi nzima, akasema ‘’Lakini! Nikishinda na mimi peke yangu ni Malkia, basi nitazivunja nguvu za makuhani hawa, na kuondoa ibada na michezo na matendo yao ya giza na siri.’’

Basi, Sir Henry akasema, ‘’Basi kama hatumfungi, ni afadhali tumwache aende zake, maana hatatusaidia kitu hapa.’’ Nyleptha alimtazama upande upande akasema, ‘’Ndiyo unavyofikiri bwana wangu?’’ Sir Henry akajibu, ‘’Ndiyo, sioni faida ya kumweka hapa.’’

Nyleptha hakujibu neno ila alimtazama na huku anakiinamisha kichwa chake kwa haya, ndipo alipofahamu akasema, ‘’Nisamehe Nyleptha. Ni kweli kuwa utaolewa nami sasa?’’

Nyleptha akajibu, ‘’Sijui bwana, lakini kama bwana wangu unataka, basi, kuhani yupo, madhabahu ipo,’’ akakielekeza kidole chake kulinyoshea hekalu dogo lililokuwa karibu, ‘’na mimi nipo tayari kufanya utakavyo bwana wangu.

Ee bwana wangu, katika muda wa siku nane au muda mfupi zaidi huna budi kuniacha kwenda vitani, maana ndiwe utakayewaongoza watu vitani, na katika vita watu pengine huuawa, na ikiwa mambo haya yatatokea, basi, ningependa niolewe nawe ili niweze kuwa na kumbukumbu,'' aliposema hivyo machozi yalimtoka machoni yakamtiririka usoni kama umande katika moyo wa ua.

Akaendelea, akasema, ''Tena, ikitokea kuwa nitashindwa, na taji itanipotea, na maisha yangu pamoja na taji, na maisha yako pamoja na yangu.

Sorais ana nguvu nyingi, tena ana uchungu sana, na akishinda hatakuwa na huruma.'' Basi niliwaacha nikarudi chumbani nikifikiri juu ya mambo, nikamtazama mzee Umslopogaas akilinoa shoka lake.

Na baada ya kupita kadiri ya muda wasaa moja, Sir Henry akaja mbio amefurahi sana, akatuuliza mimi na Bwana Good na Umslopogaas kama tutapenda kushuhudia arusi ya kweli kweli.

Tukasema tutapenda, tukamfuata mpaka hekaluni, tukamkuta Agon na uso wake ulikuwa una hasira sana. Ikatokea ya kuwa yeye na Nyleptha walipambana juu ya arusi hii.

Agon alikataa kabisa kumwoza, wala hakukubali kumpa kuhani mmojawapo wake ruhusa ya kumwoza, na kwa hivi Nyleptha alikasirika, akamkumbusha kuwa yeye ni Malkia, tena mkuu wa dini, naye amenuia ya kuwa watamtii, Agon alizidi kukataa, basi mwishowe Nyleptha akasema.

''Vyema, siwezi kumuua kuhani mkuu kwa sababu watu wataona uchungu , wala siwezi kumfunga kwa sababu makuhani wadogo watafanya kelele na ghasia lakini naweza kumwacha hekaluni mbele ya madhabahu ya Jua atafakari bila chakula cho chote, maana hii ndiyo kazi yake; nawe, ee Agon, usipokubali kunioza, utawekwa mbele ya madhabahu ile pamoja na maji kidogo tu ya kunywa, hata upate nafasi ya kulifikiri jambo hili.''

Basi, Agon alikuwa ameitwa mapema asubuhi wala hakupata nafasi ya kula chakula, na hata hapo anaona. Njaa kwa hivi baadaye kidogo akaghairi akasema ya kuwa atawaoza, lakini asichukue daraka lolote katika mambo hayo.

Basi, baadaye Nyleptha alikuja amefuatana na mabibi wawili, akaja mpaka aliposimama Sir Henry, akamshika mkono akamwongoza mpaka mbele ya madhabahu, na baada ya kitambo Agon akaja akawaoza.

Walipokwisha ozwa na Agon, mimi nilisimama mbele nimeshika kitabu cha sala mkononi mwangu, maana kila niendapo huchukua kitabu changu cha sala, nikasema:

‘’Sir Henry, mimi si kasisi, wala sina habari kuwa yale ninayoyataka kuyafanya ni mazuri najua si sheria lakini kama wewe na Malkia mtakubali nitapenda kusoma ibada ya Ndoa Takatifu ya Kanisa la Kiingereza.

Mambo unayoyafanya ni makuu, nami naona ya kuwa kwa kadiri inavyowezekana, yataka idhini ya dini yako wewe pia.’’

Sir Henry akajibu ‘’Mimi pia nimeyafikiri hayo, na nitapenda sana ufanye hivyo, maana nusu naona kama sijaoa bado.’’

Nyleptha hakukaidi, akafahamu kuwa mume wake anataka ndoa ifungwe kama desturi ya nchi yake, basi nilianza kusoma ibada ya Ndoa Takatifu toka mwanzo hata mwisho.

Huku nyuma Agon alijizuia kwa shida, maana alifahamu upesi ya kuwa wanaozwa kwa kawaida ya dini nyingine, na kwa kweli anafikiri kuwa mimi ni kuhani mkuu, kwa hiyo ni adui yake.

Basi, mambo haya yalipokwisha, Bwana Good na Umslopogaas na mimi tuliondoka tukawaacha Sir Henry na Nyleptha mume na mke. Good na mimi tulikula peke yetu siku ile, tukaona kama kwamba ndiyo kwanza tumemzika rafiki yetu badala ya kumwoza, na asubuhi yake kazi yetu ilianza kwa kweli.

Sasa makundi ya watu wenye silaha walianza kuhudhuria mjini kuitikia barua na matarishi aliopeleka Nyleptha.

Hatukumwona Nyleptha mara nyingi, wala Sir Henry, lakini Bwana Good na mimi tulikaa tukafanya mashauri pamoja na majemedari na wakuu

tukitunga mashauri ya vita, tukitengeneza habari za zana za vita, na kutoa amri na kuangalia mambo kadha wa kadha yanayopasa vita.

Watu wengi walifika, na njia ya kufika Milosis ilitapakaa bendera za wakuu wanaofika pamoja na wafuasi wao kumsaidia Nyleptha.

Baada ya siku mbili ilikuwa dhahiri ya kuwa tutaweza kuanza vita tuna askari wa miguu kadiri ya arobaini elfu, na askari wapanda farasi kadiri ya ishirini elfu, lakini kwa habari tulizozipata, jeshi la Sorais.

Lilikuwa kubwa zaidi. Alikuwa amefanya kambi yake kuu katika mji uitwao Marstuna upande wa kaskazini wa Milosis, na watu wote wa pande za huko walikuwa wakienda kwake kumsaidia, Bwana mkuu Nasta alikuwa ametoka kwake amefuatana na wafuasi wake kadiri ya ishirini na tano elfu, walio askari wakali kupita wote wa Zuvendi.

Mkuu mwingine jina lake Belusha aliyekaa katika nchi walikofuga farasi, alikuwa amefika pamoja na wafuasi wake wapanda farasi kadiri ya kumi na mbili elfu, vivyo hivyo.

Ikaonekana kwamba jumla ya askari wa Sorais hawatapungua kadiri mia elfu.

Ndipo tulipopata habari kuwa Sorais anakusudia kutoka kambini na kujia mji wa Milosis na kuingangamiza nchi yote apitamo. Basi, sasa tulifikiri shauri moja, kama ni afadhali kukaa Milosis mpaka atakapokuja, ama kutoka na kupigana naye njiani.

Tulipoulizwa shauri, Bwana Good na mimi tulisema afadhali tutoke tupigane njiani. Kama tukikaa mjini na kungoja, watu watafikiri tunaogopa.

Tena ni jambo kuu katika shauri kama hili ambalo jambo dogo huweza kugeuza mioyo ya watu, kuanza kushughulika wala si kukaa tu.

Sir Henry naye alikubali shauri letu, na Nyleptha pia. Kadiri ya maili thelathini toka Marstuna, na maili tisini toka Milosis, palikuwa na mahali ambapo njia ilipinda kidogo ikapita katikati ya milima milima yenye misitu minene na upana wa kipito cha katikati kilikuwa kadiri ya maili mbili na

nusu tu, basi, ilikuwa dhahiri ya kuwa kipito hicho kikizibwa, jeshi lenye mizigo mingi ya zana za vita halitaweza kupita.

Nyleptha alifikiri sana, kisha alikitaja kipito kile, akageuka kumtazama mume wake, akasema. ‘’Ni hapa utakapokutana na jeshi la Sorais. Napajua mahali hapo, na hapo utakutana nao na kuwafukuza mbele yako kama mavumbi mbele ya dhoruba.’’

Sir Henry alitazama tu asiseme neno.

SURA YA ISHIRINI

Siku ya tatu asubuhi Sir Henry na mimi tuliondoka. Jeshi lote lilikuwa limekwisha toka usiku isipokuwa kundi dogo tu, na mji wa Milosis ulikuwa hauna watu, tena kimya kabisa.

Hatukuweza kuacha askari mjini isipokuwa wachache tu kumlinda Nyleptha, na wale waliozuiwa wasiende vitani kwa sababu ya ungonjwa au sababu nyinginezo. Lakini hatukuona hofu kwa ajili ya mji, maana kwa namna ulivyojengwa haufikiki ila kwa shida, tena, adui wako mbele yetu wala si nyuma.

Bwana Good na Umslopogaas walikuwa wamefuatana na jeshi, lakini Nyleptha alifuatana na Sir Henry na mimi mpaka mlangoni pa mji, amepanda farasi mweupe mzuri sana jina lake Nuru, aliyesifiwa kuwa mwepesi kuliko farasi wote wa Zuvendi. Uso wake ulionyesha dalili ya machozi ya huzuni, lakini alijikaza kwa uvumilivu wa uchungu pale tulipokuwa tunaagana.

Tulipofika mlangoni, alimsimamisha farasi wake akatuaga. Jana yake alikuwa amewakagua askari na wakubwa, akawatolea hotuba ya maneno ya ushujaa akiwaambia kwamba anawatumaini kabisa ya kuwa kwa ujasiri na uhodari wao hawakosi watashinda, wakatiwa moyo, wakaondoka na huku wanapiga ukulele wa kumshangilia, mpaka ardhi ikatikisika, na leo ikawa kama anafikiri vivyo hivyo, akasema, ‘’Kwa heri Makumazahn! Kumbuka kuwa naitumainia busara yako kutuokoa na Sorais. Najua utafanya wajibu wako.

Kwa heri Bwana wangu! Rudi na hali umeshinda, ama sivyo, uchukuliwe juu ya mikuki ya askari zako’’ (maana ni desturi kuchukua maiti ya mkuu aliyeuawa vitani juu ya namna ya kitanda kilichofanywa kwa mikuki).

Sir Henry hakusema neno, ila alimgeuza farasi wake aende mbele, labda roho yake ilimpanda kooni asiweze kusema. Nyleptha akasema, ‘’Nitasimama hapa hapa kuwapokea mtakaporudi hali mmeshinda. Na sasa Bwana zangu, kwa herini!’’

Basi, tuliondoka, lakini tulipokuwa tumekwenda kadiri ya yadi hamsini hivi, tuligeuka tukamwona amesimama pale pale, anatutazama, ndipo tulipoondoka kabisa.

Tulipokwenda kadiri ya maili moja, tulisikia vishindo vya askari mpanda farasi anatufuata; tukageuka tukamwona mtu anatujia anamwongoza Yule farasi bora Nuru.

Akasema, ‘’Malkia amenituma nimletee zawadi Bwana Inkubu, naye aliniambia niseme kuwa ana mbio na juhudi ya kuendelea kuliko farasi wote wa nchi.’’

Kwanza Sir Henry hakutaka kumpokea, akasema kuwa, si vizuri kumtumia farasi bora kwa kazi iliyo mbele yetu, lakini nilimshauri ampokee, nikijua kuwa Nyleptha ataudhika akimrudisha. Basi alimpokea nakumwambia yule mtu ampe asante Malkia, tuliendelea katika safari yetu.

Ilipopata saa sita tuliwafikia askari wa nyumba ya jeshi letu, na Sir Henry akachukua daraka la kuwa mkuu wa jeshi zima. Tuliendelea bila kupigwa, na kwa kweli bila kuonekana na watu ila wachache, maana wenyeji wote wa miji na vijiji walikuwa wamekimbia wameogopa kuwa watatengwa katikati ya majeshi yanayopigana, na kusagwa kama ngano inavyosagwa katikati ya jiwe la juu na la chini ya kinu cha kusagia.

Siku ya nne jioni, maana mwendo wa jeshi kubwa ni wa pole pole, tulipiga kambi kadiri ya maili mbili upande huu wa kipito nilichotaja, na wapelelezi wetu walituletea habari kuwa Sorais na jeshi lake wanatujia, wamepiga kambi kadiri ya maili kumi upande mwingine wa kipito. Basi, kabla hakujapambazuka, tuliwatanguliza wapanda farasi elfu moja na mia tano ili wakishike kipito.

Mara walipofika, walishambuliwa na kikosi cha wapanda farasi wa Sorais, na vita vikali vikapiganwa. Sisi tulipata hasara ya watu kadiri ya thelathini waliouawa, lakini askari wengine wa upande wetu walipokifikia kikosi cha Sorais, kilirudi nyuma kikiwachukuwa wafu na majeruhi wao pamoja nao.

Jeshi letu kubwa lilifika kipito kwenye saa sita, na lazima nikiri ya kuwa shauri la Nyleptha lilikuwa zuri, maana kipito kile kilikuwa mahali pazuri

sana pa kupigania, na hasa kwa sababu jeshi la adui ni kubwa kuliko letu.

Njia ilipanda kadiri ya maili moja mpaka kufika juu ya mwinuko, kisha iliteremka taratibu mpaka kwenye mto mdogo, kisha ilipanda tena mpaka kufika uwandani. Urefu wa njia toka juu ya mwinuko mpaka mtoni ulikuwa kadiri ya nusu maili, na wa toka mto mpaka juu ya mwinuko upande wa pili, ulikuwa karibuni kupata nusu maili.

Urefu wa mwinuko wa juu ulikuwa kadiri ya maili mbili na robo, ndiyo sawasawa na upana wa kipito ambacho kilipita katikati ya milima yenye misitu minene, na upande huu na huu wa kipito kuna miamba na vichaka vinavyofaa sana kufichia askari.

Basi, Sir Henry alilipanga jeshi lake juu ya mwinuko wa upande huu. Jeshi letu ambalo lilikuwa na askari kadiri ya sitini elfu, Ilipangwa hivi: katikati askari elfu ishirini wa miguu, wenye mikuki, panga na ngao za ngozi ya kiboko walipangwa. Kwa mfano, hao walikuwa kidari cha askari, nao walisaidiwa na askari wa miguu elfu tano na wapanda farasi elfu tatu waliowekwa nyuma yao wawe mfano wa akiba.

Pande zote mbili za kidari hicho, askari wapanda farasi elfu saba walipangwa na pande zao ila kwa mbele kidogo, vikosi viwili, kila kikosi chenye askari wenye mikuki, saba elfu mia tano walipangwa; kikosi kimoja upande huu na kimoja upande huu, na wapanda farasi elfu moja mia tano kila upande. ‘Basi, jumla ni sitini elfu.

Sir Henry alikuwa mkuu wa jeshi zima, mimi nilikuwa mkuu wa askari wapanda farasi elfu saba waliokuwa katikati ya kidari na wale wa upande wa kuume, ambao walikuwa chini ya amri ya Bwana Good, na vikosi vingine vilikuwa chini ya amri ya majemadari wa Zuvendi.

Mara tulipojipanga tu! jeshi la Sorais lilianza kujipanga juu ya mwinuko wa upande ule kadiri ya maili moja mbele yetu, mpaka mahali pote palifunikwa kwa ncha za mikuki, na ardhi ilitikisika kwa vishindo vya miguu ya askari zake.

Ilikuwa dhahiri wapelelezi wetu walituambia kweli, maana jeshi lake ni kubwa kuliko letu. Kwanza tulifikiri kuwa Sorais anataka kutushambulia

papo hapo kwa jinsi wapanda farasi walivyoshughulika huko na huko, lakini vita havikutokea siku hii.

Mchana kutwa tulitazamana tukingojea, lakini hapana jambo lililotokea, na giza lilishuka, na mioto mingi sana iliwaka kila mahali kasha ikafifia tena. Saa zikapita, kukawa kimya sana kati majeshi ya pande zote mbili.

Usiku ule ulichosha sana, maana mambo mengi lazima yatengenezwe, tena hali ya kungojeshwa hivyo ilituudhi mno.

Nilifikiri juu ya vita vya kesho yake jinsi vitakavyokuwa vikubwa mno, na mauaji yatakavyokuwa ya kutisha, nilipotafakari juu ya mambo yanayotegemea vita hivi, niliona shaka nyingi. Tena, ilihuzunisha sana kufikiri kuwa majeshi haya mawili yamekutanika kuangamizana kwa ajili ya wivu na hasira ya mwanamke.

Hii ndiyo nguvu iliyofichika, nayo ndiyo itakayopeleka majeshi ya wapanda farasi wapambane kama umeme ulio hai kupitia lile bonde lililo katikati, na kuyapindua pindua majeshi kama mawingu dhoruba inapopambana na dhoruba nyingine.

Fikira hii ilikuwa ya kutisha mno, nayo iliingiza mawazo moyoni juu ya madaraka ya wakuu wa dunia. Tulikaa hivi tukishauriana usiku, wenye nyuso nyeupe na mioyo mizito, huku walinda zamu wakipita pita huku na huko, na majemedari waliovalia wakaja na kuenda, wakaja na kuenda, kimya kama kivuli.

Basi, wakati ulipita hivyo mpaka kila jambo lilipokuwa tayari kwa mauaji yanayokuja; nikalala na mawazo mengi, nikajaribu kupata usingizi nisiweze kuupata kwa hofu ya kesho maana nani anayeweza kutabiri jambo litakalotokea kesho! Majonzi na mauti ni hakika; ni zaidi ya hayo hatuna habari nazo, na lazima nikiri kuwa niliona hofu.

Basi mwishowe niliacha kutakafari juu ya mambo hayo nikayaacha yale yatakayotokea kesho katika mikono ya Mungu Mwenyenzi.

Basi mwishowe jua jekundu lilichomoza, na majeshi yaliamka kwa kishindo kikubwa na ngurumo yakajikusanya kufanya vita. Matengenezo

yote yalikuwa mazuri ya kutisha, na Umslopogaas alikuwa ameliinamia shoka lake na kuyatazama na huku anachekelea kwa furaha.

Akasema, ‘’Makumazahn, sijaona namna yake, hata mara moja. Vita vya watu wangu vilikuwa kama michezo ya watoto vikilinganishwa na vita hivi namna vitakavyo kuwa. Je, waonaje watapigana hata mwisho?’’

Nikajibu kwa huzuni, ‘’Ndiyo, mpaka kufa. Uwe radhi Inkosikazi atakula shibe yake leo. Basi, wakati ulipita bila kuwapo dalili ya shambulio.

Kundi dogo la wapanda farasi lilipita mbele yetu polepole, na kwa dhahiri lilikuwa likichungulia namna tulivyopangwa na hesabu ya askari wetu, lakini hatukulishambulia, maana tulikuwa tumekwisha kusudia kukaa na kujitetea tu wala si kupoteza hata mtu mmoja.

Askari wetu walikula chakula chao cha asubuhi, wakasimama na silaha zao tayari, na saa zikapita. Saa sita watu walipokuwa wakila chakula cha mchana, maana tulifikiri wataweza kupigana vizuri zaidi kama hawana njaa, tulisikia kelele, ‘’Sorais! Sorais!’’ ilikuwa kama ngurumo ikitokea upande wa kuume wa adui zetu, nikatwaa darubini nikatazama, nikaweza kumwona Sorais mwenyewe anapita polepole mbele ya majeshi yake amezungukwa na wakuu waliokuwa wamevaa vizuri sana.

Na alipokuwa akipita, askari walimpigia ukelele wa shangwe kama ngurumo ya magari elfu kumi, au kama mvumo wa mawimbi ya bahari upepo ugeukapo na kuchukua sauti yake ghafla masikioni mwa mtu anayesikiliza, mpaka ardhi ilitikisika na hewa ilijaa wingi wa sauti.

Basi, tulisikia kuwa hii ndiyo alama ya kuanzisha vita, tukakaa kimya tukijiweka tayari. Wala hatukuwekwa sana. Mara, kama ndimi za moto zitokazo katika mdomo wa mzinga, vikosi viwili vya wapanda farasi vilitoka mbio, wakateremka mwinuko kutujia, kwanza pole pole kidogo, na kuongeza mbio walipokuwa wakija.

Lakini kabla hawajaufikia mto ule mdogo uliokuwa bondeni, Sir Henry aliipeleka amri kupeleka askari elfu tano wapanda farasi wenye panga kuwapiga, maana aliogopa kuwa wakiachiwa kuwashambulia askari wa

miguu wa katikati kwa nguvu zao zote, hawataweza kustahimili. Basi nilipeleka askari wale, nikabaki nyuma pamoja na watu wangu waliosalia.

Basi, askari wale wapanda farasi elfu tano walikwenda wamepangwa mfano wa kabari na kuongozwa vizuri.

Na mkuu wao. Kwanza walikwenda taratibu muda wa yadi mia tatu, wakielekea sawasawa mbele, ndipo yule mkuu wao alipowapeleka ghafla upande wakazidi kupiga mbio, nikaona kabari ile inapinda, na kabla kikosi cha adui hakijaweza kwenda upande au kujizuia, ilikipiga katikati kwa kishindo kikubwa mno.

Kabari ile ya wapanda farasi iliingia mpaka katika moyo wa kikosi, na wapanda farasi adui, walitupwa upande huu na huu kama udongo unavyotupwa jembe linapovutwa na ng'ombe likipita katika shamba, au kama maji ya bahari yanavyotupwa huko na huko kwa omo la merikebu inapokwenda mbio.

Ndani ndani zaidi, na kikosi cha adui kilipinda kama nyoka anavyojipinda aumizwapo ili ailinde sehemu yake ya katikati ndani zaidi. Kumbe watu wetu wemepita na kutokeza upande wa pili, waka geuka wakashambulia tena adui waliotawanyika kama povu mbele ya upepo wenye nguvu, na huku askari zetu wote wanatazama na kupiga kelele za shangwe.

Hata mwishowe, kikosi kile cha adui kilivunjika, kikageuka kikarudi mbio katikati ya farasi wengi wasio na askari, na miali ya panga zinazopungwa huko na huko, na kelele za shangwe za askari waliokuwa wakiwafukuza. Kikarudi mbio kutafuta salama nyuma ya askari wenzao.

Basi, jeshi lililokuwa likija mbele lilifunguka kukipa nafasi ya kuingia, na askari zangu walirud, wamepata hasara ya watu kadiri ya mia tano nami nilifikiri si wengi kwa kadiri ya ukali wa vita vilivyokuwa.

Basi, sasa vikosi vya upande wa kushoto wa adui vilivyokuwa karibu vyote ni vya watu wa Nasta, vilikuwa vikitujia, na huku tukasikia kelele ‘’Nasta’’ na ‘’Sorais’’ tukaona bendera zinapepea, na panga zinapungwa, vikatujia kama makundi ya siafu.

Nilipewa amri tena nijaribu kuwapinga kwa kupeleka vikosi vya wapanda farasi, nikafanya kadiri nilivyoweza kupeleka vikosi vya watu elfu moja.

Vikosi hivyo viliwatia adui kama kisu kinachong'aa na kuingia katika moyo wao, lakini tulipata hasara ya watu wengi, maana sasa askari wa adui hawakushikamana kama katika shambulio la kwanza, ila walifunguka wakaacha nafasi ili wapanda farasi wapite katikati, kisha walijitupa chini wakawakata miguu farasi walipokuwa wakipita.

Basi kadiri tulivyoweza kufanya, adui walizidi kutukaribia, mpaka wakakishambulia kwa nguvu kikosi cha Bwana Good. Tena, wakati huo huo nikasikia kishindo kilichonifaamisha kuwa adui wameshambulia katikati na kwa upande wa kushoto pia.

Nilijiinua katika vikuku vya miguu juu ya farasi wangu nikatazama upande wa kushoto, nikaona mng'aro wa panga zinazopungwa na wa ncha za mikuki inayosukumwa upeo wa macho yangu.

Basi, hapo majeshi yalitikisika huku na huku yakishindana, pengine yakirudi nyuma, pengine yakisukumwa mbele, katika fujo ya kushambulia na kujitetea. Basi, vivyo hivyo vita viliendelea kwa muda wa saa nne bila kituo, na mwisho wa wakati huo tulikuwa haujaendelea mbele wala kurudi nyuma.

Mwishowe mashambulio yalififia na jeshi la Sorais lilirudi, nikaanza kufikiri askari zao wamechoka. Lakini sivyo, sasa Sorais aliwapanga wapanda farasi vikosi vidogo vidogo wakatushambulia kwa nguvu kila mahali, ndipo wakati huo, huo alipopeleka mbele tena jeshi kubwa.

Sorais mwenyewe alikuwa akiamrisha. Basi, wakaja mbele kama mawimbi makubwa yenye nguvu nyingi mno, wakapambana na askari wa katikati ya kidari cha jeshi letu. Basi, askari wa sehemu ya katikati ya jeshi letu walipinda kama upinde, wakafunguka, na kama askari wale elfu kumi wasingalikuwa wamewekwa nyuma kuwategemeza, wangaliangamia kabisa.

Kikosi cha Bwana Good pia kilisukumwa nyuma na sehemu moja ilivunjika, na nusu ya askari wakapotea. Lakini shambulio lilikuwa lenye

nguvu mno na nguvu zake hazikuweza kuendelea hivyo. Mara ikawa kama vita vinageuka, na kwa muda mfupi ilikuwa kama pande zote mbili zimesimama tu.

Ndipo vita vilipoanza kuiendea kambi ya Sorais. Tena, wakati huo huo kikosi cha Nasta kikarudi nyuma, sijui kama askari zake walikata tamaa kwa ajili ya hasara waliyoipata, au kama ni hila waliyofanya.

Lakini hapo, kikosi cha Bwana Good kilipaacha mahali pake kikashambulia na huku kinapiga kelele.

Na mara ile adui waligeuka wakashambulia tena kwa nguvu. Basi, adui walikizunguka kile kikosi kikaangamia kabisa, nikaona kuwa Bwana Good amepanda farasi mkubwa yu katika hatari ya kuuawa.

Baada ya dakika chache kikosi kizima kilitawanyika nami sikuweza kumwona Bwana Good katika mauaji ya kutisha yaliyofuata.

Halafu nikaona farasi mweupe anatoka mbio katika fujo, akanipita mbio hana mtu mgongoni, nikamtambua ni farasi wa Bwana Good. Basi, hapo sikusita zaidi, wala sikungoja kupewa amri, ila niliwaamrisha watu wangu kadiri ya elfu nne au tano, tukawashambulia wale watu wa Nasta wenye panga.

Walituona tunakuja, tena, walionywa kwa vishindo vya miguu ya farasi zetu, wakageuka wakatungojea. Wala hawakukubali kurudi nyuma hata kidogo, tukajaribu kuwakanyaga, tukawapigapiga, tukawatenga lakini walionekana kama wainukao tena, wakawashambulia farasi wetu kwa panga zao kali, wakaikata miguu yao, kisha wakawashambulia askari walipoanguka chini wakawakata vipande vipande.

Farasi wangu akauawa, lakini kwa bahati nilikuwa na mwingine aliyewekwa pamoja na askari nyuma, ikawa sina budi kufanya niwezavyo. Baadaye kidogo nilijiona katikati ya askari wa Bwana Good waliosalia ambao walikuwa wamemzunguka na sasa wanapigana kuyaokoa maisha yao.

Ndipo nilipojikwaa nikatazama chini nikaona rodi ya Bwana Good, alikuwa ameangushwa kigotigoti, na mtu mkubwa sana alikuwa amesimama anapunga upanga mkubwa tayari kumpiga. Sijui namna nilivyoweza, lakini niliwahi kumuua yule mtu kwa sime ya Kijivuni niliyokuwa nayo.

Lakini nilipokuwa nikifanya hivyo alinipiga dharuba moja upande wa kushoto wa kifua, na ingawa nilikuwa nimevaa deraya chini ya nguo zangu, lakini nilitambua ameniumiza vibaya sana.

Kwa dakika moja niliangukia mikono na magoti katikati ya maiti na watu waliokuwa wakifa, na moyo wangu ulielea nikataka kuzirai.

Nilipokuja juu tena, niliona ya kuwa askari wa Nasta, au wale waliosalia, wanarudi nyuma ya mto, na Bwana Good amesimama karibu na huku anachechemea, akasema, ‘’Lo! Tulikuwa karibu kufa, lakini asante tumepona.’’

Nikakubali, lakini nilijua ya kuwa nimeumia vibaya. Basi, hapo tuliona vikosi vyetu vya wapanda farasi wenye panga vya upande wa kuume na vya kushoto vilivyo wekwa nyuma, vikitoka mahali pao kama mishale na kuwangukia askari wa Sorais waliokuwa sasa wametawanyika, na shambulio hilo ndilo lililovimaliza vita.

Baada ya kupita dakika mbili tatu, adui walikuwa wakirudi nyuma kuuvuka ule mto mdogo, wakajipanga huko tena. Kisha, kukawa kimya kidogo, nikawahi kumpata farasi wangu wa pili. Aliyekuwa nyuma, nikapewa amri na Sir Henry kushambulia mbele. Basi hapo tulifanya kelele moja kwa moja, tukazipepea bendera zetu, tukapunga panga na mikuki, tukawafutia adui tukawafukuza.

Tulipokuwa tukipita juu ya chungu za maiti na watu waliokuwa wakikata roho nilimwona mtu mmoja ananijia mbio sana amepanda farasi, akaniita kwa sauti ya hofu! Nikasimama, nikamuuliza ana habari gani.

Akaniambia kuwa ana habari ya haraka sana! akaniambia, ya kuwa Malkia Nyleptha atauawa kwa hila katika jumba la Milosis mara kutakapopambazuka kesho. Aliniambia kuwa askari wa zamu watapaacha

mahali pao, na makuhani watamuua Malkia. Nikashtuka kwa ushangao, nikamuuliza, ‘’Unasemaje?’’

Akasema, ‘’Ni kweli, yule shetani Nasta aliondoka usiku akafanya shauri na Agon. Askari wa zamu wataufungua mlango, na Nasta na makuhani wa Agon wataingia na kumuua Malkia.’’

Basi, nilimchukua yule mtu nikaenda naye mbio mbio mpaka nilipomwona Sir Henry katikati ya wakuu wengine. Mara nilipomwona, askari walikuwa wanaanza kuendelea mbele tena.

Kichwa chake kilifungwa kwa kitambaa chenye damu, lakini niliona ya kuwa macho yake na kama desturi yake, na karibu naye Umslopogaas alikuwa amesimama amelishika shoka lake, jekundu kwa damu, lakini yeye alionekana mzima kabisa.

Sir Henry akauliza, ‘’Kuna nini Quatermain?’’

Nikajibu, ‘’Wanafanya hila kumuua Malkia mara kutakapo pambazuka kesho. Mtu huyu aliyetoroka toka upande wa Sorais alisikia habari za hila wanazotaka kuzifanya.’’

Rangi ya uso wa Sir Henry ilibadilika, akawa mweupe sana, akasema, ‘’Kutakapo pambazuka, na sasa jua linashuka kunapambazuka saa kumi, na toka hapa mpaka huko ni mwendo wa maili mia moja. Tutafanya nini?’’

Basi, nilifikiri shauri, nikamuuliza, ‘’Je farasi wako amechoka?’’ akajibu, ‘’La, ndiyo kwanza nimpande, tena amekwisha kula.’’

Nikasema, ‘’Na farasi wangu pia hajafanya kazi leo. Basi, shuka chini umwache Umslopogaas ampande, tutafika Milosis kabla hakujapambazuka, na kama hatuwahi kufika, basi tumeshindwa.

Sir Henry akataka kwenda pamoja nasi, Nikamwambia! Hapana, hapana, wewe huwezi kuacha vita sasa. Watu wasipokuona watakufa moyo na vita vitapotea. Askari wangefikiri umekimbia. Basi, upesi, upesi.’’

Basi mara ile alishuka, na Umslopogaas alipanda mahali pake. Nikasema, ‘’Kwa heri. Peleka wapanda farasi elfu moja watufuatie baada ya saa moja ikiwezekana tena peleka mkuu apashike mahali pangu umweleze sababu niliyotoka.’’

Akasema, ‘’Utafanya uwezavyo kumwokoa Nyleptha, Quatermain?’’

Nikajibu, ‘’Ndiyo, kadiri ninavyoweza kufanya. Sasa nenda, unaachwa nyuma.’’

Basi, alitutazama mara moja tu, kisha akageuka akawafuata watu wake akaenda upesi kujiunga na askari zake.

Na Umslopogaas na mimi tukatoka mahali pale kama mishale inavyotoka katika upinde, na baada ya kupita dakika chache, tulikuwa tumetoka kabisa mahali pale pa mauaji na harufu ya damu, na sauti za vita zikawa kama mvumo wa bahari ya mbali katika masikio yetu.

SURA YA 21

Tulipofika juu ya mwinuko tulisimama kidogo ili farasi wetu wapumzike kidogo, tukageuka kutazama vita chini yetu. Miali mikali ya jua lililokuwa likishuka liliangaza pote ikapatia wekundu.

Mzee Umslopagaas akasema, ‘’Tumeshinda! Tazama jeshi la ‘Bibi wa Usiku’ linarudi nyuma kila upande, wala halina imani tena, linapindika kama chuma kilichoyeyuka, tena watu wake wanapigana kwa nusu ya mioyo tu.

Lakini, ole wetu, vita havitakwisha kwa kushinda upande huu wala huu, maana giza linaingia na vikosi havitaweza kufuatafuata na kuua!’’ Akatikisa kichwa chake kwa huzuni.

‘’Lakini nadhani askari zake hawatapigana tena, maana wamekwisha ona kuwa nguvu zetu ni nyingi. Ah! I vyema kuishi. Leo nimepata kuona vita vilivyostahili kupiganwa, nami nimeona vita vingi.’’

Basi, huku nyuma tulikuwa tumeianza safari yetu tena, na tulipokuwa tukifuatana kando kando nilimweleza kwa nini tunakwenda Milosis, na jinsi maisha yote yaliyopotea siku hii yatakavyo kuwa yamepotea bure ikiwa hatufanikiwi katika safari yetu, akasema, ‘’Ah!

Lazima tuende mwendo wa maili mia moja kabla hakujapambazuka hali tunao farasi wawili hawa tu! Haya basi, mbio! Mbio! Mwanadamu anaweza kujaribu tu, Makumazahn, na labda tutawahi kufika kwa wakati unaofaa na kumpasulia mbali kichwa yule mchawi (yaani Agon).

Ndiye aliyetaka kutuchoma moto, yule mganga wa kuleta mvua. Na sasa anataka kumtega mama yangu (Nyleptha). Haya, vyema! Hakika, kama mama yangu yu hai au kama amekufa, nitampasulia mbali kichwa mpaka ndevu zake.

Ndiyo, naapa kwa Chaka nitafanya hivi! Akatikisa Inkosikazi alipokuwa akienda. Sasa giza likawa linazidi kuingia, lakini kwa bahati mwezi ulipanda halafu, tena njia ni nzuri.

Basi, tuliendelea mbele, na wale farasi wawili wenye nguvu walituchukua vizuri kwa hatua ndefu zisizobadilika maili kufuata maili. Hatukusema, ila tuliinama mbele shingoni pa farasi wetu tukazisikiliza pumzi zao zinavyovutwa na kujaza mapafu yao makubwa, na vishindo vya kwato zao. Basi, vivi hivi saa baada ya saa.

Halafu niliona ya kuwa farasi mzuri niliyempanda anaanza kupotewa na nguvu. Nikaitazama saa yangu, ilikuwa karibu saa sita za usiku, na tulikuwa tumemaliza zaidi ya nusu ya safari yetu.

Juu ya mwinuko palikuwa na chemchem niliyoikumbuka nikamwashiria Umslopogaas asimame hapo, maana nilikusudia kuwapumzisha farasi zetu na sisi wenyewe muda wa dakika kumi.

Basi, alisimama, tukashuka katika farasi zetu farasi walisimama wanatweta wakisimama kwanza kwa mguu huu halafu huu, na huku jasho linawatoka na mvuke wao ulionekana kama ukungu katika hewa kimya cha usiku.

Basi nilimwacha Umslopogaas awashike farasi, nikajivuta karibu na chemchem nikanywa maji yake matamu. Kisha, nilijitia maji kichwani na mikononi nikarudi, na yule Mzulu akaenda naye kunywa maji.

Kisha, tukawachukua farasi wakanywe maji kidogo tu, wala si zaidi lo! Tulishindana nao mno kuwavuta wayaache maji!

Basi, kisha Umslopogaas alinisaidia nipande juu ya farasi na yeye mtu mwenye nguvu akarukia juu yake bila kuvigusa vikuku vya matandiko yake, tukaianza tena safari yetu. Kwanza taratibu mpaka farasi wakazoea, kisha mbio.

Basi, hivyo tulienda mwendo wa maili kumi tena, ndiyo tulipofika kwenye mwinuko wa mwendo wa maili sita au saba. Mara tatu farasi wangu alitaka kuanguka, lakini alipofika juu ya mwinuko alijikaza tena akaenda mbio kuteremka kwa hatua zilizokatika katika na huku anatweta sana.

Tulikwenda mwendo wa maili tatu nne zile mbio kuliko kwanza, lakini niliona ya kuwa ni juhudi ya mwisho ya farasi wangu.

Basi ghafla alishika sana hatamu katikati ya meno yake akaenda mbio sana kadiri ya yadi mia tatu nne, ndipo aliposita hatua mbili tatu akaanguka kichwakichwa, na mimi nilijitupa mbele yake kadiri nilivyoweza.

Nilifanya haraka kusimama nikamtazama farasi wangu, akanitazama kwa macho ya kusikitisha, kisha kichwa chake kikaanguka akaguna, akakata roho.

Moyo wake ulikuwa umepasuka. Umslopagaas alisimama, nikamtazama kwa fadhaa, maana hata sasa bado mwendo wa maili ishirini, tutafika namna gani kabla ya mapambazuko hali tuna farasi mmoja tu?

Ilikuwa kama haiwezekani, lakini nilikuwa nimesahau nguvu za kupiga mbio za Mzee Mzulu. Bila kusema neno akashuka katika farasi akanipandisha mimi.

Nikamuuliza, ‘’Wewe utafanya nini?’’

Akashika kikuku cha matandiko ya farasi, akajibu, ‘’ Nitapiga mbio.’’ Ndipo tulipoanza tena kupiga mbio kama zile za kwanza.

Yule farasi Nuru alienda mbio na kila hatua alimsaidia Yule Mzulu. Ilikuwa ajabu kumwona Umslopagaas akipiga mbio maili baada ya maili, na midomo yake ikiwa wazi na mianzi ya pua imepanuka kama ya farasi.

Kila maili tano tulisimama ili kupumzika kidogo, kisha tukazidi kuendelea. Baada ya kupumzika mara tatu, nikamuuliza, ‘’Je, unaweza kuendelea au nikuache unifuatie nyuma?’’ Alishika shoka lake akakielekezea kivuli cheusi mbele yetu, nikaona kumbe ni hekalu la jua, nalo halikuwa mbali zaidi ya maili tano. Akasema na huku anatweta ‘’Nitalifikia ama nitakufa.’’

Lo! Maili tano zile za mwisho. Ngozi ya ndani ya mapaja yangu ilichubuka, na kila mara farasi wangu alipojitahidi alinitesa.

Wala si hivyo tu, Nilichoka kwa kazi nyingi na kwa njaa na kwa kukosa usingizi, tena niliumia sana kwa dhoruba ile niliyopigwa upande wa kushoto wa kifua changu, ikawa kama kwamba kipande cha mfupa au kitu kingine kinanichoma taratibu mpaka katika pafu langu.

Tena, farasi maskini Nuru alikuwa karibu kwisha, lakini hatukuweza kukawia, maana dalili ya kupambazuka ilianza kuonekana.

Na sasa mbele yetu tuliona milango ya shaba ya nje ya mji wa Milosis, nikaingiwa na kitisho. Je, wakikataa kutufungulia milango?’’ Nikapiga ukelele na huku nikatoa neno la kifalme, ‘’Fungua! Fungua! Fungua! Tarishi! Tarishi! Ameleta habari za vita!’’

Askari wa zamu akauliza, ‘’Habari gani? Nani wewe unayesafiri upesi hivi?’’

Nikajibu, ‘’Ni bwana Makumazahn na Umslopogaas.

Fungua! Fungua! Nimeleta habari.’’

Basi, milango mikubwa ilifunguliwa kwa kishindo, na daraja la kupita likashushwa, tukapita ndani mbio mbio. Yule askari wa zamu akatuuliza,

‘’Habari gani, bwana wangu habari gani?’’

Nikajibu, ‘’Bwana Inkubu analifukuza jeshi la Sorais kama wingu mbele ya upepo.’’

Ndipo nilipozidi kwenda mbele mbio.

Haya, farasi jasiri juhudi zaidi kidogo tu! Jitahidi kidogo tu mzee Mzulu jasiri mno. Usianguke sasa, Nuru, endelea zaidi muda mfupi wa dakika kumi na tano tu, na wewe mzee Mzulu wa vita kadhalika, na majina yenu yataishi milele katika habari za nchi hii.

Basi, tulipita mbio kwa vishindo katika njia za mji. Sasa tulipita Hekalu la ua, maili moja tu imesalia, maili moja tu.

Ah! Mungu ashukuriwe, sasa tumelifikia jumba, lakini tazama, miali ya kwanza ya mapambazuko inaiangaza dari ya kuba la dhahabu la Hekalu. Je, nitawahi au tendo limekwisha tendwa na njia imezibwa?

Nami nikapiga ukulele nikitaja neno la kifalme, ‘’Fungua! Fungua!’’

Hapana jibu, na moyo wangu ukataka kufifia.

Nikaita tena, na mara hii sauti moja ilinijibu, nikafurahi, maana ilikuwa sauti ya Kara, yule askari mwaminifu wa Nyleptha, ndiye yule aliyepelekwa na Nyleptha kumshika Sorais siku ile alipokimbilia Hekaluni.

Nikasema, ‘’Ni wewe Kara? Mimi ni Makumazahn, waambie askari wa zamu waufungue mlango na kulishusha daraja upesi sana. Upesi! Upesi!’’

Basi hapo kulikuwa kimya kwa muda uliokuwa kama kwamba hauna mwisho, kisha, nusu ya mlango ikafunguliwa tukaingia uani, na pale pale farasi shujaa Nuru alianguka, nikafikiri amekufa.

Niliondoka, nikaiegemea nguzo , nikatazama pande zote. Sikuona hata mtu mmoja isipokuwa Kara, nayeye alionekana kwamba anataabika, na nguo zake zimetatuka tatuka.

Alikuwa ameufungua mlango na kulishusha daraja yeye peke yake. Nikamuuliza, ‘’Je, wako wapi askari wa zamu?’’

Akanijibu, ‘’Sijui. Muda wa saa mbili wakati nilipokuwa nimelala usingizini, nilishikwa, nikafungwa kamba na askari walio chini ya amri zangu, na ndiyo kwanza nimeweza kujifungua. Naogopa, naogopa sana ya kuwa tumesalitiwa.’’

Basi, maneno yake yalinitia nguvu mpya. Nikamshika mkono nikaenda na huku ninasitasita, na Umslopagaas alinifuata huku anapepesuka kama mtu aliyelewa.

Tukapita katika vyumba mpaka katika sebule kuu mpaka chumbani alimolala malkia. Kwanza tulifika chumba cha askari wa zamu hapana hata askari mmoja.

Kwa hakika wamekwisha tenda shughuli yao, nasi tumechelewa! Ukimya na upweke wa vyumba vile vikubwa ulikuwa wa kutisha mno, ukanielemea kama ndoto ovu.

Mbele, mbele katika chumba cha Nyleptha tukajiingiza huku tunapepesuka, tukiogopa mambo tutakayoyaona, tukaona kuna taa inawaka, tena, mtu ameichukua ile taa.

Oh! Mungu ashukuriwe, ni malkia mwenyewe, naye yu salama! Hapa alikuwa amesimama amevaa mavazi yake ya usiku ameamshwa na ghasia zetu za kupenya katika chumba chake, na uzito wa usingizi bado umo machoni mwake.

Akalia, ‘’Nani? Je, kuna nini Makumazahn, ni wewe? Mbona unahangaika hivi? Umekuja kunipa habari za msiba msiba wa bwana wangu ooh usiseme ya kuwa amekufa hakufa!’’ akalia na huku anaipunga mikono yake kwa mojonzi.

Nikasema, ‘’Nilimwacha Inkubu jana jioni amejeruhiwa, lakini anawaongoza askari juu ya Sorais; kwa hiyo moyo wako na utulie.

Sorais amesukumwa nyuma kila mahali, na askari zako wanashinda.’’ Akasema kwa shangwe, ‘’Nilijua, nilijua kuwa askari zangu watashinda; nao walimwita mgeni, wakavitikisa vichwa vyao nilipomfanya mkuu wa majeshi yangu! Ulimwacha jana jioni ulisema, na sasa hakujapambazuka bado! Hakika’’.

Nikasema, ‘’Nyleptha, jivike mavazi yako utupe divai tunywe, uwaite mabibi watumishi wako upesi kama unataka kuyaokoa maisha yako. Upesi! Usisite!’’

Basi, kusikia haya tu akafanya haraka kujitupia mavazi mengine akawaita mabibi watumishi wake, wakaja. Nikamwambia, ‘’Tufuateni kimya.’’ Basi, kwanza tulikwenda katika chumba cha nje, nikamwambia, ‘’Sasa tupeni divai tunywe na chakula maana tuna karibia kufa.’’

Chumba kile kilikuwa cha wakuu wa askari wa zamu na kulikuwa na meza kwa ajili ya wakuu hao.

Na Nyleptha na mabibi, wakatuletea divai na nyama toka kabatini, Umslopogaas na mimi tukanywa, tukaona uzima unaturudia tena. Kisha, nikasema, ‘’Sikiliza Nyleptha, wako mabibi wawili katika watumishi wako unaoweza kuwatumaini kabisa?’’

Akajibu, ‘’Hakika.’’

Nikasema, ‘’Vyema, waambie waende nje mjini, watoke kwa mlango wa upande, wakawaite wanaume waaminifu wowote wawezao kuwapata, na waje pamoja na silaha zao ili kuyaokoa maisha yako.

La usiulize habari sasa, fanya tu nikuambiayo. Kara atawapeleka mabibi na kuwafungulia mlango.’’

Akageuka akachagua wawili wa mabibi wale, akawaambia maneno niliyomwambia, akawapa pia orodha ya majina ya wanaume watakaowaendea. Nikasema, ‘’Nendeni upesi na kwa siri, nendeni, maana maisha yenu yamo hatarini.’’

Basi, walimfuata Kara, ambaye nilimwambia arudi upesi awezavyo akanikute kwenye mlango wa ua mkubwa wa kutokea penye ngazi kuu. Basi, mimi na Umslopogaas tulikwenda huko, na malkia na mabibi, wale wakatufuata.

Na huku tulipokuwa tukienda, tulimega chakula na katika kukimega nilisimulia habari jinsi nilivyojua hatari inayomjia, na jinsi tulivyomwona Kara, na jinsi askari wote wa zamu walivyokuwa wametoroka, naye yupo yeye peke yake pamoja na mabibi watumishi wake tu.

Katika jumba lile kuu, na yeye aliniambia ya kuwa habari zilivuma mjini ya kuwa jeshi letu limeangamia kabisa, na Sorais anakuja Milosis kwa shangwe, na kwa maneno hayo wanaume wote walimwacha.

Basi, ingawa mambo haya yamechukua muda mrefu kuyasimulia, lakini tulikuwa tumo jumbani kadiri ya dakika sita au saba tu, na ingawa dari ya Hekalu ambayo ni ndefu sana ilikuwa imaangazwa na miali ya jua, lakini hakujapambazuka bado, wala hakutapambazuka ila baada ya dakika kumi hivi.

Basi sasa tukawa katika ua na hapo jeraha liliniuma hata nikawa sina budi kumshika mkono Nyleptha, na Umslopogaas alitufuata kwa shida na huku anakula.

Sasa tulikuwa tumevuka ua, tumefika mlango mwembamba katika ukuta unaotokea penye ngazi kuu. Nilichungulia nikashangaa.

Mlango wa mbao umekwisha ondolewa, na milango ya shaba ya nje pia imekwisha ondolewa. Ilikuwa imeondolewa kabisa katika bawaba zake na kutupwa chini kabisa kadiri ya futi mia mbili.

Basi, pale mbele yetu palikuwa na nafasi ile ya juu ya ngazi kuu, na vile vipandio kumi vya marumaru nyeusi basi!

SURA YA 22

Tulitazama nikasema, ‘’Waona, wameuondoa mlango. Je, hakuna kitu tunachoweza kukitumia ili kuuziba mlango huu? Sema upesi maana

watatufikia kabla hakuja pambazuka.’’

Nilisema hivi kwa sababu nilitambua kuwa lazima tupalinde mahali hapo kwa sababu hapakuwa na milango mahali pengine katika jumba, maana vyumba vimetengwa kwa mapazia tu.

Tena, nilijua kuwa tukiweza kupalinda mahali hapo hapana mahali pengine wauaji wanapoweza kuingilia jumbani; maana jumba halifikiki kabisa isipokuwa kwa ule mlango wa siri alioingilia Sorais usiku ule alipojaribu kumuua Nyleptha, na tangu usiku ule umekwisha zibwa na waashi.

Nyleptha, kama ilivyo, desturi yake, aligundua shauri, akasema, ‘’Najua upande wa pili wa ua viko vipande vya marumaru vilivyokatwa tayari watu wakazi walivileta kufanya msingi wa sanamu ya Bwana wangu Inkubu na tuvitumie hivyo kuuziba mlango.’’

Basi, nikaona shauri lake ni jema, nikampeleka mwanamke mmoja mtumishi ambaye baba yake ni tajiri mwenye watu wengi wa kazi, ajaribu kufanya shauri naye kutusaidia.

Tena, nikamweka mwanamke mwingine mtumishi asimame mlangoni, nasi tukauvuka ua kuvitazama vile vipande vya marumaru, hapo tukamkuta Kara ambaye alikuwa amekwisha watuma wale wanawake watumishi wawili wa kwanza.

Vipande vya marumaru vilikuwa vikubwa, na vingine vilikuwa vinene kadiri ya inchi sita, na uzito wake kadiri ya ratili themanini.

Tena kulikuwako namna ya machela zilizotumika kuyachukulia mawe yale, nikawapa kazi wanawake wanne waanze kuyachukua mpaka mlangoni. Umslopogaas akasema, ‘’Sikiliza Makumazahn, watu waovu hao wakija, mimi nitailinda ngazi kuu wasiipande mpaka mlango uishe kuzibwa. Kweli kitakuwa kifo cha kiume.

Wala usinikataze rafiki yangu, maana mwisho huu ulibashiriwa na mtu aliyekufa zamani sana.

Mchana ulikuwa mzuri, na sasa usiku na uwe mzuri pia. Tazama, nalala kidogo ili nipumzike. Watu watakapokaribia, niamshe wala si kabla ya wakati huo, maana nitahitaji nguvu zangu zote.’’

Asiseme neno tena, ila alitoka nje akajitupa chini sakafuni, na mara akashikwa na usingizi. Wakati huo na mimi pia nilishindwa na uchovu, ikawa lazima nikae karibu na mlango kusimamia mambo.

Wale wanawake waliyaleta yale mawe, na Kara na Nyleptha wakaanza kuyapanga ili kuuziba mlango.

Lakini ilikuwa lazima kuyachukua mwendo wa yadi arobaini, kisha kurudi yadi arobaini, na ingawa wale wanawake walifanya kazi kwa bidii sana, na wengine walichukua jiwe kubwa mikonononi mwao peke yao, lakini hata hivyo kazi iliendelea taratibu sana.

Mwangaza ukaanza kuzidi, na halafu katika kimya tukasikia vishindo vya watu waliovalia silaha wamefika chini ya ngazi. Ukuta tulioujenga katika nafasi ya mlango ulikuwa na kimo cha futi mbili tu, na kazi hii ilikuwa imechukua muda wa dakika nane, na sasa wamekwisha fika.

Vishindo vilikaribia, na katika mwangaza wa kijivu wa mapambazuko tuliweza kuona mistari mirefu ya watu kadiri ya hamsini wakipanda ngazi. Sasa walikuwa wamekwisha fika kituo cha katikati, na hapo walitambua kuwa kuna mambo yanayotendeka juu, wakasimama dakika mbili tatu kushahuriana, kisha, wakaanza kupanda tena kwa taratibu na kwa hadhari.

Sasa tulikuwa tumefanya kazi kadiri ya dakika kumi na tano, na ukuta ulipata kimo cha futi tatu. Ndipo nilipomwamsha Umslopagaas. Yule mtu mkubwa akaondoka, akijinyosha, akazungusha Inkosikazi kichwani, akasema, ‘’Ni vyema. Najiona kama ni kijana tena.

Nguvu zangu zote zimenirudia, ndiyo, kama taa inayopanda kabla haijazimika. Usiogope, nitapigana vyema, divai na usingizi vimenitia moyo mpya.’’

‘’Makumazahn, nimeota ndoto. Nimeota kuwa wewe na mimi tumesimama katika nyota na kuichungulia dunia chini ya miguu yetu, na wewe ulikuwa

kivuli Makumazahn, maana mwangaza uliupenya mwili wako, lakini sikuweza kuona jinsi uso wangu ulivyokuwa.

Saa yetu imefika ee mwindaji mzee. Basi, na ije. Tumeishi si haba, lakini ningependa kuona vita vingine kama vile vya jana.

‘’Wanizike kwa desturi ya kikwetu, Makumazahn, wayaelekeze macho yangu kuitazama nchi ya Wazulu .’’ akaushika mkono wangu, kisha akageuka tayari kuwakabili adui wanaokuja.

Ndipo niliposhangaa yule mtu wa Zuvendi Kara alipanda kwa utulivu na uthabiti toka katika ukuta ule tunaojenga, akasimama karibu na yule Mzulu, na huku anauchomoa upanga wake.

Yule Mzulu mzee akacheka, akasema,

‘’Je, na wewe umekuja pia! Karibu karibu shujaa! Aha! Namsifu yule mtu anayeweza kufa kiume! Aha! Na nguvu za kuua na kishindo cha silaha! Aha! Tu tayari! Tunainoa midomo yetu kama tai, mikuki yetu inang’aa katika miali ya jua twaitikisa mikuki yetu tuna njaa ya kupigana.

Nani anayekuja kumwamkia Inkosikazi?

Nani anataka kumbusu yeye ambaye matunda ya kubusu kwake ni kufa? Mimi Gotagota, mimi muuaji, mimi mwenye mbio, mimi Umslopagaas mwenye shoka, wa kabila la kizulu, mkuu wa kikosi cha Nkomabakosi mimi Umslopagaas, mwana wa ulimi wa Mfalme, mwana wa Makedama, mimi, wa damu ya Mfalme Chaka, mimi, mshindi wa wasioshindika, mimi, nawaita kama kulungu aitwavyo, nawakaribisha, nawangojea. Aha! Ni wewe, ni wewe!’ Ahahaa!”

Aliposema au kuimba wimbo wake wa vita, wale watu wenye silaha walipanda juu kwa haraka, na katika mwangaza uliokuwa ukizidi niliweza kuwatambua Nasta na Agon, na mtu mmoja mkubwa mwenye mkuki mzito akaruka juu ya vipandio vile kumi vya ngazi mbele ya wenzake akajaribu kumpiga Umslopagaas kwa mkuki wake.

Umslopagaas akauepa, lakini hakuijongeza miguu yake, na kwa hivi kipigo kilimkosa, na mara ile Inkosikazi lilipiga juu ya kichwa cha yule mtu likampasulia mbali kichwa, na maiti yake ikaporomoka ngazini.

Na alipoanguka, ngao yake ya ngozi ya kiboko ilimponyoka Yule Mzulu aliinama akaishika, na huku anaimba. Mara ile Kara shujaa naye akamuua mtu, ndipo yalipoanza mambo nisiyopata kuyaona kamwe.

Adui walipanda juu upesi upesi, mmoja, wawili, watatu pamoja, nao kadiri walivyofika juu, shoka lile lilipiga na upanga ule ulipunga, na adui walifingirika chini maiti au walikufa. Na vita vilipozidi kuwa vikali macho ya mzee Mzulu yalizidi kuwa mepesi na mikono yake kupata nguvu.

Aliita wito wa vita na majina ya wakuu aliowaua, na vipigo vya shoka la kutisha vilianguka imara na sahihi, vikipasuka kila vilipoangukia.

Kila kipigo mtu alianguka na kuporomokea ngazini kwa vishindo. Walimpiga na kumkata kwa panga na mikuki wakimjeruhi mara nyingi mpaka akatapakaa damu mwili mzima.

Lakini ngao ile ilikikinga kichwa chake na deraya alizovaa zilimlinda kiwiliwili, akaendelea kuilinda ngazi akisaidiwa na Yule shujaa mzuvendi.

Hatimaye upanga wa Kara ulikatika, akashikana na adui wakaporomoka ngazini pamoja, akakatwa vipande vipande, akafa kishujaa.

Umslopagaas hakusita wala kugeuka hata kidogo, akazidi kuwapiga adui mpaka wakarudi nyuma wameshangaa, wakifikiri kuwa huyu si mwanadamu.

Sasa ukuta ule wa vipande vya marumaru ulikuwa na kimo cha futi nne na nusu, na moyo wangu ulianza kupata tumaini tena nilipouegemea.

Lakini nilipomtazama Umslopagaas jinsi anavyopigana kwa ujasiri, niliyasaga meno yangu kwa uchungu kwa kuwa sikuweza kumsaidia. Sikuweza kufanya kitu, maana silaha zangu zilikuwa zimepotea vitani.

Na mzee Umslopagaas akaliegemea shoka lake, na ingawa alikuwa tayari kuzimia kwa udhaifu kwa ajili ya majeraha yake, aliwadhihaki, akawaita ‘wanawake’ yule mzee shujaa aliwakabili wote peke yake!

Kwa muda hapana aliyethubutu kumshambulia, ingawa Nasta alijaribu kuwatia moyo, mpaka yule mzee Agon alipoona kuwa ukuta huo utamalizika kujengwa, na hila zake zitashindwa, aliutikisa mkuki wake mkubwa akaruka juu ya ngazi iliyoteleza kwa damu.

Yule Mzulu alizitambua ndevu zake nyeupe akalia,

‘’Ah! Ah! Ni wewe mpelelezi wa wachawi! Njoo, njoo, nakungojea mganga mweupe, njoo! Njoo! Nimeapa kuwa nitakuua, nami nimezoea kutimiza viapo vyangu.’’

Agon akaja kwa nguvu akampelekea Umslopagaas mkuki wake kwa nguvu nyingi hata ukapenya ngao yake ukamchoma shingoni kama kumparaza.

Yule Mzulu aliitupilia mbali ngao yake iliyochomwa kwa mkuki, na dakika ile ilikuwa dakika ya mwisho ya Agon, maana kabla hajaweza kuuchomoa mkuki wake na kupiga tena, Umslopagaas alilia.

‘’Na hiki ni chako, mfanya mvua,’’ akashika Inkosikazi kwa mikono miwili akalipunga juu sana akaliteremsha kwa nguvu, akampasua kichwa mzee Agon, na Agon alikufa, akaporomoka mpaka kwenye maiti za wauaji wenzake.

Na hapo alipoanguka, sauti kuu ilitoka chini ya ngazi, nikatazama juu ya ukuta ule tuliokuwa tukiujenga, nikaona askari wenye silaha wanakuja kutuokoa, nikaitikia sauti zao. Basi, hapo wale waliotaka kutuua waligeuka wapate kukimbia wasiweze, wakauwa wote. Mtu mmoja tu alisalia, ndiye yule mkuu Nasta.

Kwa muda alisimama ameuegemea upanga wake mrefu, kama kwamba amekata tamaa, kisha alilia kwa sauti ya kutisha sana akamrukia yule Mzulu, akaupunga upanga wake kwa nguvu nyingi kukizunguka kichwa chake, akampiga dhoruba moja hata ukapenya deraya ya chuma ukaingia

mbavuni mwake Umslopagaas, na kwa muda kidogo alisimama kama amepooza, na shoka lake lilianguka chini.

Basi, hapo Nasta aliuinua upanga wake tena akaruka mbele ili ammalize Umslopagaas, lakini hakujua jinsi alivyo adui yake.

Maana Yule Mzulu alijitikisa akatoa sauti ya ghadhabu akamrukia Nasta kooni, kama nilivyoona simba aliyejeruhiwa akiruka.

Alimpiga pale mguu wake ulipofika juu ya kipandio cha juu ya ngazi, akamshika kwa mikono yake mirefu kama kwamba ni kamba ya chuma, wakavingirika pamoja wakishindana vikali.

Nasta alikuwa mtu mwenye nguvu nyingi, tena anapigania maisha yake, lakini hakuweza kumshinda yule Mzulu ingawa alijeruhiwa vibaya, maana nguvu zake ni za fahari.

Basi, mwisho ukafika. Nilimwona mzee Umslopagaas akifanya juhudi akasimama wima, akajitahidi akamwinua Yule Nasta na huku anashindana mikononi mwake, akatoa sauti ya shangwe, akamtupa chini apondwe juu ya mawe yaliyoko chini kadiri ya futi mia mbili.

Basi, watu wale walioitwa na watumishi mabibi tuliowapeleka walikuwa wamekwisha fika na sauti kubwa zilitufaamisha kuwa watu wa mji wameamshwa, na wanaume na wanawake pia wanakuja wanataka kuingia.

Wengine katika mabibi hodari wa Nyleptha waliosaidia kuujenga ule ukuta walikwenda wawapitishe katika mlango wa upande, na wengine wakaanza kuubomoa ukuta ule tulioujenga kwa kazi ngumu.

Ukuta ulibomolewa upesi na Umslopagaas akaingia mlangoni amefuatwa na umati wa watu waliokuja kutusaidia.

Yule mzee Mzulu alikuwa wa kutisha sana, amefunikwa kwa majeraha, nikajua kwa macho yake ya kuwa anakufa. Damu ilimchuruzika usoni.

Alikuwa na jeraha shingoni pale alipochomwa na mkuki wa Agon na jeraha jingine mkononi, na katika ubavu wa kuume palikuwa na jeraha la urefu wa

inchi sita pale upanga mkubwa wa Nasta ulipoingilia mpaka ndani kabisa.

Sasa, Yule mzee mkali aliendelea amelishika shoka lake mkononi, na wale wanawake walisahau kuogopa kuona damu, wakampigia kelele za shangwe alipokuwa akipita, lakini asisite wala kuwaangalia.

Huko alikwenda akipepesuka na mikono yake imenyoshwa mbele, na sisi tulimfuata. Alipita katika vichochoro, akazunguka mahali mawe yale yalipokuwapo, akapita katika mapazia ya mlango mpaka katika sebule kubwa ambayo sasa ilikuwa inajaa watu waliokuwa wakiingia kwa mlango wa upande mwingine.

Alipita moja kwa moja katika sebule na huku anaacha alama ya damu nyuma yake, mpaka alipoufikia ule mwamba mtakatifu uliopo katikati, na hapo ikawa kama kwamba nguvu zake zinamwishia, akasimama akaliegemea shoka lake. Kisha, akapaza sauti yake, akasema kwa sauti kuu,

‘’Nakufa, nakufa lakini vilikuwa vita vya kifalme.

Wako wapi wale walioipanda ngazi kuu? Siwaoni. Wewe upo Makumazahn, au umekwisha nitangulia katika mahali pa giza ninakokwenda mimi? Damu inanipofusha naona kizungu zungu, nasikia ngurumo ya maji. Ninaitwa!’’

Ndipo alipoonekana kama kwamba amepata wazo jingine, akalinua shoka lake jekundu akalibusu bamba lake. Akalia,

‘’Kwa heri Inkosikazi. Hapana, hapana, tuta kwenda pamoja, hatuwezi kuagana mimi na wewe. Tumeishi pamoja siku nyingi, wewe na mimi. Hapana mwingine atakayekushika.

‘’Pigo jingine moja tu! Pigo lililonyooka! Pigo lenye nguvu!’’

Akajinyosha urefu wake wote, akapiga ukelele uliotikisa hata moyo, akaliinua shoka lake juu ya kichwa chake kwa mikono yake miwili, akalizungusha kichwani mpaka lilionekana kama ni duara ya nuru.

Ndipo alipolipiga kwa nguvu za kutisha sana juu ya mwamba mtakatifu. Cheche za moto ziliruka juu, na nguvu zilikuwa za ajabu hata mwamba ule wa marumaru ulipasuka kwa kishindo ukavunjika vipande vipande, na kipini chake tu.

Vile vipande vya mwamba mtakatifu vikaanguka chini kwa kishindo kikubwa, ndipo yule mzee Mzulu shujaa alipoanguka chini, amekufa lakini angali ameshika sehemu ya kipini cha Inkosikazi mkononi mwake.

‘’Basi, ndivyo alivyokufa Yule shujaa.’’

Sauti ya mastaajabu na ushangao iliwatoka wote waliyoyashuhudia mambo hayo, kisha mtu mmoja akalia, ‘’Bashiri, bashiri! Ameuvunja mwamba mtakatifu!’’ na hapo pakatokea mnong’ono.

Nyleptha akasema, ‘’Ndiyo, ndiyo watu wangu. Ameuvunja mwamba mtakatifu, na tazama, ubashiri umetimia, maana mfalme mgeni anatawala katika Zuvendi. Inkubu, bwana wangu, amelisukuma nyuma jeshi la Sorais, nami simwogopi tena, naye yule aliyeiokoa taji ndiye atakayeipata.’’

Akageuka akauweka mkono wake begani mwangu akasema, ‘’Na bwana huyu, ingawa alijeruhiwa katika vita vya jana, alisafiri pamoja na yule mzee shujaa ambaye amelala hapa sasa, kwa mwendo wa maili mia moja katikati ya kuchwa jua na kupambazuka kwake ili aniokoe katika hila za watu wenye ukatili.

Ndiyo, naye ameniokoa, ingawa nilikuwa karibu kuuawa, na kwa hivi kwa ajili ya matendo waliyoyafanya matendo ya utukufu ambayo hayapo katika habari za nchi yetu na kwa hivi nasema, jina la Makumazahn na jina la marehemu Umslopagaas, ndiyo, na jina la Kara, mtumishi wangu aliyemsaidia kuilinda ngazi kuu.

Yataandikwa kwa herufi za dhahabu juu ya kiti changu cha kifalme, nayo yatakuwa matukufu siku zote mpaka nchi yetu itakapokwisha.

Mimi, Malkia, nimesema haya.’’

Watu walipoisikia hotuba hii ya uhodari, walipiga vigelegele vya shangwe, na mimi nikasema kuwa tumefanya yaliyotupasa tu, kama ilivyo desturi ya Waingereza na Wazulu, wala si jambo la kusifiwa zaidi na waliposikia haya walizidi kupiga vigelegele vya shangwe.

Ndipo nilipoongozwa na kusaidiwa kuuvuka ua wa nje mpaka chumbani kwangu, ili nilazwe kitandani.

Na nilipokuwa nikienda nikamwona yule farasi shujaa Nuru aliyekuwa amelala chini vile vile alivyolala tulipoingia, nikamwambia wale waliokuwa wakinisaidia waniongoze ili nimtazame mnyama yule mwema kabla hawajamchukua.

Na nilipokuwa nikimtazama, nilistaajabu, maana aliyafumbua macho yake, akakinua kichwa chake kidogo, akalia kidogo.

Nikataka kupiga ukelele wa furaha nilipotambua kuwa hakufa, lakini nilikuwa sina nguvu ya kupiga ukelele.

Hata hivyo, masaisi waliitwa, wakamtunza Yule farasi, na baada ya kupita siku kumi na nne alikuwa amekwisha pona na kupata nguvu tena, naye anasifiwa na watu wote wa Milosis, ambao kila wamwonapo huwaonyesha watoto wao na kuwaambia kuwa huyu ni farasi aliyeyaokoa maisha ya Malkia wetu.

Basi, nililala kitandani, nikaogeshwa, na mavazi yangu ya deraya yakavuliwa. Wale walionisaidia waliniumiza sana waliponivua mavazi, wala si jambo la kustajabia, maana palikuwa na maumivu makubwa katika upande wa kushoto wa kifua na mbavu zangu kwa sababu ya jeraha kuambatana na deraya yangu.

Hapo, sikuwa na habari za mambo mengine mpaka niliposikia vishiko vya wapanda farasi waliofika nje ya jumba baada ya kupita muda wa saa kumi.

Nilijiinua nikauliza kuna habari gani, nikaambiwa kuwa jeshi la wapanda farasi lililotumwa na Sir Henry kumsaidia Malkia limefika toka vitani.

Walikuwa wametoka saa mbili baada ya kushuka jua. Walipotoka, mabaki ya jeshi la Sorais walikuwa wakiukimbilia mji wa Marstuna wakifuatiwa na wapanda farasi wetu.

Sir Henry alikuwa amefanya kambi yake katika kambi ile ile aliyoipanga Sorais usiku uliotangulia, naye alikusudia kuuendea Marstuna asubuhi.

Basi, nilipoyasikia hayo niliona kuwa naweza kufa mwenye moyo mwepesi, kisha sikuwa na habari tena nikazirai. Nilipoamka tena, kitu cha kwanza nilichokiona ni rodi ya Bwana Good, nikasikia sauti yake, ‘’Je, waonaje rafiki yangu?’’

Nikauliza kwa sauti ndogo, ‘’Unafanya nini hapa? Kwa nini hukuenda Marstuna? Je, umetoroka nini?’’ akajibu kwa shangwe, ‘’Marstuna? Ah! Marstuna imepigwa na kutekwa sasa siku saba zimepita umelala umezirai kwa muda wa siku kumi.’’

Nikauliza, ‘’Na Sorais’’ Akajibu, ‘’Sorais! Sorais ni mfungwa, watu wake walimhaini. Analetwa hapa, sijui watamfanya nini, maskini!’’

Nikauliza, ‘’Sir Henry yupo wapi?’’

Akajibu, ‘’Yupo pamoja na Nyleptha. Atakuja kukutazama kesho, mabwana waganga waliona kuwa afadhali asije leo.’’

Basi, kesho yake Sir Henry na Nyleptha wakaja kunitazama, na Sir Henry akanieleza habari zote zilizotokea tangu Umslopagaas na mimi tulipoondoka mbio vitani ili kuyaokoa maisha ya Malkia.

Nikauliza, ‘’Sorais atafanywa nini.’’ Mara uso wa Nyleptha ulikunjika akakasirika, lakini Sir Henry akaanza kusema maneno mengine, akasema, ‘’Nadhani utapata nafuu tena siku hizi hizi.’’

Nikatikisa kichwa changu, nikasema, ‘’La, usijidanganye, labda nitaweza kupata nafuu kidogo, lakini sitapona tena.

Sir Henry, mimi ninakufa. Labda nitakufa polepole, lakini kufa lazima nife. Unajua ya kuwa asubuhi yote nimetema damu? Nakuambia kuwa kuna kitu

kinacho ni choma kwenye upande huu wa pafu langu, naweza kukisikia.

Basi, usihuzunike, nimeishi siku nyingi, na siku zangu za kufa zimefika tayari, ni kama ilivyo desturi kwa kila mwanadamu siku yake ya kufa ikifika hakuna wakuizuia.’’

Basi, hapo Nyleptha akaanza kulia, Sir Henry akabadili mazungumzo, akaniambia kuwa tiyari wamefanya picha ya Umslopagaas ili wachore sanamu kubwa ya marumaru nyeusi mfano wake kuonyesha namna alivyouvunja ule mwamba mtakatifu, tena watatengeneza sanamu kubwa nyingine kwa marumaru nyeupe ya yule farasi Nuru na mimi namna tulivyoonekana tulipofika uani akianguka chini mbele yangu.

Tangu wakati huo nimeziona sanamu zile, maana ninapoandika haya miezi sita imepita tangu vita vilipokwisha, nazo karibu zitakuwa tayari. Ni nzuri sana na hasa ile ya Umslopagaas, ambayo imefanana naye sana.

Ndipo waliponiambia kuwa usia wa Umslopagaas umetimizwa, alizikwa kwa desturi ya Kizulu.

SURA YA 23

Baada ya kupita siku saba tangu Nyleptha alipokuja kunitazama niliweza kupata nafuu kidogo, na Sir Henry alinileta habari kuwa Sorais ataletwa mbele yao katika chumba cha Malkia kwenye saa sita, akaniomba nihudhurie kama nikiweza.

Basi, nilivutwa na udadisi kumwona yule mwanamke mzuri maskini tena, nikaenda na huku ninasaidiwa na watumishi. Nilipofika, watu wengine walikuwa hawajafika bado isipokuwa wakuu wachache tu.

Nilipokwisha kukaa kidogo, Sorais akaletwa na kundi la askari, mzuri, mshupavu, lakini uso wake wa kiburi ulionyesha namna alivyotaabika, alikuwa amevaa mavazi ya kifalme kama desturi, naye ameshika mkuki ule mdogo mkononi mwake. Halafu kidogo Nyleptha akaja amefuatana na Sir Henry, na Bwana Good, wakakaa.

Nyleptha alikaa kimya kidogo, kisha akasema, ‘’Salamu Sorais dada yangu! Tazama jinsi ulivyo upasua ufalme wetu kama kitambaa, umewaua watu wangu elfu nyingi, umefanya hila ovu mara mbili kuniua, tena, umeapa kumuua bwana wangu na wenziwe na kunitupa mimi toka juu ya ngazi kuu mimi chini yake.!

Kweli dada yangu nini kimekupata hata ufikirie kuniua? Ni wivu tu wa mapenzi ulio tutenganisha? Au kuna kitu kingine! Je, unalo neno la kusema kutoa sababu usiuawe? Sema, ee Sorais!’’

Sorais akajibu kwa sauti thabiti, ‘’Sina neno la kusema ila laiti ningalishinda kuliko kushindwa. Basi, nifanye upendavyo.’’ Akajivuta juu akaukunja uso wake na huku anauchezea ule mkuki mdogo wa fedha.

Nyleptha akasema, ‘’Sorais, tangu mwanzo nimekuwa dada mwema kwako. Watu walipozungumza juu ya habari za kuwapo Malkia wawili, mimi niliwaambia waache ukae kitini pamoja nami, maana tulikuwa mapacha ingawa mimi nilizaliwa kwanza.

Tulipokuwa watoto tulicheza pamoja tulilala kitanda kimoja na huku tumekumbatiana, na kwa hiyo moyo wangu unakuonea huruma sana hata naumia kwaajili yako. Sorais, kwa uovu wa mambo uliyoyafanya wewe ukiwa hai nchi haitakuwa na amani. Lakini hata hivyo hufi, maana bwana wangu mpenzi ameomba usiuawe.

Basi, nakutoa na kukuweka katika mikono yake akufanye apendavyo.’’

Sorais alibadilika rangi, asiseme neno. Kisha Sir Henry akasema, na huku anamtazama Bwana Good.

‘’Nafahamu ya kuwa wewe ulimpenda Malkia Sorais, sijui namna unavyoona sasa. Lakini labda mambo yatakwisha vizuri ukimwoa. Anazo mali zake na nchi zake mwenyewe, na sisi hatutamdhuru.’’

Bwana Good akajibu, ‘’Kwangu mimi, naweza kusahau mambo yote yaliyopita, yaani ikiwa yeye atanikubali. Ni tayari kumwoa hata kesho, nami nitajaribu kuwa mume mwema kwake.’’

Basi, sasa watu wote walimtazama Sorais, na huku yeye amesimama na kutabasamu kidogo. Kisha akamtazama Nyleptha akasema, ‘’Nakushukuru ee dada yangu Malkia mwenye huruma, na kwa ajili ya mapenzi yote ulionionyesha tangu utoto wangu.

Ustawi, amani na neema ziandamane na njia zako. Uishi na kutawala siku nyingi, ee Malkia mkubwa mtukufu, na upendo wa mume wako uhifadhiwe, na watoto wako wanaume na wanawake wawe wengi.

Nakushukuru bwana wangu Inkubu Mfalme nakushukuru kwa kuwa umeikubali zawadi na kuitia tena katika mikono ya mwenzako Bwana Bougwan.

Mwisho, nakushukuru sana wewe Bwana Bougwan kwa kuwa umekubali kunipokea tena.

Nakushukuru mara elfu, wewe ni mtu mwema mwaminifu. Na sasa nimekwisha kuwashukuru wote, ninalo neno moja la kusema.

‘’Malkia Nyleptha, huwezi kunifahamu hata kidogo ukifikiri nitaridhika na mambo yalivyo. Naidharau huruma yako, tena, nakuchukia kwa ajili yake. Natupa mbele yako misamaha yako kana kwamba ni nyoka na mimi niliyesimama hapa, nimesalitiwa, nimeachwa nimetukanwa, mimi peke yangu nitakushinda.

Namdhihaki, namchukia kila mmoja wenu. Na hili ndilo jibu langu.’’ Na mara ile kabla mtu hajaweza kukisia anachotaka kufanya, alijichoma kwa mkuki wake mdogo wa fedha aliouchukua mkononi, akajichoma mbavuni kwa nguvu nyingi, akaanguka chini.

Nyleptha alipiga ukulele wa uchungu, na Bwana Good akataka kuzimia, na sisi sote wengine tukamkimbilia Sorais.

Lakini ‘’Bibi wa Usiku’’ alijiinua akauegemea mkono mmoja, akautazama uso wa Sir Henry kwa macho yake mazuri dakika moja, kama kwamba anataka kumwambia neno, kisha kichwa chake kikaanguka chini, akaugua, na roho yake ikamtoka.

Siwezi kueleza hali iliyotokea hapo! Maskini Bwana Good maana aligeuka kama mfu.

Basi, alizikwa kwa desturi ya kifalme, na huu ndio mwisho wake. Baada ya kupita mwezi mmoja tangu mambo hayo yalipotokea, palikuwa na tamasha kuu katika Hekalu la Ua, na Sir Henry akatawazwa kuwa mfalme wa Zuvendi.

Mimi sikuwapo, maana ugonjwa ulinizidi sana, lakini Bwana Good alikuwapo akanieleza habari za mambo yaliyofanyika.

Aliniambia kuwa Nyleptha alikuwa mzuri sana, na Sir Henry akaonekana kuwa Mfalme halisi, na watu wote walimshangilia na kumfurahia.

Tena, aliniambia kuwa yule farasi Nuru alikuwa katika andamano, na watu wote walikuwa wa kiimba ‘’Yu wapi Makumazahn yu wapi Makumazahn!’’ mpaka sauti zao zilipwea, wala hawakukubali kunyamaza mpaka walipoambiwa kuwa ungonjwa umemzidi, na kwa hivyo hukuweza kuja.

Basi, baada ya mambo hayo, niliomba nihamishwe katika nyumba ninamokaa sasa ninapoandika maneno haya. Ni nyumba nzuri mwendo wa maili mbili kutoka mji wa Milosis. Miezi mitano imepita tangu nilipohamishiwa hapa, na wakati huo wote nimelala kitandani na kujizungumza kwa kuyaandika maneno haya yanayosimulia habari za safari yetu.

Labda habari hizi hazitasomwa na mtu, lakini si kitu, maana kazi ya kuziandika imenisaidia kuvumilia maumivu ya saa nyingi. Lakini namshukuru Mungu ya kuwa saa nyingi hazibaki sasa.

Tangu nilipoyaandika maneno hayo ya juu, juma moja limepita, na sasa naitwaa kalamu yangu mara ya mwisho maana najua mwisho wangu u karibu. Akili zangu bado zi timamu, na hata sasa ninaweza kuandika lakini kwa shida sana.

Maumivu katika pafu langu yamenizidi sana juma hili, lakini sasa yametulia na naona kama upande huu wa pafu langu umekufa ganzi. Tena, pamoja na

maumivu, hofu ya kufa imeniondokea, naona kama kwamba ninakwenda kulala katika mikono ya raha isiyoelezeka.

Mambo yote yanabadilika machoni pangu. Giza linakaribia na mwangaza unafifia. Lakini ni kama kwamba naweza kulipenya giza, na hata sasa ninaanza kuona shangwe ya watu wengi waliokwisha fariki walio tayari kunipokea.

Mtoto wangu Harry naye yupo pamoja na wengine, na zaidi ya wote ni mke wangu mpenzi, Yule mwanamke mzuri kuliko wote walionifurahisha kwenye dunia hii.

Jua linashuka na kulifanya kuba kubwa la Hekalu kuwa kama moto mkubwa unaowaka, na vidole vyangu vinachoka. Basi, kwa wote walionijua au waliozijua habari zangu, na wote wanaoweza kumkumbuka mzee mwindaji kwa huruma, naunyosha mkono wangu toka nchi ya mbali na kuwapa kwa heri.

Na sasa naiweka roho yangu katika mikono ya Mwenyezi Mungu aliyenileta duniani. Na kama wasemavyo Wazulu, ‘’Nimesema.’’

SURA YA 24

Mwaka mzima umepita tangu rafiki yangu mpenzi Allan Quatermain alipoliandika neno lile ‘’Nimesema’’ mwisho wa taarifa ya mambo yaliyotupata.

Nisinge penda kuyaongeza maneno yake, lakini kwa namna ya ajabu ipo, njia ambayo kwayo labda maandiko yake yataweza kupelekwa Uingereza.

Kweli ni jambo la kubahatisha tu, lakini Bwana Good na mimi tunafikiri afadhali na tubahatishe, kwa muda wa miezi sita wameshughulika katika mipaka ya Zuvendi ili waone kwamba ziko njia nyingine za kutokea na kuingilia katika nchi hii, na moja imeonekana.

Njia hii ndiyo ile aliyopita Yule mtu maskini aliyefika kwa Bwana Mackenzie, nayo ilijulikana na makuhani wa nchi tu, wakaificha kabisa.

Sasa njia hii itazibwa kabisa, lakini kabla ya kuiziba tunapeleka tarishi ayachukue maandiko ya Bwana Allan Quatermain na barua kadha wa kadha toka kwa Bwana Good, kwa rafiki zake, na toka kwangu kwenda kwa ndugu yangu George Curtis.

Nasikitika sana ya kuwa sitamuona tena ndugu yangu, na katika barua yangu namwambia kwa kuwa yeye ni mrithi wangu, basi azichukue mali zangu zote.

Lakini sasa nataka kuongeza maneno kidogo juu ya mzee Quatermain. Alifariki asubuhi na mapema siku iliyofuata ile ambayo aliyaandika maneno ya mwisho ya sura iliyotangulia. Nyleptha, Bwana Good na mimi tulikuwapo alipofariki.

Saa moja kabla hakujapambazuka ilikuwa dhahiri ya kuwa anakufa, tukahuzunika mno.

Kulipopambazuka, aliomba ainuliwe aweze kulioa jua mara ya mwisho linavyotoka, akalitazama sana kwa muda, kisha akasema, ‘’Katika muda wa dakika chache nitakuwa nimekwisha ipita milango ile ya dhahabu.

Ninakwenda safari ya ajabu kupita zile zote tulizokwenda pamoja. Mungu awabariki, nitawangojea huko.’’ Akaugua, akalala, akafariki dunia.

Basi, hivyo ndivyo alivyo fariki mtu ambaye nadhani tabia yake ilikuwa nzuri kuliko tabia za watu wote niliopata kuonana nao. Bwana Good alisoma ibada ya kuzika wafu, na Nyleptha na mimi tulikuwapo.

Kisha kwa kuwa watu wote waliomba sana, maiti yake ilichukuliwa kwa sherehe nyingi na kuchomwa moto kama ilivyo desturi ya Wazuvendi.

Basi, dakika chache kabla ya kushuka jua, maiti iliwekwa juu ya milango ya shaba mbele ya madhabahu, tukasimama huko kuungojea mwali wa mwisho wa jua linaloshuka.

Halafu mwali wa mwisho ulipenya dirishani, ukauangazia uso wake kama mshale wa dhahabu, ukafanya kama taji ya dhahabu juu ya paji lake, ndipo

panda zililia, na milango ilifunguka, na maiti ya rafiki yetu mpenzi ilianguka chini motoni .

Basi, huu ulikuwa mwisho wa maisha ya ajabu ya mwindaji Quatermain. Tangu mambo hayo yalipotokea, tumestawi sana.

Bwana Good anashughulika kuunda merikebu za vita za kusafiri katika ziwa la Milosis, na ziwa jingine, na kwa merikebu hizo tunatumaini kuzidisha biashara na kuwatuliza watu wengine wenye matata wanaokaa kando kando ya maziwa hayo.

Maskini Bwana Good! Mara nyingi huuzunika sana kwa kile kifo kibaya cha Malkia Sorais, maana alimpenda sana.

Lakini natumaini ipo siku machungu yake yataisha na kuhuzunika kwake kutaisha. Maana Nyleptha anamtafutia mke atakayemfaa. Na kwa habari zangu mimi, nadhani afadhali nisijaribu kuzisimulia, maana sijui nianzie wapi.

Cheo changu cha Kifalme kina madaraka makubwa sana, lakini natumaini kufanya mema siku zote, nami nimekusudia mambo mawili makubwa, yaani kuunganisha sehemu mbalimbali za wenyeji chini ya serikali yenye nguvu, na kuzipunguza sana nguvu za makuhani.

Na baadaye, Mungu akinijalia, natumaini kuweka tayari njia ya kuiondoa dini isiyo ya akili ya kuliabudu jua na kuingiza dini ya kweli ya Kikristo.

Kwa heri,

HENRY CURTIS.

Nilisahau kusema ya kuwa zamani za miezi sita, Nyleptha alijifungua mtoto mwanaume mzuri sana nadhani atakuwa mrithi wangu.

HC.

MAELEZO YA BWANA GEORGE CURTIS

Hati ya maandiko hayo yenye anwani yangu iliyoandikwa kwa mkono wa ndugu yangu mpenzi Henry Curtis ambaye nilifikiri kuwa amekwisha kufa, iliwasili salama. Ilichukua muda wa miaka miwili kinifikia.

Nimeyasoma kwa ushangao, na ingawa sasa nimefarijika kujua kuwa yeye na Bwana Good wako hai, lakini kwa jinsi wanavyokaa katika nchi ile ya mbali naona ni kama kwamba wamekwisha kufa.

Wamejitenga na Uingereza na rafiki na jamaa zao milele.

Namna hati hii ilivyopata kunifikia sijui, lakini naona kwamba yule tarishi aliyetumwa alimkabidhi bwana mmojawapo aliyeitia katika posta. Barua zile alizozitaja ndugu yangu hazikuniwasilia, na kwa hivi naona zimepotea njiani.

GEORGE CURTIS.

MWISHO.